ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.

19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.

21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.

33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.

44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais

64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Saba – Tarehe 19 Juni, 2010

Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Thuwaibah Edington Kissasi) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZENI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Mkamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala (Mhe. Haji Mkema Haji): Mhe. Mwenyekiti, naomba Kuwasilisha Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Huhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Zakia Omar Juma): Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 67

Uandikishaji Kwenye Daftari

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Katika zoezi la Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura pamoja na jitihada za Tume ya Uchaguzi kuendesha zoezi hilo kwa awamu tofuati bado wapo wananchi wengi waliokosa kujiandikisha kutokana na sababu mbali mbali na hivyo kutokuwemo katika Daftari jipya lililoboreshwa la mwaka 2010.

(a) Je, hadi kumalizika kwa zoezi hilo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imeandikisha Wapigakura wangapi?

(b) Inaonekana wazi kuwa takwimu za Wapigakura kwa Uchaguzi wa 2010 zitakuwa ndogo kuliko zile za 2005. Je ni sababu zipi za msingi zilizofanya takwimu za mwaka huu kushuka kiasi zilichoshuka?

(c) Kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi tatizo moja lililosababisha Wazanzibari kutoandikishwa ni kukosa kitambulisho cha Ukaazi cha Mzanzibari (Zanzibar ID). Kwa nini ID iwe kikwazo ilhali kisheria kila Mzanzibari aliyetimza miaka 18 analazimika kuwa nayo; na kutokuwa nayo ni kosa?

(d) Kwa nini wale watu wanaokwaza wananchi wenzao kupata ID kwa maksudi wasichukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nam. 67 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri nilivyokuwa nikifanya majumuisho ya baadhi ya maswala ya waheshimiwa suala hili nilijaribu sana kuweza kulitolea ufafanuzi. Lakini pamoja na jawabu zile pia naendelea kumjibu Mheshiwa Mwakilishi swali lake.

a) Mhe. Mwenyekiti, hadi kumalizika kwa zoezi hilo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imeandikisha wapiga kura 408,401.

b) Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kuwa takwimu za wapiga kura kwa uchaguzi wa mwaka 2010 zitakuwa ni ndogo kuliko zile za mwaka 2005, sababu za msingi zilizofanya takwimu za mwaka huu kushuka ni hizi zifuatazo:-

1. Kwa umakini wa uandikishaji wa wapiga kura Tume imeweza kuandikisha zaidi ya asilimia 80.

2. Kwa kuwa suala la uandikishaji ni haki ya hiari ya kimsingi ya mpiga kura kwa hivyo mtu anaweza akenda kujiandikisha na anaweza vile vile kwa makusudi asiende kujiandikisha

3. Kutokana na Teknolojia iliyotumika imezuwia mtu mmoja kujiandikisha zaidi ya mara moja katika kituo zaidi ya kimoja

c) Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (ID) au (ZEN ID) iwe kikwazo ilhali sheria ya kila Mzanzibari aliyetimiza miaka 18 analazimika kuwa nayo na kutokuwa nayo ni kosa. Hii inatokana na watu kukosa kufuata taratibu zinazohusiana na upatikanaji na umilikaji wa kitambulisho hicho.

d) Mhe. Mwenyekiti, wale watu wanaowakwaza wadau wenzao kupata ID kwa makusudi wasichukuliwe hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria. Hii inatokana watu hao kutopeleka madai au malalamiko yao kwenye vyombo vya sheria kudai haki zao.

Kwa hivyo mtu yeyote ambaye anazuia kupata hati yake ya kimsingi na sio ya kitambulisho cha Uzanzibari, lakini haki yake yoyote mtu ambayo anahisi hii ni haki yangu anazuiwa basi vyombo vya kisheria vipo aende kupeleka malalamiko yake na hatua za kisheria zitachukuliwa. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Tulipata taarifa kwamba Tume iliwagundua watu waliojiandikisha kwa makusudi au kwa bahati mbaya zaidi ya mara moja, naomba kujua Tume ilichukua hatua gani; na

(b) Hivi sasa baada ya kumalizika kwa taratibu za uandikishaji Tume tayari imepeleka orodha za wapiga kura majimboni au vituoni kwa ajili ya uhakiki. Zoezi linaendelea la kini baadhi ya majina yameparaganyika, jina la kitu hiki limekwenda kituo hiki. Je Tume itawasaidia vipi wananchi kupata taarifa ili baadaye iseje ikawa tatizo huko mbele.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Ni kweli Tume ya Uchaguzi baada ya zoezi la uandikishaji wa Daftari kuna baadhi ya watu wajanja ambao walijaribu kuijaribu Tume. Kwa sababu kutokana na teknolojia tuliyokuwa nayo sasa hivi huwezi kujiandikisha mara mbili bila ya kugundulikana. Kwa hiyo wananchi tu kwa utashi wao pengine walikuwa wanajaribu tu, mimi siamini

kwamba mtu alikuwa. anataka kufanya *double registration*. Lakini alikuwa anaijaribu kweli nitaweza kugunduliwa. Kwa hivyo hilo zoezi limefanyika na hao watu tayari wamegundulikana. Kama nilivyosema hatua ya mwanzo kwanza jina lake linaondolewa linabakishwa moja. Hatua ya pili taratibu za kisheria zipo, unapokiuka taratibu za kimsingi za Tume ya Uchaguzi hatua za kisheria zitachukuliwa. Moja katika hatua za kuchukuliwa za kisheria watu hawa watapandishwa Mahakamani na kujibu hayo makosa yao.

(b) Hivi sasa kuna uhakiki wa majina ambayo ya watu waliojioandikisha, yanawekwa katika vituo walivyojiandikisha watu wanakwenda kuhakikisha kama majina yao yapo na kama hayapo wanapeleka malalamiko yao Tume ya Uchaguzi ili kuangalia kama kuna hizo karoro zilizojitokeza. Mhe. Hijja anasema kwamba kuna baadhi ya watu jina lake limetoka katika kile kitua kituo alichojiandikisha kwenda katika kituo chengine.

Hiyo ndio madhumuni hasa ya kuweka ile *dispay* kuhakikisha mtu kwamba ile haki yake anahakikishe kwamba ataitumia pale alipokusudia asijeakapelekwa pahala ambapo alipokuwa hajakusudia. Hiyo ndiyo kazi yenyewe ambayo inafanywa kila Mzanzibar ambaye ametimiza masharti, amejiandikisha tunaomba na tunaoa wito kwa wananchi wote ambao waliojiandikisha waende wakaangalie majina yao. Kama jina lako hulioni unapaswa uende Tume ya Uchaguzi na kwa kuwa kuna kipande ulichopewa kile ndio kitakachokuwa na vielelezo vyako vyote, umeandikisha pahala gani na kura yako utapiga pahala gani.

Zaoezi hili la *display* likishamaliza mtu sasa asije akaleta lawama. Kwa hiyo naomba sana na sisi Waheshimiwa ambao wanachama wetu ndio ambao tunategemea watatupigia kura, tuwashajihishe, sio tuende sisi vituoni tukawachagulie majina hapana bali tuwashajihishe wao wenyewe waende katika vituo vile ili wakaangalie majina yao.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Waziri alipokuwa akieleza alieleza kwamba sababu ya idadi hii kuwa ndogo umakini, haki ya hiari, na imezuia watu kujiandikisha mara mbili. Taarifa tulizozipata kutokana na Mkurugenzi wa Vitambulisho kwamba watu wenye vitambulisho mpaka siku ya kufungwa kusimama kuandikishwa ni laki tano na hamsini elfu, mia tano na kumi na tano (550,515,000). Sasa kwa

mujibu wa hesabu ya Mhe. Waziri kuna watu wana vitambulisho laki moja na hamsini na mbili elfu, mia moja na kumi na nne (152, 114) hawakuandikishwa. Je, tuseme kwamba vitambulisho vimetolewa ovyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kwamba vitambulisho vilivyotolewa na Idara ya Vitambulisho kupitia kwa Mkurugenzi ni kama hiyo aliyoitaja laki tano na hamsini elfu mia tano na kumi na tano.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba zuezi hili la kujiandikisha ni suala la hiari. Wamo watu humu wanavyo vitambulisho vya Uzanzibari lakini kwa makusudi anasema mimi sitaki kwenda kujiandikisha kupiga kura. Kuwa na kitambulisho cha Uzanzibari ni haki yake ya kisheria. Kwa mujibu wa sheria zetu kama Mzanzibari umeshatimiza sifa zote hujakuwa na kitambulisho ni kosa kisheria.

Lakini unaweza ukawa na kitambulisho cha Uzanzibari lakini kama hujenda kujiandikisha hilo sio kosa kwa sababu kujiandikisha kupiga kura ile ina maana ni hiyari ya mtu. Kwa hiyo inawezekana wamo watu ambao yatari wanavyo vitambulisho vya Uzanzibari lakini kwa makusudi tu hawakwenda kujiandikisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hivi karibuni kuna baadhi ya vijana niliwahi kukutana nao na katika kukutana nao nikajaribu kuwauliza. Kwa sababu tuna utaratibu sasa hivi lakini huo ni utaratibu wa ndani ya Chama cha Mapinduzi, kama mtu hukujiandikisha basi hutoweza kupiga kura ya maoni kumchagua Mwakilishi wako. Sasa kuna baadhi ya vijana wakasema aah! Mimi watu walipokuwa wakijiandikisha nilikuwa sipo. Kitambulisho cha Uzanzibar anacho na huyo tena ni CCM lakini hakwenda kujiandikisha.

Kwa hiyo mimi nakubaliana na Mhe. Juma Duni Haji wapo wananchi ambao pengine kutokana na taaluma ndogo hawakuipata au wenyewe uwelewa wao unakuwa mdogo, wanavyo vitambulisho vya Uzanzibari lakini wameshindwa kwenda kujiandikisha katika daftari la kudumu la kupiga kura.

Mhe. Zakia Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Pamoja na majibu yake pengine ni mazuri lakini kwa sababu zijaridhika. Pamoja na kwamba anasema pengine hajapenda tu mwenyewe kujiandikisha sasa sisi tunao wengi ambao wamependa kujiandikisha na wamefika kwenye vituo vya kujiandikisha lakini hawakuandikishwa na sifa zote wanazo, vyeti

vya kuzaliwa, wengine wana wajukuu mikononi waliyokuwa hawana vyeti, kuonesha kwamba wao ni watu wazima hao unatwambia Mhe. Waziri tuwafanyeji ili waweze kupata haki yao. Kwa sababu wao wanataka kuandikishwa na hawajaandikishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Tume ya Uchaguzi, wamejitahidi sana. Mimi nadhani karibu mwaka mmoja nyuma siku zote tulikuwa tunajibu maswali hapa watu watafute vitambulisho waliokuwa hawana na tunashukuru waheshimiwa wengi walifanya jitihada zao za makusudi kwenda kuwashajihisha wale ambao hawana vitambulisho yaani hawana vyeti vya kuzaliwa.

Suala la kusema mtu ana mjukuu bado kisheria halijakuwa la kuweza kumpa nguvu ya kuweza kupata haki zote. Mtu hata kama ana mjukuu sheria zetu zinasema kuna wazee ambao katika hiyo miaka ya nyuma waliyozaliwa hawakuwahi kupata vyeti vya kuzaliwa, wale wanatakiwa waende Mahakamani wakale kiapo na wapo wengi ambao walikuwa hawana vyeti vya kuzaliwa wamekwenda Mahakamani wamekula kiapo na tayari wamepata haki yao na wamepewa vyeti na wamepewa na vitambulisho vya Uzanzibari. Lakini sasa ndio kama hivyo ninavyozungumza kwamba uwelewa bado, kuna watu wengine uwelewa unakuwa mdogo.

Nataka nirejee suala la Mheshimiwa kwa sababu hivi kwa sababu tume ya Uchaguzi ilikuwa ina programu yake tumekwenda zoezi la uandikishaji mara ya mwanzo, tumekwenda zoezi la uandikishaji mara ya pili, tumerejea tena mara ya tatu kwa dharura ili wale ambao hawajakamilisha taratibu waendelee kukamilisha taratibu na katika kipindi chote hicho walikuwa wanajitahidi na wamo watu katika kipindi hicho walipata nafasi wakatimiza yale masharti wakaingizwa ndani ya daftari la kudumu la kupiga kura.

Mimi nadhani kwa asilimia 80 tuliyojiandikisha tumepiga hatua kubwa sana, ukilinganisha hata hayo mataifa ya Ulaya hawafikii asilimia. Sasa hawa waliobaki mimi nadhani wastahamili tukijaaliwa kwa kuwa wanavyo vitambulisho vyao basi uchaguzi sio mwaka huu tu mwaka 2010 uchaguzi ipo mwaka 2015 mwaka 2020 na mwaka 2025 tutakuwa tunaendelea. Kwa hiyo wale waliokuwa wana sifa waliokuwa hawakuwahi kuandikishwa safari hii mpaka sasa hivi hawajaingia kwenye daftari kwa kweli taratibu zetu sasa hivi hatuna namna ya kuweza kuwaandikisha tena ndani ya daftari.

Hata Waingereza juzi sisi wenyewe mashahidi tuliwaona, watu wanalalamika wanasema jamani sisi tumekosa haki yetu ya kupiga kura. Uingereza ndio hao mataifa yaliyoendelea ambao na sisi sheria zetu taratibu zetu nyingi tunafuata

kutoka kwao pia walikosa nafasi hiyo. Sio hivyo tu Mwenyekiti. Unajua hili suala nivumilieni kwa sababu ni suala zito, hata katika vyama vyetu vya siasa kuna wanachama wetu sasa hivi kuna baadhi ya vyama vimeshapiga kura ya maoni. Watu wamelalamika kwenye vyombo vya habari wanazo kadi zao za vyama vyao lakini wamekosa nafasi ya kuwachagua wawakilishi wao.

Mfano mdogo hata Mhe. Jadi, juzi katoa mfano kwamba ndani ya Jimbo lake kuna watu wanachama wake lakini hawakupata haki ya kumchagua yeye. Sasa watakuja kumchagua mwakani. Mimi nadhani mambo haya yanajitokeza kwa pande zote mbili. Ahsante Mwenyekiti.

Nam. 42

Taaluma ya Kuhifadhi Mazingira

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Hivi sasa tayari wataalam wa mazingira wametowa tahadhari juu ya utumiaji mbaya wa mazingira pamoja na nishati na kubashiri kuwa visiwa vyote vidogo vidogo vilivyomo katika Dunia pamoja na vyetu Unguja na Pemba huenda vikazama baada ya kupita miaka hamsini (50) ijayo kama mazingira yataendelea kuharibiwa.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa Wizara yako inahusika imechukua hatua gani kuifanyia kazi tahadhari hiyo ya kimatai*fa?*

(b) Kwakuwa ukataji wa miti na uchimbaji mchanga kiholela unaendelea, Wizara inatowa wito gani kwa wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo lakini kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafutayo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba tahadhari imeshatolewa na wataalamu wa mazingira duniani kwamba kuna baadhi ya visiwa huenda baada ya miaka 50 ijayo vikazama. Hata hivyo, naomba nitofautiane na Mhe. Mwakilishi kwamba visiwa vya Zanzibar havimo katika kundi hilo. Visiwa ambavyo viko katika hatari zaidi ni *Maldives*.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wote imekuwa ikitoa elimu ya mazingira kwa jamii juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwa kupanda kwa kina cha bahari ni miongoni mwao. Kazi nyengine tunayoifanya ni kuendeleza kampeni za upandaji miti ya juu na mikandaa au mikoko na kutokuikata iliyopo pamoja na kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa katika kupanga na kutekeleza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Pamoja na hayo wizara yangu pia kupitia Idara ya Mazingira inaendelea na juhudi zake za kuendelea kuishajihisha jamii pamoja na vikundi kushiriki katika suala zima la uendelezaji la uhifadhi wa mazingira.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu inatoa wito kwa wananchi wote kufuata taratibu zilizopo katika uvunaji wa maliasili zetu ikiwa ni pamoja na uchimbaji mchanga, kifusi na uchukuaji wa mawe. Aidha, naomba kuitahadharisha jamii kutokata miti ovyo kwani kufanya hivyo tutakuwa tunajihatarishia maisha yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumezaliwa katika ukanda wa pwani. Historia inaonesha tulipokuwa wadogo hadi kufikia leo kama mita arobaini mpaka hamsini zimeshaliwa na bahari. Kwa sababu minazi na mivinje iliyokuwepo katika maeneo hayo imeshazama au imeshatoweka kabisa.

Je, kwa kuangalia hayo na tahadhari ambayo dunia inaambiwa kwamba visiwa vilivyokuwemo katika ulimwengu huu vipo hatarini. Taaluma ndio sehemu ya mwanzo kuhakikisha kwamba vinanusurika visiwa vyetu kutokana na mambo mbali mbali ya mazingira. Hivyo wizara ina mpango gani wa makusudi kuanzisha eneo la mfano wa kulinda mazingira katika sehemu za pwani kama kujenga kwa mawe au kujenga ukuta mkubwa wa aina yoyote ile ili kunusuru bahari yetu isile ardhi yetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii. Kama Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira alivyojibu swali mama kwamba tatizo hili kwa jumla ni

la Kitaifa na Mataifa na sio la mtu mmoja au taasisi fulani. Sote kwa pamoja kila mtu aweze kutoa mchango wake katika hifadhi ya mazingira.

Suala alililouliza la kuhusu kwamba Wizara imeshukua hatua gani kuhusu mmong'onyoko wa ardhi kutokana na kupanda kwa bahari katika maeneo ya visiwa vyetu. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba wizara inamaliza hatua ya kupitia visiwa vyote Unguja na Pemba katika maeneo yote ambayo yanaendelea kuathirika na hatimae kukusanya ripoti hiyo na kukaa kitaka kuipangia mikakati namna gani ya kuweza kuhifadhi maeneo hayo. ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Serikali Kuu pamoja na kushirikiana na wahisani mbali mbali katika dunia, namna gani tutaweza kuhifadhi maeneo hayo ya mmong'onyoko kwa mfano labda kujenga ma - *bridge* makubwa ya saruji na kadhalika.

Kwa ufupi kwamba Wizara inalijua hilo na hivi karibuni itapatikana ripoti kamili itamalizwa ili nayo tuifanyie kazi.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nakupongeza sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kisiwa Panza ambacho kipo katika jimbo langu ni kisiwa kimojawapo kilichovamiwa na maji ya bahari. Na kwa kuwa taarifa hii niliitoa katika wizara ya Mheshimiwa. Na kwa kuwa wizara ilileta wataalamu wakaja tukakaguwa na tukaona kuna mwahala kama tukifanya juhudi ndogo tunaweza tukaidhibiti ile chumvi isiingie katika maeneo ya kilimo.

Na kwa kuwa wakati wa ukoloni tatizo kama hili lilitokezea na wakoloni wakalidhibiti pamoja na kwamba wakoloni walikuwa wabaya hawatutakii mema lakini waliweza kulidhibiti.

(a) Je, Mheshimiwa haona kwamba Kisiwapanza kama serikali itakusudia kikweli kweli kudhibiti Chumzi isiingie katika maeneo ya Kilimo uwezekano huo upo?

(b) Haoni kwamba Wizara yake Mheshimiwa imekuwa na maneno mengi sana lakini utekelezaji mdogo?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba taarifa hii hata serikali kuu inajua tumeiarifu hali ilivyo katika visiwa vyetu kuhusu mmong'onyoko wa maeneo mbali mbali na hatua tumeshaanza kuchukua. Serikali pia ipo pamoja nasi kwamba mara tu

tukimaliza utafiti huu au zoezi hili basi itashirikiana nasi katika kuweza kutusaidia idadi ya fedha fulani kuweza kukabiliana na hali hii kama tulivyosema.

Mara tu baada ya ripoti hii kumalizika utekelezaji nitaufanya kwa kipaumbele mle mlimoharibika zaidi au mle mnamohatarisha zaidi basi humo ndio tutaanza mwanzo, kama alivyosema Mheshimiwa sehemu hii ya Kisiwapanza. Kwa hivyo pengine tutaanza kwako.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa sababu hali ya mazingira dunia inatueleza kama kila mmoja ayalinde sehemu yake au nchi yake kuhusu mazingira jinsi yalivyo duniani. Juzi Mhe. Waziri Kiongozi akijibu swali kama hili alisema maeneo ya Wigwi, Tumbe na maeneo mengineyo na kama Kisiwapanza lakini alisahau na eneo moja la jimbo langu Ambasha mashamba tayari yameshavamiwa na chumvi, kwa hivyo wananchi hawapati kulima.

Mhe. Waziri Kiongozi kasema kumetumwa watu wakapige makuta ya udongo. Je, kwa sababu makuta ya udongo ikija mvua yamamong'onyoka. Serikali ina mpango gani wa makusudi kujenga makuta ya mawe ili kuzuia mmong'onyoko ule usiendele kuvamia maeneo mengine.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mara tukimaliza ripoti yetu basi tutatizama yale maeneo ambayo yanaathirika na yako katika hali mbaya kuweza kuyapa *priority* pengine ikiwa pamoja na eneo alilolitaja Mhe. Mwakilishi kisiwani kwake Kojani. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba wasubiri na wataona hatua zitaanza kuchukuliwa.

Nam. 54

Karakana za Kuchongea Vipuri

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

(a) Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani mahsusi wa kuvifanyia matengenezo vifaa vya ujenzi wa Barabara ambavyo vimeharibika na vipo kwa wingi kwenye Karakana za UUB Unguja na Pemba.

(b) Wizara yako ina mpango gani wa kufufua Mashine za kuchongea vipuri vya kutengenezea magari na vifaa vyengine ambazo sasa haziko katika hali nzuri katika Karakana za Wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utendaji wa Barabara tayari imevifanyia ukaguzi na tathmini vyombo vyake vyote Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Kampuni ya *"Mantrac Tanzania Ltd,"* kutokana na tathmini iliyofanywa, wizara yangu inajiandaa kupanga mpango wa matengenezo ya vyombo hivyo kutokana na vitendea kazi hivyo. Aidha, fedha kwa ajili ya matengenezo ya zana zitaombwa kutoka Mfuko wa Barabara katika bajeti ya 2010 – 2011 ambapo mazungumzo ya awali yamefanyika na kuonesha dalili za mafanikio ya upatikanaji fedha hizo; na

(b) Wizara yangu inaendelea kutafuta fedha za kuzifufua baadhi ya *machine* kwenye Karakana zetu za kutengenezea zana nzito ikiwemo magari na vifaa vya ujenzi wa barabara.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa *machine* hizi zimekaa kwa muda mrefu na inawezekana kwamba vikitengenezwa gharama yake ni kubwa zaidi kuliko kununua vipya. Lakini mara nyingi mali za serikali zinapotaka kuuzwa au kutengenezwa hupitia Idara ya Uhakiki Mali.

Je, Mhe. Naibu Waziri tayari ameshaiambia Idara ya Uhakiki Mali ihakiki na kumpa mawazo kwamba vinaweza kutengenezeka au havitengenezeki.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Idara ya Uhakiki Mali ndio inayoshughulikia masuala ya vyombo vya serikali aidha viwe vizima au vibovu katika kuvifanyia uhakiki na suala hilo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tutaangalia vile ambavyo vitakuwa havitengenezeki basi tutatafuta uamuzi wa kuviuza na vile ambavyo vitatengenezeka basi tutavitengeneza kwa ajili ya kuendeleza idara yetu hii.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba katika Baraza lako hili tukufu tuliambiwa kwamba kuna vifaa vipya vitakavyoagizwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Kusini Pemba ili vifaa hivyo baadae utakapomalizika mradi iwe ni mali ya serikali.

a) Je, ni vifaa gani vilivyoletwa mpaka sasa katika ujenzi wa barabara hizo ambavyo baadae vitakuwa ni mali ya serikali?

b) Kwa kuwa katika ujenzi wa barabara hizo vinatengenezwa vyombo vikongwe ambavyo vinatumika wiki moja wiki ya pili vinakuwa vibovu. Je, Mhe. Naibu Waziri atatwambiaje haoni kama kufanya hivyo ni kupoteza fedha bure?

c) Pia haoni kwamba kufanya hivyo ni kuzichelewesha zile barabara zisimalizike kutokana na vifaa?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara yangu imesema kwamba itanunua vifaa vipya kwa ajili ya kuongezea vile vilivyopo kwa ajili ya matengenezo ya barabara na hasa zile barabara za Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tayari baadhi ya vifaa hivyo vipo pale Mwambe. Kuhusu ni vifaa gani nitampatia jibu baada ya kuwasiliana na wenzetu kwa sababu sijavinakili sawa sawa ni vifaa vipi ambavyo vimeletwa lakini nina hakika kwani hata juzi tulipofanya ziara na Mhe. Waziri Kiongozi wamethibitisha hilo kwamba tayari baadhi ya vifaa vipo pale.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu matengenezo na kununua vifaa vipya kwamba nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni vyema tukawa na vifaa vipya kwa sababu tunapokuwa na vifaa vipya tunaweza kufanya kazi vizuri zaidi kwa sababu hata sisi tunakwenda na suala la kwamba tunakwenda kwenye kazi lakini mara leo kijiko kimeharibika huwa inatuongezea muda na hatwendi na wakati kama vile ambavyo tumeamua kufanya. Kwa hivyo, ushauri wake tunaupokea na pale ambapo uwezo utapatikana basi tuko tayari kufanya kila kinachowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba Mfuko wa Barabara umetuahidi kwamba utatusaidia kupata vyombo vipya ili kuona kazi zetu zinakwenda vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kupitia pesa za msamaha wa madeni tumeweza kununua vifaa vingi sana kwa Idara ya UUB yale magari unayoyaona mapya ya blue, makatapila, ma-*bulldozer* tumeyapeleka Pemba na Unguja ndio maana kasi ya Kitengo cha UUB sasa imekuwa nzuri zaidi, sikumbuki ni pesa ngapi hizo nitaweza kumpatia lakini kwa kweli hata hivyo vifaa vidogo vidogo alivyosema kwa zile zana zilizokufa basi tumetumia pesa zile tukaanza kununua ndio maana sasa hivi kitengo kile kimeimarika. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba baadhi ya vifaa vipya ambavyo vimenunuliwa viko Mwambe na kwa kuwa mimi ni mzaliwa hasa wa Mwambe na pia ni mkaazi wa huko na kwa barabara hiyo ya Mtambile-Mwambe ndio inaendelea kujengwa. Mhe. Mwenyekiti, tatizo moja linalokwamisha barabara ile ni vifaa na kwa kuwa nimeshuhudia *bulldozer* likitembea Mtambile-Mwambe, Mtambile-Kangani na sehemu nyengine.

a) Je, anaweza akaniambia kweli vifaa hivyo viko Mwambe na ameviona au ameambiwa tu?

b) Mhe. Mwenyekiti, tatizo la barabara ile ni greda na *bulldozer* na bahati mbaya sijaliona *bulldozer* jipya limeingia siku gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka arekebisha yale maelezo yake ya mwisho kwamba sijaeleza kwamba tumenunua *bulldozer* jipya lakini nimesema kwamba baadhi ya vifaa viko pale, ni vifaa gani, vile vile nikamwambia kwamba tutavieleza baada ya kupata maelekezo mazuri na wale wenzetu walioko kule.

Pia Mhe. Mwakilishi kama anavyosema ni mwakilishi wa jimbo lile atakubaliana na mimi kwamba katika barabara ile hivi sasa tumefanya kazi kubwa na miongoni mwa vifaa vilivyopale ni kuwa lami tunayo ya kutosha mpaka barabara ile inamalizika na maeneo mengine, kama ametembelea ameona hiyo hali halisi iliyoje. Vile vile ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi kila baada ya muda akatembelea pale na akapata maelezo kutoka kwa wale wenzetu kwa sababu wewe ni miongoni mwa wadau katika barabara hiyo.

Nam. 60

Sifa za Kujiunga na Chuo cha Afya Mbweni

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-
Taasisi ya Sayansi ya Afya Mbweni ni Chuo pekee kinachotoa taaluma ya mambo ya Afya hapa Zanzibar kinachotegemewa kuwapatia nafasi za masomo watoto wa kizanzibari ili waisaidie Zanzibar kuondoa tatizo la upungufu wa wataalamu wa mambo ya Afya. Lakini yapo malalamiko mengi juu ya kunyimwa nafasi kwa vijana wengi waanaomaliza mafunzo ya Sekondari kwa visingizio vya kukosa sifa.

(a) Mhe. Waziri, Bodi ya Chuo imeweka vigezo gani vinavyotakiwa ili mtu aweze kujiunga na Chuo hicho?

(b) Zipo taarifa kuwa Chuo hicho kimejaa ubaguzi na upendeleo ambao unafanya vijana wenye sifa za kujiunga na Chuo hicho kuachwa na kupewa nafasi vijana wasio na sifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Afya Mbweni ni taasisi rasmi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria namba 10/1988 na kupewa jukumu la kufundisha wataalamu wa kada za katikati za taaluma za afya.

Chuo cha Afya kinasomesha wanafunzi wenye kada mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Uuguzi, Ukunga na magonjwa ya akili (*SNMW*/SNPY) miaka mitatu;
- Wasaidizi madaktari (*Clinical Officers*) miaka mitatu;
- Maofisa Afya Mazingira (*Enviromental Health Officers*) miaka mitatu;
- Mafundi sanifu Maabara (*Medical Laboratory Technicians*) miaka mitatu;
- Madaktari wasaidizi wa meno (*Dental Therapy*) miaka miwili; na
- Wakunga wa Afya ya jamii vijijini (*PHNB Health Nurse B*) miaka miwili.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukueleza ya kuwa Bodi ya Chuo cha Afya imeweka vigezo vifuatavyo ili mtu aweze kujiunga na chuo hicho:-

Mhe. Mwenyekiti, masomo ya afya ni masomo ya sayansi na kwa hivyo wanaostahiki kupata masomo hayo lazima wawe na sifa za masomo ya sayansi kama ifuatavyo:-

a) Wawe wamemaliza masomo ya kidato cha 4 au cha 6 na awe amefaulu kwenye mitihani ya taifa kwenye masomo ya sayansi;
b) Awe amefaulu angalau alama D kwenye masomo manne (4) ya *Biology*, *Chemistry*, *Physics*, *Math na Giography* katika kidato cha 4;
c) Awe amepasi somo la Kiingereza ambalo ndilo somo la kusomeshea;
d) Awe na umri kati ya miaka 19 -25 kwa wanafunzi wapya wanaomaliza skuli na kwa wafanyakazi wawe na miaka 25 - 39;
e) Awe amefaulu masomo ya darasa la 12 au 14 ya sayansi kama yalivyoelezwa hapo juu; na
f) Baada ya kupata sifa za hapo juu anatakiwa kijana afaulu mtihani unaotungwa na Chuo cha Afya wa maandishi yaani *thoery* na mahojiano *"Oral examination"* na kupasi kwa kupata alama asilimia 50% na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana kijana akapasi vizuri kwenye mitihani yake ya taifa bali akawa hakufanya vizuri kwenye mitihani ya majaribio ya Chuo cha Afya tukizingatia kuzuka wimbi la vijana kudanganya kwenye vyeti vyao vya kumaliza skuli na kushindwa kuendelea na masomo ya afya yanayowakabili. Kuhusu taarifa za kuwepo ubaguzi na upendeleo unaofanywa vijana wenye sifa za kujiunga na chuo kuachwa na kupewa nafasi vijana wasio na sifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kueleza kuwa si sahihi kuwa Chuo cha Afya kinafanya upendeleo, isipokuwa kinachotokea hata kama amesoma masomo yasio ya sayansi midamu amemaliza kidato cha 6 au hana mjumuiko wa sayansi ya afya na anapoambiwa hana sifa hapo huelezwa chuoni upo ubaguzi. Kwa hoja kuwa amemaliza darasa la 14 la masomo ya (*Art*) sanaa na siyo sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wenye sifa na wanaokamilisha masharti ndio wanaostahiki kuchaguliwa kujiunga na masomo ya Chuo cha Afya Mbweni na wala hakuna upendeleo wa aina yeyote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyengine kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, sina hakika kwamba Mhe. Naibu Waziri majibu yake yalikuwa na utafiti mzuri, lakini naomba nimuulize suala langu kwamba je, wataalamu wetu ambao wanamaliza wanao uwezo wa kupambana katika soko la ajira la Afrika Mashariki ambalo keshokutwa litakuwa na nchi tano; na

b) Sifa kubwa ambayo ameitaja ni kumaliza darasa la 12 na 14 tena kwa masomo ya sayansi, lakini tunazo taarifa na tunawajua watu ambao wamemaliza darasa la 12 wana alama za *Physics, Biology, Histry, Chemistry* na *Math* na wameachwa wamechukuliwa wanafunzi wa darasa la 10. Je, kama hao wapo huo si ubaguzi ni kitu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nataka kumwambia kwamba wataalamu wetu watakaomaliza pale katika mafunzo wanayopata pale chuoni watakuwa na uwezo wa kuingia katika ushindani wa ajira Afrika Mashariki hakuna wasi wasi kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachokifahamu na ninachokielewa na wahusika walivyonieleza ni haya majibu niliyojibu na nina hakika hivi hawawezi wakenda kinyume na haya yaliyoelezwa kwani mwenye sifa pale lazima awe amepata mafunzo hayo niliyoyataja hapo mwanzo. Mhe. Mwenyekiti, sasa kama wanahisi kuna jambo hili kuonekana kama kuna wengine wamechukuliwa bila ya kuwa na sifa. Mhe. Mwenyekiti, hilo mimi silifahamu na kama jambo hilo lipo basi namuomba mheshimiwa tuwe karibu zaidi ili anielezee na mimi nitalifanyia uchunguzi zaidi wa kina.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, katika kamati yangu nina mjumbe ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi katika chuo hiki na wao ndio wanaohusika katika kuchagua au kupitisha wale ambao wanachaguliwa kujiunga na chuo. Yeye ametupa taarifa ndani ya kamati kwamba yeye ni Mjumbe wa Chuo na walimkataa mwanafunzi ambaye hakuwa na sifa lakini wakati tunatembelea chuo hicho mwanafunzi tulimkuta darasani.

a) Je, kuna chombo kingine ambacho kina mamlaka zaidi au Mkuu wa Chuo anakuwa na mamlaka kuliko bodi?

b) Mhe. Mwenyekiti, wakati tunatembelea chuo hicho tuliwakuta wanafunzi nafikiri wa mwaka wa kwanza wale wakiwa katika hali mbaya ya kidarasa, wamekaa chini, hawana vikalio lakini mpaka pale mlangoni wamejaa. Je, haya ndio mazingira mazuri tukizingatia kwamba chuo hiki hivi karibuni kimeongezewa majengo na kutanuliwa ili wanafunzi hawa wapate elimu nzuri?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nimesema ya kwamba linawezekana hilo jambo lipo lakini mimi hiyo taarifa sina, na taarifa hii ndio tunaposema Waheshimiwa Wajumbe kama kuna jambo linaonekana katika taasisi zetu mahali popote haliendi vizuri basi tusingojeane moja kwa moja hapa tunaweza kulitengeneza suala hilo kabla halijaharibika zaidi kuliko hatua iliyofikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba kama haya mambo yapo basi tuwasiliane zaidi na wahusika wanaolijua hili jambo na hasa akiwemo Mjumbe wa Bodi na mimi ningelipenda huyo Mjumbe wa Bodi tukawa naye pamoja atueleza hili suala. Mhe. Mwenyekiti, tuna masikitiko kwa kuwa Mjumbe wa Bodi wetu amelijua suala hili sisi kama viongozi hakuja kutueleza moja kwa moja, lakini inawezekana binadamu akifikisha kwenye kamati yote ni sawa. Tunaomba sisi tuwe tunapata hizi taarifa kwani ndio changamoto zetu za kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mazingira mazuri inawezekana kipindi hicho kilikuwa kile ambacho madarasa yalikuwa hayajaongezwa, lakini sasa hivi nataka kusema kwamba Chuo cha Afya kinamazingira mazuri, madarasa yameongezwa, mabweni ya kulalia wanafunzi yameongezwa na hali sasa hivi inaendelea kuwa nzuri. Pia tumeshapata mfadhili mwengine ambaye anategemea kutujengea wakati wowote ni mfadhili wa Ubalozi wa Oman. Kwa hivyo, tunategemea kwamba hali ya chuo chetu itazidi kuwa na mazingira mazuri.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hii hoja ni kubwa na imetoka kwa wajumbe ambao wana uhakika kwa sababu ni wajumbe wamehusiana na hili. Mhe. Mwenyekiti, na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na hatuna habari ya aina hii.

Je, Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukamuomba Mhe. Naibu Waziri akairuhusu kamati yako ikafanye uchunguzi lakini kiti chako kiwawezeshe, uwezekano huo upo ili kuondosha hilo tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo suala linatakiwa aulizwe Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, najua kamati zinautaratibu wake kwa hivyo mimi ningeliomba kamati tukae nayo sisi kwanza uongozi wa wizara watwambie zile habari zilivyo na tuone sisi tunazifanyia kazi namna gani, na kama hapo itakuwa kama kuna suala wataliona bado halijakaa sawa hapo ndio kuna utaratibu labda mwenyekiti utaruhusu uwawezeshe wende wakafuatilie hilo jambo. Mimi naona kama kuwezeshwa wawezeshwe kwanza tukae nao na tulijadili kwa kina hili suala ili tuweze kulifanyia kazi vizuri zaidi.

Nam. 92

Meneja Mkuu wa *ZECO* Kushiriki Kwenye Vikao vya Bodi

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu – Aliuliza:-

Meneja Mkuu wa sasa wa Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) amepewa likizo ya lazima ili Serikali kutathmini utendaji wake, lakini bado anahudhuria Mikutano ya Bodi ya Wakurugezi *TANESCO* ambayo anashiriki akiwa kama Mkurugenzi Mkuu wa *ZECO*.

Kitendo hiki inaashiria kuwa Meneja huyo anapata au kulipwa posho asilolifanyia kazi.

(a) Ni sheria au utaratibu gani wa *TANESCO* unaomwezesha Mkurugenzi huyo kusimamishwa kuhudhuria Mikutano ya Bodi ya *TANESCO*;

(b) Kwa kuwa Meneja huyo bado anashiriki vikao hivyo, na kwa kuwa pamoja na kushiriki kwake, kwa nini huwa hawasilishi taarifa na maamuzi ya vikao vya Bodi kunakohusika;

(c) Mhe. Waziri, kwa kuwa Bodi ya *TANESCO* wanalijua suala la muhusika kwa taarifa rasmi na bado wanaendelea kuwa naye katika vikao vyao, huoni kuwa kuna mchezo mchafu kati ya Shirika la *TANESCO* mtu anayelalmikiwa; na

(d) Ni lini Serikali italipatia ufumbuzi suala la Meneja huyu hasa kwa kuwa taarifa yake ya likizo haijataja muda wa kumalizika kwa likizo hiyo, na kwamba ushiriki wake katika Bodi una mashaka na unakuwa kikwazo kwa Kaimu Meneja aliyepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Aliuliza:-

Mhe Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 92 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo lakini kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafutayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningependa kueleza utaratibu wa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya *TANESCO*. Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO* wanateuliwa kwa amri ya Waziri wa Nishati wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*Ministerial Order*) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (*Public Corporation Act, 1992*). Utaratibu uliopo kwa miaka mingi, mjumbe mmoja anateuliwa kutoka Zanzibar kutokana na shughuli zinazofanywa na Mashirika ya *TANESCO* na *ZECO*.

Wakati Bodi mpya inapotaka kuteuliwa, Mhe. Waziri wa Nishati wa Serikali ya Muungano anamuandikia Waziri anayehusika na Nishati upande wa Zanzibar kupeleka jina la mjumbe anayependekeza Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme, baada ya mapendekezo hayo Mhe. Waziri wa Nishati humteua rasmi pamoja na wajumbe wengine. Kwa maeneo mengine Mjumbe wa Zanzibar katika Bodi ya *TANESCO* haingiii kwa nafasi yake (*ex-official*) bali kwa uteuzi baada ya Waziri wa Nishati wa Serikali ya Muungano kushauriwa na Waziri wenzake wa Zanzibar.

Kwa mujibu wa utaratibu huo wizara inayohusika na nishati Zanzibar inapotaka kufanya mabadiliko ya Mjumbe wake inawajibika kumuandikia Mhe. Waziri wa Nishati wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Meneja Mkuu wa *ZECO* anahudhuria vikao vya Bodi ya *TANESCO* akiwa Mjumbe halali aliyeteuliwa na Waziri wa Nishati kwa hivyo anaendelea kuwa Mjumbe hadi uteuzi wake kama Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO* utakapofutwa au atakapomaliza muda wa uteuzi wake. Hata hivyo wizara yangu itaendelea kumkumbusha Mhe. Waziri wa Nishati wa Serikali ya Muungano wa Tanzania kufanya mabadiliko kulingana na mabadiliko ya uongozi katika *ZECO*;

(b) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Mjumbe huyo bado ana wajibu wa kuwasilisha taarifa na maamuzi yanyaofanywa katika Bodi ya *TANESCO* kwa vile maamuzi hayo wakati mwengine yanaathiri utendaji wa *ZECO*. Wizara itamkumbusha mjumbe wake huyo juu ya wajibu wake na lengo la kuteuliwa kwake kuwa mjumbe katika Bodi hiyo; na

(c) Mhe. Mwenyekiti, mjumbe huyu anasita kuhudhuria katika vikao hivyo vya Bodi ya *TANESCO* mara tu Mhe. Waziri wa Nishati wa Bara atakapomteua rasmi Mjumbe mwengine kuchukua nafasi ya Meneja aliyeko likizo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: (anaendelea) Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini kabla sijauliza swali hili, na mimi niungane na wanaokuambia kiti hicho kimefaa mimi nakuombea uwe spika.

Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwamba Kaimu Meneja Mkuu wa *ZECO* tangu kukaimu ni zaidi ya mwaka sasa. Hivyo ile sheria ya kukaimu si zaidi ya miezi sita imeondoka? Kama haikuondoka kwa nini hadi leo anakaimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Mwakilishi, Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako hili tukufu ambaye pia ameifanyia kazi sana wizara hii. Bado sheria ile ingalipo, lakini wakati utafika meneja yule ambaye kwa sasa anakaimu nafasi ile kwa muda wa zaidi ya hiyo miezi sita, basi atakuwa meneja kamili na tuendelee kumuombea dua. Najua wajumbe wangu wengi hapa mnapigia kelele na kwa kweli anastahiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Muda wa maswali umekwisha. Watendaji wananambia muda umeongezwa nusu saa, kwa hivyo mpaka saa nne na nusu basi tuendelee.

Watendaji wananiyumbisha hebu tusikie utaratibu kutoka kwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Mwenyekiti, nadhani kiutaratibu tumekubaliana kwamba maswali yachukue muda wa saa moja tu kwenye kipindi hiki. Kwa hivyo, madhali tumeanza saa tatu, basi saa nne tunamaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Waziri. Sasa kama nilivyosema muda wa maswali na majibu umekwisha tunaendelea na hoja.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, nimefarijika sana kwa kupata bahati nyengine hii leo kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mbele ya Baraza lako tukufu. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na uwezo huu.

Ninamuomba Mola wetu atuzidishie baraka na neema katika nchi yetu na aendelee kutujaalia amani na utulivu. Nasi viongozi pamoja na Wawakilishi wa wananchi, Mwenyezi Mungu atupe upeo na ujasiri wa kuamua na kutekeleza maamuzi yote tunayokubaliana. Mwenyezi Mungu awazidishie wananchi wetu imani ya kuipenda nchi yetu na kuwaamini viongozi wetu wakuu kwa wanayoyatenda kwa nia njema ya kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimwa Spika, nawasilisha hotuba hii sio tu wakati ambapo Baraza letu linamaliza muhula wake, bali pia Serikali ya Awamu ya Sita inamaliza kipindi chake cha pili na cha mwisho cha uongozi wake. Naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani A. Karume kwa uongozi wake thabiti na kuiweka nchi yetu katika mustakbali mpya wa maelewano ya kisiasa na kijamii.

Kadhalika, napenda kulipongeza Baraza la Mapinduzi kwa kuwajibika kikamilifu kwa wananchi katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, CCM na maazimio tuliyoyaahidi wakati Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri hasa kwamba tumechukulia maanani kiti hiki umekikalia hivi karibuni tu. Hakika, busara,

hekima uliyonayo na unayoendelea kutuonesha, inakuwa mfano wa kuigwa na kulijengea heshima kubwa. Baraza letu tukufu na hasa kwa upande wa akina mama. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie afya njema na uzima ili upate ari mpya katika utendaji wa kazi zako za kila siku.

Napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Baraza lako tukufu, ambazo zimekuwa zikitusaidia katika kutupa miongozo na ushauri katika utendaji wetu mzuri wa kazi. Shukrani zangu maaalum na mahsusi kabisa ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mhe. Haji Omar Kheri, Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu na Kamati ya Hesabu za Serikali iliyo chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe.

Wakati huo huo, naomba nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako hili kwa mashirikiano yao mazuri waliokuwa wakitupa wizara hii na mimi binafsi katika kipindi chote cha mwaka 2009/2010.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi yetu tumetangaza nia ya kwenda kuomba ridhaa ya wananchi watuchague tena majimboni mwetu. Naomba nieleze machache katika kurasa ya hotuba hii kuhusu maudhui ya uongozi adilifu. Wanafalsafa wa Kichina wamesema kuwa naomba kunukuu; “Utajiri wa Cheo ni mambo ambayo mwanadamu anatamani, na kila mmoja wetu angependa awenavyo, lakini binadamu asipokuwa mwadilifu hastahili kumilikishwa hayo”.

Ninawasihi viongozi wenzangu kuzidisha uadilifu katika kazi zetu ili wananchi wasije kutuhukumu kwa hilo. Ninawatakia kila la kheri wale waliotangaza nia ya kurudi tena katika Baraza hili. Pia niwapongeze wale ambao chama chao kimeshawapitisha kwa ngazi moja ya kurudi hapa tena. Pia naomba niwatakia maisha mema ya kustaafu wale wote walioamua kupumzika.

Mhe. Mwenyekiti, nilitamka hapo awali kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inakaribia kuhitimisha kipindi chake cha uongozi. Tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi chote cha miaka kumi. Nimeeleza kiufasaha kabisa mafanikio yetu wakati niliposoma Bajeti ya Serikali 2010/2011 siku chache zilizopita. Naomba kusisitiza kuwa Serikali yetu imeendelea kufuata Sera sahihi za Uchumi Mkuu na Marekebisho ya Mifumo ya Utendaji chini ya Mpango wa Mageuzi Makuu. Kipaumbele cha Mageuzi Makuu haya ni kupiga vita umasikini. Kutokana na azma hiyo, serikali imewekeza vizuri katika ujenzi wa miundombinu na kuifanya kuwa ya kisasa. Miundombinu hiyo ikiwemo ujenzi wa barabara, uwanja wa ndege, umeme, bandari, vituo vya afya, umalizaji wa nyumba za maendeleo, skuli,

hospitali na huduma za maji. Pamoja na changamoto mbali mbali zinazotukabili, uchumi wetu umeendelea kukua kwa viwango vya kuridhisha na viashiria vya uchumi vinathibitisha hayo.

Mhe. Mwenyekiti, amani, utulivu na mshikamano ndio siri kuu ya mafanikio ya maendeleo yetu. Mazungumzo ya maridhiano kati ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani A. Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*), Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad yaliyofanyika Ikulu Zanzibar tarehe 5 Novemba, 2009 ni ishara tosha ya jinsi Wazanzibari wanavyoweza wenyewe kutafuta ufumbuzi na suluhisho la kudumu katika changamoto zinazotukabili. Mazungumzo ya viongozi hawa wawili yametoa nuru mpya ya maelewano ya kisiasa katika historia ya Zanzibar. Naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza viongozi hao na tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie busara na hekima.

Mhe. Mwenyekiti, katika kudumisha na kuendeleza uhusiano wa Zanzibar na nchi marafiki, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameendelea kukutana na viongozi na wawakilishi wa mashirika mbali mbali ya kimataifa pamoja na kuhudhuria mikutano ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa viongozi aliokutana nao ni pamoja na Rais wa Kenya Mhe. Mwai Kibaki, Waziri Mkuu wa Msumbiji Mhe. Aires Bonifacio, Kiongozi wa Jumuiya ya Ismailia Mhe. Agha Khan.

Pia ameweza kuhudhuria Mikutano ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Uchumi wa Dunia (*World Economic Forum*) uliofanyika Dar-es-salaam na Doha, Mkutano Mkuu wa *UNESCO* uliofanyika Paris, na Mkutano wa Wawekezaji wa Afrika Mashariki uliofanyika Nairobi, Kenya. Aidha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amehudhuria sherehe za kutimiza miaka 47 ya uhuru wa Burundi na maonesho ya biashara Shanghai, China. Matukio haya yote yameiwezesha kuitangaza Zanzibar na kushiriki katika shughuli za kilimwengu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza utangulizi huu, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Dimani kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani A. Karume, kwa imani yake kubwa kwangu katika nafasi hii ya uwaziri. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi na kwa wananchi wote wa Jimbo la Dimani walionichagua. Naomba tena kuwasilisha salamu za wananchi wa jimbo la Dimani kwa kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza ahadi yake ya kumaliza ujenzi wa barabara ya Mazizini – Fumba kabla ya kumaliza kwa kipindi cha uongozi wake.

Kwa hakika tatizo hili lilikuwa kero kubwa na la muda mrefu kwa wananchi wa Jimbo la Dimani. Tunasema hatuna cha kumpa katika kuonesha furaha yetu ila; “AHSANTE SANA”. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, amuepushe na balaa, shari na amjalie maisha yenye furaha na amani ya kustaafu.

Mhe. Mwenyekiti, uweledi wa Mhe. Dk. Amani A. Karume katika kuiongoza nchi hii umeonekana si Zanzibar pekee yake, bali hata nje ya Zanzibar. Mabalozi na viongozi wengine mbali mbali waliofika Ikulu Zanzibar wameweza kumpatia sifa kemkem kwa mafanikio makubwa Zanzibar iliyopata kwenye maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii, hasa mafanikio katika vita dhidi ya malaria. Kwa kuthibitisha hilo, tarehe 14 Novemba, 2009 Chuo Kikuu cha Hurbert Kairuki kimemtunukia Shahada nyengine ya heshima ya Udaktari wa Falsafa kutokana na mchango wake katika kupambana na malaria hapa Zanzibar.

Muundo na Majukumu ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar na Malengo kwa Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo kuhusiana na muundo wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar na baadae kuelezea utekelezaji wa majukumu kwa kuangalia idara moja moja kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2010 na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inatekeleza majukumu na shughuli zake kwa kupitia idara na vitengo kumi vifuatavyo:-

a. Afisi ya Baraza la Mapinduzi
b. Tume ya Utumishi Serikalini
c. Idara ya utumishi Serikalini
d. Chuo cha Utawala wa Umma
e. Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa
f. Idara ya Mipango na Sera
g. Idara ya Huduma za Rais
h. Idara ya Mawasiliano
i. Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*)
j. Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba

AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mapinduzi likiwa msimamizi wa shughuli zote za serikali limeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuzipitia na kuzijadili Nyaraka za Sheria, Sera na miongozo kutoka wizara mbali mbali za serikali na hatimae kuidhinishwa kwa utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/2010, Afisi ya Baraza la Mapinduzi imeandaa vikao 12 vya Baraza la Mapinduzi vilivyojadili nyaraka 33. Nyaraka hizo pia zilihusisha sheria 13 na sera 2. Miswada ya sheria iliyojadiliwa katika Baraza la Mapinduzi baadae ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha Afisi ya Baraza la Mapinduzi iliandaa vikao 18 vya Kamati ya Makatibu Wakuu vilivyojadili nyaraka ambazo baadae ziliwasilishwa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa ushauri wa kitaalamu.

Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi imehakikisha kuwa kumbukumbu zote za Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu zimetunzwa vizuri na pia maagizo yote yaliyotolewa yametekelezwa kwa uhakika na ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Baraza la Mapinduzi imeendelea na juhudi za kuwaendeleza wafanyakazi wake ambapo mfanyakazi mmoja yupo katika hatua za mwisho za masomo yake ya Shahada ya Pili ya Utawala, huko Chuo Kikuu cha Dodoma na mfanyakazi mwengine anaendelea na masomo ya Stashahada ya Juu ya Uhasibu katika Chuo cha Uhasibu Arusha. Pia wafanyakazi wawili wamehudhuria mafunzo mafupi, kati ya hao mmoja amehudhuria mafunzo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na mwengine mafunzo ya Uandishi wa Sheria nchini India.

Katika kufanikisha dhamira ya utekelezaji wa Mkakati wa Marekebisho ya Utumishi wa Umma, wataalamu wamekamilisha utayarishaji wa mkakati huo ambao umeainisha maeneo makuu matano yaliyotiliwa mkazo kutekelezwa katika kipindi cha miaka miwili (2010/2011– 2011/2012). Maeneo hayo ni kubadilisha miundo na mifumo ya utoaji wa huduma kwa lengo la kuimarisha huduma, kuimarisha mazingira mazuri ya kiutendaji na maslahi kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundo ya utumishi, kuanzisha sera ya muda wa kati ya ulipaji mishahara, kuanzisha mfumo mzuri wa utunzaji kumbukumbu na taarifa za wafanyakazi ambao utafanikisha utekelezaji wa shughuli za serikali na mwisho kuimarisha Serikali za Mitaa na mpango mzuri wa uongozi na uwajibikaji.

Pia wataalamu wamekamilisha ripoti ya kupitia mfumo wa kumbukumbu za mishahara (*Payroll System*). Utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti hiyo

utaanza katika mwaka wa fedha unaokuja. Aidha, Sheria mpya ya Utumishi wa Umma na Sera ya Utumishi wa Umma zimeshatayarishwa na zinategemea kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi mapema katika mwaka ujao wa fedha ili utekelezaji uanze.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, serikali imeipatia Afisi ya Baraza la Mapinduzi kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa afisi zake hapo Mazizini. Ujenzi huo utahusisha Afisi za Idara ya Utumishi Serikalini, Afisi ya Tume ya Utumishi Serikalini na Afisi za Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi. Matayarisho ya ujenzi yataanza mapema mwaka ujao wa fedha. Kukamilika kwa ujenzi wa afisi hizo kutapelekea kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi na kuzidisha ufanisi katika utoaji huduma. Viambatanisho “K” na “L” vinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukuza uwezo na ujuzi wa wafanyakazi wa umma, serikali inaendelea na harakati za ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma – Tunguu ambapo mkandarasi ameanza kazi ya kukamilisha eneo la chini la jengo hilo. Chuo cha Utawala wa Umma kinatumika kuwajengea uwezo wafanyakazi wa serikali na hata wafanyakazi kutoka Sekta Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Baraza la Mapinduzi imekusudia kutekeleza malengo 6 yafuatayo:-

- Kuendelea kuandaa na kusimamia vikao vya Baraza la Mapinduzi na vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Kwa mwaka wa fedha ujao Afisi ya Baraza la Mapinduzi inatarajia kuandaa vikao 12 vya Baraza la Mapinduzi na vikao 48 vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Katika kutekeleza lengo hili Afisi ya Baraza la Mapinduzi itasimamia utekelezaji wa maagizo na maamuzi ya Serikali, Sera na Sheria na kuhakikisha yanatekelezwa kwa ufanisi;

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Marekebisho ya Utumishi wa Umma kwa kufanikisha utekelezaji pamoja na kutoa machapisho ya ripoti ya Mkakati wa Marekebisho ya Utumishi wa Umma na kusambaza kwa wahusika. Lengo hili pia litahusisha Mkakati wa kuwashirikisha washirika wa maendeleo ili waweze kutuunga mkono katika marekebisho haya;

- Kuandaa semina elekezi kwa wanasiasa na watendaji wakuu wa Serikali kuhusu Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma Zanzibar;

- Kutekeleza mpango wa mafunzo kwa kuwaendeleza wafanyakazi wanne kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali. Mfanyakazi mmoja anatarajiwa kuchukua mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Sheria, mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya Stashahada ya juu ya Uhasibu na wafanyakazi wawili watahudhuria mafunzo ya muda mfupi ya Uhazili;

- Kuendelea kusimamia miradi ya maendeleo kwa ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu; na

- Kuanza matayarisho ya ujenzi katika kiwanja kipya cha Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, ili Afisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa Shilingi 1,784,908,000/= ambapo kati ya hizo shilingi 534,908,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi 1,250,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti, usimamizi wa haki na maadili ya wafanyakazi wa serikali ndio msingi wa kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi Serikalini. Kwa kuzingatia msingi huo, Tume ya Utumishi Serikalini inatekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria, utaratibu na kanuni za utumishi serikalini ili kulinda haki na kudumisha maadili ya wafanyakazi. Majukumu ya kisheria ya Tume ya Utumishi Serikalini ni pamoja na kupandisha vyeo wafanyakazi, kusikiliza rufaa, kupandisha daraja na kuthibitisha kazini. Msisitizo mkubwa umewekwa kwa watumishi wa serikali juu ya kutoa huduma bora bila ya upendeleo na utii kwa serikali, kufanyakazi kwa uadilifu na kuheshimu sheria.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Tume ya Utumishi Serikalini imewapandisha vyeo wafanyakazi watatu, imesikiliza rufaa saba, kati ya hizo, rufaa nne zimekubaliwa na kutakiwa waajiri wao kuwalipa waajiriwa haki zao walizozuiliwa wakati kesi zao zinasikilizwa. Rufaa tatu zimekataliwa ambapo tume imekubaliana na uamuzi uliotolewa na mamlaka zao za ajira wa kuwafukuza kazi watumishi baada ya kuthibitisha makosa yao. Aidha, Tume ya Utumishi Serikalini imewathibitisha kazini wafanyakazi 416 na imewarekebishia mishahara wafanyakazi watatu (Kiambatanisho “B” kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya uandaaji wa mafunzo na mitihani ya kitaalamu kwa wafanyakazi wa serikali inaendelea vizuri kwa mashirikiano kati ya Tume ya

Utumishi Serikalini na Chuo cha Utawala wa Umma. Mafunzo ya kitaalamu yanayotolewa ni fani za utunzaji kumbukumbu, utawala, masjala, uhazili na kompyuta. (Kiambatanisho "C" kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo la kuwaendeleza kitaalamu wafanyakazi wa Tume ya Utumishi Serikalini, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, wafanyakazi wawili wamepelekwa masomoni. Mfanyakazi mmoja amesoma mafunzo ya uhazili kiwango cha cheti katika Chuo cha Utawala wa Umma na mfanyakazi mwengine anaendelea na masomo yake ya utawala wa Biashahara (*Business Administration*) ngazi ya stashahada katika chuo cha Biashara Dodoma (*C.B.E.*).

Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tume ya Utumishi Serikalini imepanga kutekeleza malengo manne yafuatayo:-

- Kuelimisha Wafanyakazi Kanuni za Utumishi Serikalini (G.O) katika sehemu za kazi. Katika kuitekeleza kazi hii, Wajumbe wa Tume pamoja na Wataalamu wa Sheria za Kazi watatembelea Taasisi za Serikali kutoa elimu kuhusu kanuni hizo;

- Kuendelea kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar katika kupanga utaratibu wa kufanya mitihani ya kitaalamu kwa wafanyakazi wa Serikali. Mitihani hiyo inalengo la kukuza ujuzi wa Watumishi kulingana na fani zao. Fani zinazotegemewa kuwemo ni utunzaji kumbukumbu, rasilimali watu, utawala na kompyuta;

- Kuendelea kusimamia haki za wafanyakazi wa serikali ikiwa pamoja na kuthibitisha kazini, kusikiliza rufaa kwa wafanyakazi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na mamlaka zao za ajira, kupandishwa vyeo wafanyakazi na marekebisho ya mishahara; na

- Kuwaendeleza wafanyakazi wake kimasomo, Tume ya Utumishi Serikalini imepanga kuwapeleka masomoni wafanyakazi wake watano (5). Mmoja atasoma mafunzo ya shahada ya kwanza katika fani ya Utawala, mfanyakazi mwengine atasoma shahada ya pili katika fani ya sheria. Wafanyakazi watatu watapatiwa mafunzo mafupi katika fani za utawala na masjala.

Ili Tume ya Utumishi Serikalini iweze kutekeleza malengo yake, inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 166,034,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya mageuzi ya utumishi wa umma ni pamoja na kuipa nguvu Idara ya Utumishi Serikalini katika kutekeleza majukumu yake. Majukumu hayo ni kusimamia sera, sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji utumishi wa serikali. Serikali itahakikisha kuwa Idara ya Utumishi Serikalini inajengewa uwezo kitalaamu, vitendea kazi vinaimarishwa na kuweka mazingira mazuri katika kutekeleza kazi zake.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Utumishi Serikalini imeweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wanane ikiwa ni moja ya hatua ya kuwajengea uwezo na kuimarisha ufanisi. Wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya Shahada ya Pili katika fani ya Utawala, ambapo mfanyakazi mmoja yupo katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Morogoro na mfanyakazi mmoja pia anaendelea na masomo nchini Japan katika fani ya Sera za Umma. Mfanyakazi mwengine mmoja amepata mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika fani ya Mawasiliano ya Habari katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Dar es Salaam. Wafanyakazi wawili wamepata mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Utawala katika Chuo Kikuu cha Zanzibar - Tunguu. Mfanyakazi mmoja amepata mafunzo ya Stashahada ya Uhasibu katika Chuo cha Biashara *CBE* – Dodoma. Mfanyakazi mmoja amepata mafunzo ya Stashahada ya Uchumi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Dar es Salaam. Mfanyakazi mmoja amepata mafunzo ya Stashahada ya Utawala katika Chuo cha Utawala wa Umma.

(Kiambatanisho “J” kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi Serikalini pia ina jukumu la kuratibu mafunzo mafupi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji serikalini. Mafunzo hayo ni pamoja na yale yanayofadhiliwa na kugharamiwa na nchi wahisani pamoja na washirika wa kimaendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 jumla ya watumishi 26 wamepatiwa mafunzo mafupi nchini India. Watumishi 3 wamefanikiwa kujiunga na mafunzo yaliyotolewa nchini Japan. Aidha, watumishi 2 wamefanikiwa kujiunga na mafunzo ya muda mfupi katika fani ya utawala nchini Korea ya Kusini. Jumla ya wafanyakazi 37 walihudhuria mafunzo mbali mbali yaliyodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, (Kiambatanisho “D” kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya marekebisho ya mishahara na kutayarisha miundo mipya ya mishahara kama ilivyoahidiwa katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka ulopita. Hatua ya marekebisho ya awali ilianza mwezi wa Oktoba, 2009 na kukamilika mnamo mwezi wa Disemba, 2009. Marekebisho hayo yalifanyika kwa kupandisha kiwango cha chini cha mishahara kutoka shilingi 80,000/= hadi shilingi 90,000/=.

Hatua ya pili ya marekebisho ya mishahara ilifanyika mwezi wa Januari, 2010 ambapo kima hicho kilipanda kutoka shilingi 90,000/= hadi shilingi 100,000/=. Pia miundo mipya ya mishahara imeshatayarishwa ambayo imezingatia miundo ya utumishi ya kada mbali mbali zilizomo katika utumishi wa serikali na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza rasmi wakati wowote. Hata hivyo, kwa watumishi waliomo katika kada ya ualimu tayari wameshafanyiwa marekebisho ya mishahara kwa kuzingatia miundo hiyo mipya kuanzia mwezi wa Aprili, 2010.

Hatua ya utayarishaji wa miundo ya utumishi "*Scheme of Service*" imekamilika ambapo jumla ya miundo 50 yenye kada 138 imeshatayarishwa. Kada 113 zimechanganywa katika miundo 25 na kada 25 zilizobaki zimo katika miundo inayojitegemea. Miundo ya utumishi imezingatia majukumu yanayotekelezwa na kila wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi Serikalini imeendelea kuwapangia kazi vijana waliorejea masomoni kutoka vyuo mbali mbali ambapo jumla ya wahitimu 757 wameajiriwa kwa mwaka huu. Kati ya hao vijana 500 wameajiriwa kwa kazi ya ualimu kwa upande wa Unguja na Pemba kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa walimu na vijana 257 wameajiriwa kujaza nafasi katika kada tofauti katika Mawizara na Maidara ya Serikali. Aidha, wafanyakazi 223 wamestaafu kazi kutokana na kufikia umri wa kustaafu kazi kwa lazima. Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Utumishi Serikalini inakusudia kutekeleza malengo tisa yafuatayo:-

- Kusimamia utekelezaji wa Miundo ya Utumishi kwa kufanya uchambuzi wa kazi, kupanga madaraja kwa kada zote na kupanga majukumu ya kazi kwa kila mfanyakazi wa serikali;

- Kuhakiki kumbukumbu za wafanyakazi wa serikali wanaoajiriwa na wale wanaostaafu. Katika kutekeleza lengo hili wafanyakazi 341

wanategemewa kustaafu kazi kwa mwaka ujao. (Kiambatanisho “E” kinatoa maelezo ya ziada);

- Kuendelea kuratibu utoaji wa mafunzo kwa watumishi wote wa Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo;

- Kuweka mazingira bora ya ufanyaji kazi ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi na kufanya matengenezo ya afisi;

- Kuendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake ambapo kwa mwaka huu tunatarajia kusomesha wafanyakazi 5 katika viwango vya Shahada ya Kwanza na Shahada ya Pili;

- Kutayarisha Kanuni za Uongozi wa Utumishi Serikalini;

- Kutayarisha Sera ya muda wa kati ya ulipaji mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali “*Medium Term Pay Policy*”;

- Kutoa ushauri na mafunzo yatakayosaidia kudhibiti bajeti ya mshahara. Mafunzo hayo yatajumuisha wafanyakazi wa Idara ya Utumishi Serikalini na Wizara ya Fedha na Uchumi; na

- Kuchapisha makala, majarida na vipeperushi vinavyohusiana na Mageuzi ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Utumishi Serikalini iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 171,668,000/=.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma kinaendeleza juhudi za serikali za kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbali mbali. Mafunzo hayo yanahusisha fani za Uhazili, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Utawala wa Umma, Ugavi na Ununuzi, uwekaji kumbukumbu pamoja na mafunzo ya Kompyuta. Chuo cha Utawala wa Umma kina wanafunzi 654 wanaopata mafunzo mbali mbali katika ngazi ya msingi, cheti na stashahada.

Kimsingi hivi sasa Mitaala ya Chuo cha Utawala wa Umma imetambuliwa na Baraza la Mitihani la Taifa (*NACTE*) na hatua zinaendelea za kupata usajili. Katika mwaka 2009/2010 Chuo cha Utawala wa Umma kimeanzisha mafunzo

maalum ambayo hutolewa kwa awamu. Chini ya mfumo huu, mshiriki hutunukiwa cheti baada ya kukamilisha sura alizopangiwa ***(Module)***. Chuo kimeshatowa vyeti kwa Makatibu wa Halmashauri 4 za Wilaya za Unguja kwa kufuata utaratibu huu. (Kiambatanisho "F" kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wakufunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma wafanyakazi 4 wamepatiwa mafunzo katika kipindi hichi. Wafanyakazi 2 wamepatiwa Stashahada ya Uzamili katika Vyuo Vikuu vya Dodoma na Dar es Salaam na mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya Diploma ya Juu ya Uongozi nchini India, wakati mfanyakazi mwengine anaendelea na mafunzo ya Ukutubi katika Chuo cha Ukutubi, Bagamoyo.
Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma kimefanya kazi nzuri ya kuimarisha uhusiano na vyuo vyengine. Katika kipindi hichi Chuo cha Utawala wa Umma kimekubaliana na Chuo cha *VETA* cha Chang'ombe kushirikiana katika maeneo ya kubadilishana wataalamu na uzoefu katika kuendesha mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Pia, kuandaa wanafunzi kushiriki katika mitihani inayoendeshwa na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi (*VETA*) katika kada za Uhazili na Uwekaji Kumbukumbu. Wakati huo huo, Taasisi ya *Tanzania Global Development Learning Centre* iliyoanzishwa maalumu kwa ajili ya kuendeleza Mageuzi ya Utumishi wa Umma, Tanzania imesaini mkataba wa makubaliano wa kuendesha mafunzo ya pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Chuo cha Utawala wa Umma kinakusudia kutekeleza mambo manne yafuatayo:-

- Kutoa nafasi zaidi kwa Watumishi wa Serikali kujiunga na mafunzo maalum ya awamu katika fani za Utawala, Utunzaji Kumbukumbu na Kompyuta kwa ajili ya kuwaongezea uwezo ili waweze kumudu vyema kazi zao;

- Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma ambapo wafanyakazi watatu wanategemewa kujiunga na mafunzo katika viwango vya Shahada ya Uzamili na Stashahada;

- Kuendeleza mashirikiano na Vyuo vya Utumishi wa Umma vilivyo ndani na nje ya Tanzania ili kuweza kupata ujuzi na uzoefu wa vyuo hivyo; na

- Kuboresha mitaala ili iende sambamba na masharti ya Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi (*NACTE).*

Mhe. Spika, ili Chuo cha Utawala wa Umma kiweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 145,390,000/= kwa kazi za kawaida.

AFISI YA URATIBU WA UCHUMI NA UHUSIANO WA KIMATAIFA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa, iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya uratibu na uwezeshaji wa ushiriki wa Zanzibar katika ushirikiano wa kikanda ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama. Jumuiya hizo ni pamoja na zile za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *SADC*, Jumuiya ya Afrika Mashariki *EAC*, Jumuiya ya Nchi za ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Rim*) pamoja na Uratibu wa Majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi *(EPA*) baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya nchi za Ulaya *(EU).*

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa malengo na madhumuni ya kuundwa kwa jumuiya hizo za kikanda yapo mambo makubwa ambayo yameshaamuliwa na kuanza kutekelezwa na nchi wanachama na yapo yale ambayo bado yanaendelea kujadiliwa katika ngazi mbalimbali za jumuiya hizo. Naomba kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza lako mambo muhimu yaliyojitokeza katika jumuiya hizo kama ifuatavyo:-

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*

Mhe. Spika, katika mkutano wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya hii *Summit* uliofanyika mwezi Septemba, 2009 huko Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)* wakuu hao walijadili na kufanya maamuzi yafuatayo:-

i) Kuichagua nchi hiyo kuwa Mwenyekiti mpya wa jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 ambapo Namibia imekuwa Makamu Mwenyekiti. Sambamba na uamuzi huo, wakuu hao waliiteua nchi ya Msumbiji kuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Ulinzi na Usalama ya *SADC* ambayo itasaidiwa na nchi ya Zambia kama Makamu Mwenyekiti wake;

ii) Kuteua viongozi wakuu wa Sekretarieti ya *SADC* ambapo Dr. Tomaz Augusto ambae ni raia wa Msumbiji aliteuliwa kuendelea kushika wadhifa wake wa kuwa Katibu Mtendaji Mkuu. Kiongozi huyo atasaidiwa na Manaibu Katibu

Watendaji Wakuu wawili. Naibu Katibu Mtendaji mmoja atashughulikia Fedha na Utawala na mwengine atashughulikia Uimarishaji wa ushirikiano *(Integration);*

iii) Kufanya uamuzi wa kuisimamisha uanachama wa *SADC* nchi ya Madagascar kutokana na kuondolewa madarakani isivyohalali, Rais wa nchi hiyo aliechaguliwa kidemokrasia, vile vile kutokana na ukaidi wa utawala mpya kutotekeleza Mkataba wa Maputo wa kuwa na Serikali ya pamoja; na

iv) Wakuu wa Jumuiya hiyo, walitilia mkazo haja ya kuleta maelewano ya haraka na kupata suluhisho la mgogoro wa kisiasa ulioibuka nchini Lesotho kufuatia matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika mapema mwaka 2007. Juhudi za usuluhishi wa mgogoro huo zinasimamiwa na Rais Mstaafu wa Botswana Mhe. Quette Ketumile Jon Masire. Matokeo ya uchaguzi mkuu huo yalizua mtafaruku mkubwa kutokana na kutoelewaka miongoni mwa wananchi na makundi mengine kwa utaratibu mpya wa uwakilishi uliotumika. Uwakilishi wa *Proportional Representations* ndio uliotumika na hivyo kulalamikiwa.

Kutokana na hali hiyo ya kisiasa ya nchi ya Lesotho, nchi za *SADC* zilijizuia kuunga mkono ombi la nchi hiyo la kutaka kuwania uenyekiti wa Umoja wa Afrika *(AU)* na badala yake kuunga mkono ombi la nchi ya Malawi.

Viongozi hao walipokea na kuzingatia taarifa ya hali ya chakula katika eneo la jumuiya na kubaini kuwa kwa ujumla bado hali ya chakula katika eneo la *SADC* siyo ya kuridhisha. Kutokana na hali hiyo, nchi wanachama walisisitizwa kuendelea kutekeleza Azimio la Dar es Salaam *(The Dar es Salaam Declaration 2002)* linalozitaka nchi hizo kuimarisha na kufanya mapinduzi katika kilimo.

Mhe. Spika, licha ya kuwepo maamuzi hayo makubwa, bado yapo mambo makuu ambayo yanajadiliwa katika ngazi mbali mbali za kitaalamu ndani ya jumuiya ya *SADC*. Mambo hayo ni kama yafuatayo:-

(i) Uni Visa;

(ii) Kuoanisha Mfumo wa Biashara baina ya Jumuiya za *COMESA, EAC na SADC; na*

(iii) Soko Huru la Biashara *(Free Trade Area).*

Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC*)

Mhe. Spika, kama ilivyokuwa kwa Jumuiya ya *SADC*,yalikuwepo pia maamuzi muhimu yaliyofikiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki pia kuwepo maeneo mengine ambayo bado yanaendelea kujadiliwa katika ngazi mbalimbali za jumuiya hiyo. Mambo hayo muhimu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuiteua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2009/2010;

(ii) Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iii) Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iv) Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi *(Economic Partnership Agreement); na*

(v) Umoja wa Kifedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki imejitokeza haja ya kuwepo kwa Umoja wa Kifedha ndani ya Jumuiya hiyo. Majadiliano kuhusu suala hili yameanza na kwamba Kamati ya wataalamu wa ngazi za juu kuhusu suala hili imeundwa ambapo pia wataalamu kutoka Zanzibar wanashiriki.

Shirikisho la Afrika Mashariki

Suala la uundwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki na hasa uharakishaji wake limeendelea kuwa tete ambapo baadhi ya nchi wanachama wakiunga mkono hatua za uharakishaji na wengine wakiwa na mtizamo tofauti. Katika mkutano wao wa Novemba, 2009, wakuu wa nchi za Jumuiya walielekeza kuundwa kwa Kamati ya Wataalamu (watatu kutoka kila nchi mwanachama) kuchambua na kubainisha maeneo ambayo yanakwaza uanzishaji wa shirikisho hilo. Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania timu hiyo inaundwa na wanasheria watatu ambao mmoja wao anatoka Zanzibar.

Miradi ya Zanzibar

Miradi ya Zanzibar ambayo iliwasilishwa *EAC* ili iweze kutekelezwa kikanda inaendelea kupatiwa mazingatio mazuri. Hivi sasa juhudi zinaendelea katika Sekretariat ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutafuta fedha kwa ajili ya

kuifanyia utafiti miradi hiyo ili iweze kuombewa fedha za utekelezaji wake. Afisi inaendelea kuliratibu na kulifuatilia kwa karibu suala hili kwa kushirikiana na Wizara husika ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa.

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Rim – Association for Regional Cooperation)*

Mhe. Spika, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi ilianzishwa kwa madhumuni ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara pia kuimarisha historia iliyojengeka baina ya nchi hizo kwa karne nyingi. Tokea kuanzishwa kwake mwaka 1977, Umoja huo umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri. Hata hivyo, hivi karibuni ilibainika kuwa bado ipo nafasi kubwa ya kuimarisha zaidi ushirikiano baina ya nchi wanachama iwapo kutafanyika marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya hiyo. Hivyo, pamoja na kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake, kazi kubwa inayofanyika hivi sasa ni kuandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Mkataba wa jumuiya hiyo ili yazingatiwe na nchi wanachama Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa inatarajia kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kawaida matano kama ifuatavyo:-

- Kuratibu na kufuatilia shughuli za ushirikiano wa Jumuiya mbali mbali za kikanda kwa lengo la kuifanya Zanzibar ishiriki kikamilifu na kufaidika na ushiriki huo;

- Kuendelea na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha uhusiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa;

- Kuendeleza juhudi za kukuza mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajili ya maandalizi ya Tanzania katika mikutano ya ushirikiano wa Kimataifa; na

- Kuimarisha utendaji kazi wa Afisi kwa kuongeza idadi ya watumishi wake, kuwaendeleza na kuimarisha vitendea kazi.

Mhe. Spika, ili iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa inaomba kuidhinishiwa Tzs. 651,000,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera ni kiungo muhimu baina ya Idara na Vitengo vyote vilivyo chini ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Idara hii ina jukumu la kusimamia shughuli zote zinazohusiana na utekelezaji wa mipango na Sera pamoja na kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji. Vile vile, Idara hii ina jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Ikulu fungu (10) zilizoidhinishwa kwa ajili ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Mipango na Sera imeendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake saba katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu na uhazili, watano wanachukua cheti Chuo cha Utalii Maruhubi katika fani ya uhudumu na upishi na mmoja anachukua Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro katika fani ya Maendeleo ya Mipango Vijijini.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera imeendelea kuwachukulia dhamana za mikopo wafanyakazi 106, ambapo kati ya hao wafanyakazi 76 wamekopeshwa na Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ*) na wafanyakazi 30 wamechukua mikopo katika Benki ya Posta ya Tanzania. (Kiambatanisho “G” kinatoa maelezo ya ziada).

Mhe. Spika, katika kuweka mazingira bora kazini, Idara ya Mipango na Sera imewapatia sare wafanyakazi wake 18, ambapo kati ya hao wafanyakazi kumi na moja ni Katibu Wahutasi na saba ni wahudumu katika Afisi ya Rais-Ikulu.

Mhe. Spika, katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Idara ya Mipango na Sera imehamasisha wafanyakazi wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI – Zanzibar. Jumla ya wafanyakazi 153 walishiriki katika zoezi hilo wakiwemo wanawake 75 na wanaume 78. Viambatanisho “K” na “L” vinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Mipango na Sera inakusudia kutekeleza mambo manne yafuatayo:-

- Kuendelea Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Sera na Mipango katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa mradi wa

mawasiliano na mradi wa matengenezo ya Ikulu na nyumba za Serikali *(State Lodges);*

- Kuendelea Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za fungu 10 Ikulu;

- Kuendelea Kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji yakiwemo masuala ya uajiri, maslahi na mafao mbali mbali; na

- Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake katika fani mbali mbali kwa viwango tofauti.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 436,263,000/= kwa kazi za kawaida na Tzs.1,500,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA HUDUMA ZA RAIS

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Idara ya Huduma za Rais inaratibu na kusimamia upatikanaji wa huduma bora za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Afisi ya faragha. Huduma hizo ni pamoja na makaazi, chakula, wageni wa Serikali, Usafiri, Utunzaji wa Ikulu na nyumba za Serikali. Idara hii ina Afisi zake Pemba, Dar – es – salaam na Dodoma.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Huduma za Rais imetekeleza majukumu yake katika hali ya kuridhisha, kama ivyoelekezwa. Kazi ambazo zimetekelezwa ni pamoja na kuratibu shughuli za Kitaifa na Kimataifa kupitia Afisi ya faragha, utunzaji wa jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja na nyumba za Serikali za Chake Chake, Wete, Mkokotoni, Laibon – Dar-es-salaam, Bwefum na Dodoma.

Mhe. Spika, idara hii vile vile imeweza kununua vifaa vya ndani katika Ikulu ya Mnazi Mmoja na nyumba za Serikali za Chake Chake Pemba na Laibon - Dar es salaam. Ikulu ya Mnazi Mmoja imepata masofa mapya na mazulia ambayo yameweza kukidhi sehemu za kumbi zote za Ikulu pamoja na Afisi ya Mheshimiwa Waziri, na Makatibu Wakuu. Aidha, nyumba ya Mkokotoni imefanyiwa matengenezo kwa kuezuliwa bati kongwe na kuezekwa bati mpya, kufanyiwa matengenezo dari na milango yote ya ndani kupakwa rangi na kuwekwa mipya.

Vile vile nyumba hii imefanyiwa ukarabati madirisha kwa kuwekwa waya za mbu, feni na taa mpya. Nyumba ya Laibon ya Dar es salaam imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa kupakwa rangi sehemu zote za nyumba hiyo, kusafishwa milango, madirisha, matengenezo ya sehemu ya vyoo, kuwekwa masofa mapya, mapazia na mazulia mapya. Mabadiliko makubwa yamefanywa katika Ikulu ya Chake Chake kwa kuipatia masofa mapya na mapazia pamoja na vipoza hewa vipya. Pia, Idara ya Huduma za Rais imepokea gari tatu mpya za aina ya *Toyota Land Cruiser* kwa ajili ya huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara hii inakusudia kutekeleza mambo manne yafuatayo:-

- Kuendeleza na kuimarisha Huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kufanikisha uendeshaji wa Afisi ya Faragha;

- Kushughulikia huduma muhimu za makaazi, chakula, usafiri na wageni wa Serikali wanaostahiki kupatiwa huduma za Ikulu;

- Kushughulikia utunzaji wa majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali za Unguja, Pemba, Dar-es-salaam na Dodoma kwa kufanya matengenezo pamoja na kusimamia masuala ya usafi maeneo yanayozunguka majengo hayo. Katika kipindi hichi nyumba ya Serikali ya Bwefum itafanyiwa matengenezo makubwa. Pia zitajengwa nyumba mpya Dar es Salaam na Dodoma chini ya mradi wa ujenzi wa nyumba za viongozi wa Kitaifa; na

- Kushughulikia safari za ndani na nje ya Zanzibar za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ili kufanikisha majukumu yaliyopangwa kutekelezwa, Idara ya Huduma za Rais kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 1,035,968,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakuwa karibu na wananchi na kwamba wananchi hao wanapatiwa taarifa sahihi juu ya mipango ya maendeleo inayotekelezwa, Serikali imeanzisha Idara ya Mawasiliano katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Idara hii inafanya kazi zake kwa mashirikiano ya karibu na Maofisa wa Mawasiliano wa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara hii imeweza kutayarisha vipindi vya televisheni vinavyoonesha maendeleo yaliyopatikana katika sekta za afya, utalii na miundo mbinu. Aidha Idara ilichapisha kalenda 3,500 za mwaka wa 2010 zinazoonesha maendeleo yaliyopatikana katika sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii pamoja na uzinduzi wa miradi mipya yenye lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2010/2011 inakusudia kutekeleza malengo matatu yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo kwa Maafisa Mawasiliano wa Wizara na Taasisi za SMZ, masheha na jumuia za kijamii juu ya kutoa habari kwa ufanisi na urahisi zaidi;

- Kuchapisha vijarida 6,000 vinavyoonesha mafanikio yaliyopatikana katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa pamoja na kuchapisha kalenda 3,500 za mwaka 2011; na

- Kumpatia mafunzo ya Shahada ya Pili ya Uandishi mfanyakazi mmoja. Aidha, Idara inakusudia kununua vitendea kazi vipya kwa ajili ya kupata ufanisi katika kazi zake.

Mhe. Spika**,** ili Idara ya Mawasiliano iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 39,704,000/= kwa kazi za kawaida.

KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI *(GSO)*

Mhe. Spika, kila mtumishi wa umma ana jukumu la kudhibiti na kuzingatia usalama wa shughuli za Serikali na Taasisi zake. Aidha, Serikali pia ina haki ya

kuwatambua watumishi wake kabla na baada ya kuwaajiri au kupewa dhamana nyengine. Idara ya Usalama wa Serikali ina jukumu la kisheria la kudhibiti usalama wa Serikali. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kutoa mafunzo ya usalama, kufanya upekuzi *(security vetting)* na utoaji wa kiapo cha utunzaji wa siri.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Kitengo cha Usalama wa Serikali kimefanya ukaguzi katika baadhi ya Afisi za Serikali Unguja na Pemba kuhusu udhibiti wa nyaraka za Serikali na kupendekeza njia bora zinazofaa. Ukaguzi huo ulijumuisha ukaguzi wa nyaraka katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni, Halmashauri za Wilaya ya Kaskazini, Magharibi, Chake Chake na Wete, Afisi za Baraza la Mji la Chake Chake na Wete. (Kiambatanisho "H" kinatoa maelezo zaidi)

Mhe. Spika, katika kipindi hichi, Idara ya Usalama wa Serikali imetoa mafunzo ya usalama kwa Maafisa wa Idara ya Uhamiaji wa Mikoa mitano ya Zanzibar. Aidha, wafanyakazi wa Serikali 464 walifanyiwa upekuzi. (Kiambatanisho "I" kinatoa maelezo zaidi) Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Kitengo cha Usalama wa Serikali *(GSO)* kinakusudia kutekeleza majukumu matano kama ifuatavyo:-

- Kuendelea kufanya ukaguzi wa Wizara na Taasisi za Serikali katika eneo la udhibiti na utunzaji wa nyaraka za Serikali na kutoa ushauri unaofaa;

- Kuendelea kufanya ukaguzi katika Taasisi mbali mbali za Serikali kuhusu ulinzi na usalama wa vituo muhimu, ikiwemo majengo ya Serikali, maeneo na miundo mbinu ya Serikali;

- Kuendelea kutoa mafunzo juu ya utunzaji wa siri za Serikali kwa Maafisa Waandamizi wa Serikali na watumishi wa ngazi mbali mbali wanaoshughulikia nyaraka za Serikali;

- Kuendelea kuwafanyia upekuzi watumishi wa Serikali na Taasisi zake; na

- Kuendeleza ushirikiano na Idara ya Utumishi Serikalini katika kusimamia kanuni za utumishi na kuhakikisha zinatekelezwa hususan zile zinazogusa usalama wa mali na nyaraka za Serikali.

Mhe. Spika, ili Kitengo cha Usalama wa Serikali *(GSO)* kiweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kinaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 29,859,000/= kwa kazi za kawaida.

AFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Spika, Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utawala, utumishi, huduma na shughuli za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinazofanyika Pemba. Shughuli hizo ni pamoja na utunzaji wa majengo ya Serikali Pemba na kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Kimataifa wanapotembelea Pemba kwa shughuli za Kiserikali. Aidha, Afisi hii inasimamia utekelezaji wa matoleo mbali mbali ya Serikali kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, kazi zilizofanywa na Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ni pamoja na kusimamia ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Katika kipindi hichi jumla ya ziara saba zimefanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya ziara moja na Mheshimiwa Makamo wa Rais amefanya jumla ya ziara tatu. Aidha, Afisi ya Afisa Mdhamini imefanya matengenezo ya nyumba za Serikali Wete na Chake Chake yaliyohusisha pia uwekaji wa vifaa vipya vya ndani kama vile vitanda, masofa, meza za kulia na vipoza hewa.

Mhe. Spika, Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba imeweza kuwapatia nafasi za mafunzo wafanyakazi wake watatu. Mfanyakazi mmoja anachukua fani ya uhudumu katika Chuo cha Utalii Maruhubi na wafanyakazi wawili wanachukua mafunzo ya Uwekaji Kumbukumbu katika Chuo cha Utawala wa Umma. Aidha, imewachukulia dhamana za mikopo wafanyakazi wake wanane kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ).* Vile vile, kupitia maelekezo ya Idara ya Utumishi Serikalini, imefanya uhamisho kwa wafanyakazi sita kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa kazi. Kiambatanisho "K" kinaonesha fedha zilizotengwa na zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba inakusudia kutekeleza malengo matano yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia na kuratibu shughuli zote za Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba zikiwemo kusimamia Ziara za Viongozi Wakuu, utunzaji wa nyumba za Serikali na utawala;

- Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wake;

- Kuifanyia ukarabati Ikulu ya Mkoani, pamoja na kuipatia vifaa vipya;

- Kuendelea Kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji yakiwemo maslahi ya wafanyakazi na kusimamia utekelezaji wa matoleo mbali mbali ya Serikali; na

- Kuanza matayarisho kwa ajili ya ujenzi wa Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 199,207,000/= kwa kazi za kawaida.

JUMLA YA GHARAMA ZA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa malengo ya Idara zote zilizo chini ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo ya muhtasari wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na maombi ya fedha kwa mwaka wa 2010/2011.

Mhe. Spika, katika kipindi kinachomalizikia Juni, 2010, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilikadiriwa kutumia jumla ya Tzs. 2,723,200,000/= kati ya hizo Tzs.1,693,200,000/= kwa kazi za kawaida na Tzs. 1,030,000,000/= kwa kazi za maendeleo (Fungu 10 – Afisi ya Rais – Ikulu) Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa Tzs. 608,000,000 kwa kazi za kawaida (Fungu 07 Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa) (Fungu 08 – Afisi ya Baraza la Mapinduzi) imeidhinishiwa jumla ya Tzs. 1,340,970,000/= kati ya hizo Tzs. 890,970,000/= kwa kazi ya kawaida na Tzs. 450,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs. 3,241,000,000/= miongoni mwa fedha

hizo Tzs 1,741,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tzs. 1,500,000,000/= kwa kazi za maendeleo (Fungu 10 Afisi ya Rais Ikulu). (Fungu 07 Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa) Tzs. 651,000,000/= kwa kazi za kawaida. (Fungu 08 Afisi ya Baraza la Mapinduzi) jumla ya Tzs. 2,268,000,000/= kati ya hizo Tzs. 1,018,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tzs. 1,250,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, uchambuzi wa fedha zilizoainishwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na zilizopatikana mpaka mwezi wa Mei 2010 pamoja na fedha zinazoombwa 2010/2011 zimeoneshwa katika Viambatanisho "K" na "L"

HITIMISHO

Mhe. Spika, mageuzi ya kisiasa na kiuchumi yamepanua sana mipaka ya haki na uhuru wa wananchi wa Zanzibar. Naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwa adilifu na wazi kwa wananchi wake na kuhakikisha kuwa mafanikio yaliopatikana yanakuwa endelevu. Hata hivyo, tuelewe kuwa hatuwezi kupata maisha mapya ya kisasa ikiwa baadhi yetu tutakuwa bado tunang'ang'ania tabia, khulka na mienendo ya kizamani. Ninawasihi viongozi na wananchi wenzangu kukubali mabadiliko yanayotokea. Wahenga wamesema "penye nia pana njia". Kutokana na nia safi waliyonayo Wazanzibari kuwa na umoja, amani na utulivu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametuonesha njia ya kuwa tunaweza kutafautiana bila ya kugombana na naamini sote tunakubaliana na hilo.

Mhe. Spika, ninawashukuru wananchi wote wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla kwa kudumisha amani, upendo, utulivu na mshikamano. Ninawashukuru pia wafanyakazi wa Serikali kwa juhudi zao walizozionesha katika utoaji wa huduma na kujenga nchi yetu. Aidha, napenda kuitumia fursa hii kuzishukuru Sekta Binafsi, Taasisi za kiraia pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa kushirikiana nasi na kutuunga mkono katika utekelezaji wa mipango mbali mbali ya kimaendeleo. Mashirikiano yao yametoa mchango mkubwa katika kukabiliana na changamoto nyingi za kimaendeleo zilizotukabili. Sote ni mashuhuda wa hayo. Nimalizie kwa kunukuu usemi maarufu wa msanii Bi Siti binti Saadi "Zanzibar ni njema atakae aje".

Mhe. Spika, mwisho, naomba nichukue fursa hii adhimu tena kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake na usimamizi mahiri uliopelekea mafanikio makubwa katika sekta za kiuchumi, kijamii na za kisiasa. Shukrani mahsusi ziwaendee Watendaji Wakuu na wafanyakazi wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao walionipa katika kipindi hichi cha uongozi. Mwisho kabisa ninawashukuru wafanyakazi wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Zanzibar kwa kufanikisha upatikanaji wa vitabu hivi kwa wakati.

Mhe. Spika, ninawashukuru wote kwa kunisikiliza na natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa michango yenu mtakayoitoa katika kuijadili hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KIAMBATANISHO "A"

WAGENI MBALI MBALI WALIOTOKA NJE YA TANZANIA NA KUONANA NA MHE. RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI – JUNI, 2009 – JUNI, 2010

NAM	TAREHE	JINA	ANUANI (NCHI WANAZOTOKA)
1.	30 Juni, 2009	Mhe. Sander Curbnz	Balozi wa Uturuki nchini Tanzania
2.	2 Julai, 2009	Mhe. Juan Manuel Gonzalie	Balozi wa Hispania nchini Tanzania
3.	3 Julai, 2009	Bw. Danny Glover	Balozi wa Heshima wa UNICEF
4.	8 Julai, 2009	Mhe. Joy Lomoy	Balozi wa Norway nchini Tanzania
5.	10 Julai, 2009	Mhe. Yudhistiranto Sungad	Balozi mpya wa Indonesia nchini Tanzania
6.	17 Julai, 2009	Mhe. Mwai Kibaki	Rais wa Kenya
7.	21 Julai, 2009	Mhe. Janet Sidah	Balozi wa Canada nchini Tanzania
8.	28 Julai, 2009	Bw. Tomie	Mshauri wa Kampuni ya Nishizawa ya Japan
9.	30 Julai, 2009	Bw. H.H. The Agha Khan	Kiongozi wa Jumuiya ya Ismailia
10.	18 Agosti, 2009	Bw. Peter Dozst	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini Netherlands
11.	18 Agosti, 2009	Bw. Stoxen Baira	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini Norway
12.	18 Agosti, 2009	Bw. Robert Qrr	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini Canada
13.	18 Agosti, 2009	Bw. Andrew Ershammar	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini Sweden
14.	18 Agosti, 2009	Bw. Tam Bennam	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini UK
15.	18 Agosti, 2009	Bw. David Scort	Balozi wa Nchi za Ulaya nchini USA
16.	19 Agosti, 2009	Bibi Magreth Chan	Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani
17.	11 Septemba,	Bi. Diaroton Gaye	Mkurugenzi wa Benki ya

	2009		Maendeleo ya Afrika
18.	15 Septemba, 2009	Mhe. Edzin A. Chimoyo	Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania
19.	24 Septemba, 2009	Mhe. Jon Homoy	Balozi wa Norway nchini Tanzania
20.	28 Septemba, 2009	Mhe. Sander Curbnz	Balozi wa Uturuki nchini Tanzania
21.	6 Oktoba, 2009	Dk. Adkoekkoek	Balozi mpya wa Uholanzi nchi Tanzania
22.	8 Oktoba, 2009	Bi. Eva Lindastorom	Mkaguzi Mkuu wa Hesabu nchini Sweden
23.	10 Oktoba, 2009	Mhe. Sindiso G. J.	Balozi wa Afrika kusini nchini Tanzania
24.	11 Oktoba, 2009	Mhe. Jon Homoy	Balozi wa Norway nchini Tanzania
25.	12 Oktoba, 2009	Bw. Alberia Kacom	Mkurugenzi Mkaazi wa UNDP
26.	12 Oktoba, 2009	Bi. Diana Coner	Balozi wa Uingereza nchini Tanzania
27.	19 Oktoba, 2009	Bw. Koichiro Matsanra	Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO
28.	29 Oktoba, 2009	Mhe. Abdul-Mounaan Ahriz	Balozi wa Algeria nchini Tanzania
29.	25 Novemba, 2009	Dk. Cheikh Tidiane	Mkurugenzi na Mwakilishi Mkaazi wa UNESCO
30.	3 Disemba, 2009	Mhe. Alfonso Lenhard	Balozi mpya wa Marekani
31.	7 Disemba, 2009	Profesa Anna Tibaijuka	Mkurugenzi Mtendaji wa UN HABITAT
32.	21 Disemba, 2009	Bw. Jose Piquer	Rais wa Neurosurgical Education Development kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi – Kenya
33.	18 Februari, 2010	Bw. John Murray, Bw. Dieter Schelling na Bw. Bonas Mchomru	Mkurugenzi Mkaazi wa Benki ya Dunia Tanzania/Burundi
34.	6 Machi, 2010	Mhe. Aires Bonifacio	Waziri Mkuu wa Msumbiji
35.	29 Aprili, 2010	Bw. Ibrahim M. Al-Shigair	Kiongozi wa Mfuko wa Saudi Arabia pamoja na viongozi wa Benki ya Kiarabu wa Maendeleo ya Afrika
36.	9 Mei, 2010	Bibi Helen Clarke	Msimamizi Mkuu wa Miradi ya Maendeleo (UNDP)

37.	12 Mei, 2010	Mhe. Tim Clarke	Kiongozi wa Mabalozi wa Umoja wa Ulaya akiongozana na Mabalozi mbali mbali wa Umoja huo

KIAMBATANISHO "B"

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TUME YA UTUMISHI SERIKALINI KWA MWAKA 2009/2010

NAM.	**KAZI**	**IDADI YA WATUMISHI WALIOZINGATIWA**
1.	KUTHIBITISHWA KAZINI	416
2.	MAREKEBISHO YA MSHAHARA	3
3.	KUPANDISHWA CHEO	3
4.	KUSIKILIZA RUFAA	7
	JUMLA	**429**

KIAMBATANISHO "C"

WAFANYAKAZI WALIOSHIRIKI KUFANYA MITIHANI YA KITAALAMU KATIKA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA KWA MWAKA 2009/2010

NO.	WIZARA	IDADI YA WAFANYAKAZI
1.	WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO	10
2.	WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII	4
3.	WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI	4
4.	WIZARA YA NCHI (AR) TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA SMZ	8
5.	WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI	2
6.	WIZARA YA NCHI AFISI YA WAZIRI KIONGOZI	2
7.	WIZARA YA KAZI, VIJANA, MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO	3
8.	WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA	11
9.	WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA	8
10.	WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI	3
	JUMLA	**55**

KIAMBATANISHO "D"

WATUMISHI WALIOPATA MAFUNZO MAFUPI NCHI ZA NJE JULAI 2009/2010

NAM	AINA YA MAFUNZO	NCHI	JUMLA
1	Radio transmission	China	3
2	Water Harvesting and Irrigation	China	5
3	Health Care Management	China	8
4	Hotel Management and Tourism	China	9
5	Economic Management	China	7
6	Project Management	China	5
7	International Training Program in Human Resource Planning and Development	INDIA	2
8	Governance and Management of Non Profit Organization	INDIA	2
9	Telecom Networking Planning and Engineering	INDIA	1
10	Advanced Certificate course in Information and Technology in Education and Training	INDIA	1
11	Human Resource Development and Entrepreneurship Education Training	INDIA	1

12	Tourism and Hospital Management	INDIA	1
13	Enterprises Development through Micro Finance (EDMF)	INDIA	1
14	International Training Program Prevention of HIV/AID in the World of Work	INDIA	1
15	Empowerment of Women through Enterprises	INDIA	1
16	Management Development Program on Operation Maintenance and Repair of Biomedical Equipment	INDIA	1
17	Computer Network Engineering and Management	INDIA	1
18	Advanced Course in Multimedia and Web Design Technology	INDIA	1
19	Advanced Diploma Course in Human Resource Planning and Development	INDIA	1
20	International Training Program in Manpower Research	INDIA	1
21	Certificate in Database Administration and E-Commence	INDIA	1
22	Diploma in Mobile Communication -GSM and CDMA	INDIA	1
23	international Training in Legislative Drafting (LD)	INDIA	1
24	Training Method and skill for Managers (TMSM)	INDIA	1

25	Certificate Course on Modern Library Practices	INDIA	
25	Training Program on information and Network Security	INDIA	1
27	Capacity Building for Providing Alternative Livehood Opportunity for poor	INDIA	1
28	Optical Fibre System	INDIA	1
29	Diploma in Advanced Network	INDIA	1
	Master in Public Policy	JAPAN	1
30	Training Program on information and communication Technology	JAPAN	2
31	International Training Program on Labour and Employment Relation in Global Economy	INDIA	1
32	Master in Human Resource Planning and Development	INDIA	1
33	International Business	South Korea	1
34	Development Study	South Korea	1

KIAMBATANISHO "E"

WAFANYAKAZI WANAOTEGEMEA KUSTAAFU KAZI
KWA MWAKA WA 2010/2011

S/N	JINA LA WIZARA	UNGUJA	PEMBA	JUMLA
1	**AFISI YA RAIS IKULU**	3	-	3
2	**AFISI YA WAZIRI KIONGOZI**	3	-	3
3	**KATIBA NA UTAWALA BORA**	7	3	10
4	**AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA**	21	9	30
5	**WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**	3	1	4
6	**WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**	33	8	41
7	**WIZARA YA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO**	17	-	17
8	**WIZARA YA MAJI UJENZI NISHATI NA ARDHI**	37	4	41
9	**WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI**	25	36	61
10	**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**	32	46	78
11	**WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA MAZINGIRA**	37	11	48
12	**WIZARA YA UTALII BIASHARA NA UWEKEZAJI**	2	3	5
13	**WIZARA YA KAZI MAENDELEO YA VIJANA WANAWAKE NA WATOTO**	-	-	-
		220	**121**	**341**

KIAMBATANISHO “F”

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA ZANZIBAR

TAARIFA YA MAFUNZO YA MUDA MFUPI YA KIUONGOZI NA KIUTAWALA KWA MAKATIBU WA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA UNGUJA

N.	**HALMASHAURI**	**AINA YA MAFUNZO**	**IDADI**
1	WILAYA YA MAGHARIBI	UONGOZI NA UTAWALA	1
2	WILAYA YA KASKAZINI ‘A’	UONGOZI NA UTAWALA	1
3	WILAYA YA KUSINI	UONGOZI NA UTAWALA	1
4	WILAYA YA KASKAZINI ‘B’	UONGOZI NA UTAWALA	1

KIAMBATANISHO "G"

WAFANYAKAZI WA AFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI WALIOPATIWA UDHAMINI NA KUPATA MIKOPO MBALI MBALI
MWAKA 2009/2010

NAM	JINA LA BENKI /TAASISI	IDADI YA WATUMISHI WALIOKOPA
1.	BENKI YA WATU WA ZANZIBAR LIMITED	101
2.	BENKI YA POSTA TANZANIA	31
3.	SHIRIKA LA BIASHARA YA MAGARI	6
	JUMLA	**138**

KIAMBATANISHO “H”

TAASISI/WIZARA ZILIZOKAGULIWA NA KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI 2009/2010

NO	IDARA/TAASISI
1.	HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI “A”
2.	HALAMASHURI YA WILAYA YA KASKAZINI “B”
3.	HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI
4.	HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE
5.	HALMASHAURI YA WILAYA YA WETE
6.	BARAZA LA MJI WA CHAKE CHAKE
7.	BARAZA LA MJI WA WETE

KIAMBATANISHO "I"

WIZARA NA TAASISI ZILIZO WASILISHA MAOMBI YA KUTAKA KUFANYIWA UPEKUZI KATIKA KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI

S\N	JINA LA WIZARA/TAASISI	IDADI YA MAOMBI
1.	WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII.	117
2.	WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI.	109
3.	BODI YA MAPATO ZANZIBAR.	23
4.	BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ).	54
5.	AFISI YA WAZIRI KIONGOZI.	43
6.	WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO.	20
7.	IDARA YA UTUMISHI SERIKALINI.	07
8.	AFISI YA USAJILI NA KADI ZA VITAMBULISHO.	08
9.	AFISI YA RAIS	05
10.	AFISI YA MKUU WA MKOA MJINI/MAGHARIBI	25
11.	TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA SMZ	36
12.	BARAZA LA WAWAKILISHI	07
13.	SHIRIKA LA UMEME (ZECO)	05
14.	MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)	05
	JUMLA	**464**

KIAMBATANISHO "J"

WAFANYAKAZI WA AFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZIWALIOPATIWA NAFASI ZA MASOMO MWAKA 2009/2010

AFISI/IDARA	KIWANGO CHA ELIMU	AINA YA MASOMO	IDADI YA WATUMISHI	JUMLA
AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI	SHAHADA YA PILI	UTAWALA	1	**2**
	STASHAHADA YA JUU	UHASIBU	1	
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI	STASHAHADA	UTAWALA WA BIASHARA	1	**2**
	CHETI	UHAZILI	1	
IDARA YA UTUMISHI SERIKALINI	SHAHADA YA PILI	UTAWALA	2	**8**
	SHAHADA YA KWANZA	UTAWALA	2	
	STASHAHADA YA UZAMILI	MAWASILIANO YA HABARI	1	
	STASHAHADA	UHASIBU	1	
	STASHAHADA	UCHUMI	1	
	STASHAHADA	RASILIMALI WATU	1	

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA	SHAHADA YA PILI	UTAWALA	1	**4**
	STASHAHADA YA UZAMILI	UJASIRIAMALI	1	
	STASHAHADA YA JUU	UONGOZI	1	
	STASHAHADA	UKUTUBI	1	
MIPANGO NA SERA	CHETI	UTUNZAJI KUMBUKUMBU	1	**1**
HUDUMA ZA RAIS	CHETI	UHAZILI	1	**5**
	CHETI	UPISHI	1	
	CHETI	UHUDUMU	1	
	CHETI	UHUDUMU	1	
	CHETI	UHUDUMU	1	
IDARA YA MAWASILIANO - IKULU	SHAHADA YA PILI	MAENDELEO YA MIPANGO	1	**2**
	CHETI	UPISHI	1	
AFISI YA AFISA MDHAMINI- PEMBA	CHETI	UHUDUMU	1	**4**
	CHETI	UHUDUMU	1	
	CHETI	MASJALA	1	
	CHETI	MASJALA	1	

KIAMBATANISHO 'K'

MATUMIZIYA KAZI ZA KAWAIDA
FEDHA ZILIZOIDHINISHWA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2009/2010 NA FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MWEZI WA MEI 2010, NA FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MWAKA 2010/2011

AFISI/IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2009/2010	FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MEI,2010	FEDHA ZILIZOTUMIKA	ASILIMIA	FEDHA ZINAZOOMBWA 2010/2011
(FUNGU 07) AFISI YA URATIBU WA UCHUMI NA UHUSIANO WA KIMATAIFA	608,000,000.00	571,772,253.00	571,772,253.00	94%	651,000,000.00
JUMLA	**608,000,000.00**	**571,772,253.00**	**571,772,253.00**	**94%**	**651,000,000.00**

(**FUNGU 08**) AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI	499,456,000.00	412,349,838.00	391,608,301.00	78.4%	534,908,000.00
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI	132,210,000.00	110,941,389.00	110,848,595.00	84%	166,034,000.00
IDARA YA UTUMISHI SERIKALINI	141,168,000.00	112,036,063.00	108,790,683.00	77%	171,668,000.00
CHUO CHA UTAWALA WA UMMA	117,594,000.00	98,268,520.00	95,673,535.00	81%	145,390,000.00
JUMLA	**890,970,000.00**	**733,595,810.00**	**706,921,114.00**	**79.3%**	**1,018,000,000.00**

AFISI / IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2009/2010	FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MEI, 2010	FEDHA ZILIZOTUMIKA	ASILIMIA	FEDHA ZINAZOOMBWA 2010/2011
(FUNGU 10) AFISI YA RAIS - IKULU AFISI KUU PEMBA	175,588,000.00	172,023,236.00	I60,837,397.00	91.5%	199,207,000.00
MIPANGO NA SERA	390,627,000.00	364,329,600.00	364,329,600.00	93.2%	436,263,000.00
HUDUMA ZA RAIS	1,067,393.000.00	1,048,952,460.00	1,048,952,460.00	98.2%	1,035,968,000.00
USALAMA WA SERIKALI	24,858,000.00	24,858,000.00	24,858,000.00	100%	29,859,000.00
MAWASILIANO NA HABARI	34,734,000.00	32,889,509.00	32,889,509.00	94.6%	39,704,000.00
JUMLA	**1,693,200,000.00**	**1,643,052,805.00**	**1,631,866,966.00**	**96.5%**	**1,741,000,000.00**
JUMLA KUU	**3,192,170,000.00**	**2,948,420,868.00**	**2,910,560,333.00**	**91.2%**	**3,410,000,000.00**

KIAMBATANISHO "L"

MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO
FEDHA ZILIZODHINISHWA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2009/2010 NA FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MWEZI MEI, 2010, NA FEDHA ZINAZOOMBWA KWA MWAKA 2010/2011

AFISI/IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2009/2010	FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MEI, 2010	FEDHA ZILIZOTUMIKA	ASILIMIA	FEDHA ZINAZOOMBWA 2010/2011		JUMLA
					WAHISANI	SMZ	
(FUNGU 08) AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI 1. MPANGO WA MAREKEBISHO YA UTUMISHI WA UMMA	150,000,000.00	150,000,000.00	150,000,000.00	100%	800,000,000.00	150,000,000.00	950,000,000.00
2. UJENZI WA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA	300,000,000.00	298,299,660.00	298,299,660.00	99%	-	300,000,000.00	300,000,000.00
JUMLA	**450,000,000.00**	**448,299,660.00**	**448,299,660.00**	**100%**	**800,000,000.00**	**450,000,000.00**	**1,250,000,000.00**
(FUNGU 10) AFISI YA RAIS –IKULU MRADI WA KUIMARISHA MAWASILIANO IKULU	30,000,000.00	20,500,000.00	20,500,000.00	68.2%	-	50,000,000.00	50,000,000.00
UKARABATI NA UJENZI WA NYUMBA ZA VIONGOZI WAKUU	1,000,000,000.00	238,518,515.00	238,518,515.00	23.8%	-	1,450,000,000.00	1,450,000,000.00
JUMLA	**1,030,000,000.00**	**259,018,513.00**	**259,018,513.00**	**25.1 %**	**-**	**1,500,000,000.00**	**1,500,000,000.00**
JUMLA KUU	**1,480,000,000.00**	**707,318,173.00**	**707,318,173.00**	**47.8 %**	**800,000,000.00**	**1,950,000,000.00**	**2,750,000,000.00**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Haji Mkema Haji (Kny: Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza wa Jala kwa kunipa taufiki ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa na afya njema ili niwasilishe rasmi mchango wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu kuhusu, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu na adimu ya kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu mchango wa Kamati hii baada ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Aman Abeid Aman Karume kwa heshima na busara zake za kuiongoza Nchi yetu ya Zanzibar, kwa kuheshimu Utawala wa Katiba na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, tatu naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa jitihada zao kubwa walizozionesha na kumudu kutekeleza malengo na majukumu yao kwa bidii kubwa katika kipindi cha mwaka 2009/2010, lakini pia, kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa wakati tulipopitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuulinda muda na kwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi wanajulikana, naomba itoshe kutamka kuwa nauthamini mchango wao mkubwa walioutowa katika Kamati yetu ilipokuwa ikipitia Bajeti ya Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifuatavyo:-

AFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI (IKULU)

IDARA YA HUDUMA ZA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaiomba Idara hii kuyatunza vyema majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri mbele ya Baraza hili na kuhakikisha kuwa muda wote majengo haya yapo katika hali

ya usafi. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya majengo haya hufanyiwa usafi pale tu anapokwenda Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuifanyia matengenezo makubwa nyumba ya Serikali ya Bwefum katika mwaka wa fedha ujao.

Hii ni faraja kwetu na inadhihirisha wazi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayathamini na kuyafanyia kazi maoni ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kutamka haya kwa kifua kipana kwani katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi hii mwaka wa fedha 2009/2010 aliyoiwasilisha mbele ya Baraza hili tuliishauri Serikali kutekeleza hili na kwa mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Waziri kaahidi kulitekeleza hili katika hotuba yake ukurasa wa 37 na 38.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Kamati yetu inaomba kupatiwa ufafanuzi juu ya kiwanja cha Dodoma kinachotarajiwa kujengwa nyumba ya Maakazi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwani tuliarifiwa kuwa eneo tulilopatiwa halikuwa na hadhi inayostahiki kwa kujengwa nyumba ya Kiongozi huyu, lakini leo hii Mheshimiwa Waziri anaahidi kuwa anatarajia kujenga nyumba hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

IDARA YA MAWASILIANO

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katueleza kuwa miongoni mwa malengo yanayotarajiwa kutekelezwa na Idara ya Mawasiliano katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mwaka wa fedha ujao kuchapisha vijarida 6,000 vinavyoonesha mafanikio yaliyopatikana katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inalipongeza hilo, hata hivyo, inaiomba Serikali kuvisambaza vijarida hivyo kwa wingi Kisiwani Pemba, ili na wananchi wa huko wayajue mafanikio yaliyopatikana. Kwani kama tujuavyo kuwa kwa muda mrefu Pemba Televisheni Zanzibar haipatikani kikamilifu.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi imeridhishwa na namna Afisi hii ilivyoratibu na kusimamia vyema Miradi miwili iliyo chini ya Fungu 10, Afisi ya Rais – Ikulu. Hii ni faraja kubwa kwetu kwani inadhihirisha wazi kuwa Watendaji wa Afisi hii ni mahiri na wana uzoefu wa kutosha juu ya masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaomba kupatiwa majina halisi ya miradi inayosimamiwa na afisi hii. Hii ni kutokana na kuwa kuna utofauti wa majina ya miradi baina ya kitabu cha hotuba cha Mhe. Waziri na lile buku la Mswada wa Makadirio ya mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Kwa mfano;- ukiangalia kiambatanisho "L" cha hotuba ya Mhe. Waziri utaona miradi iliyoombewa fedha ni Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano Ikulu na Mradi wa Ukarabati na Ujenzi wa Nyumba za Viongozi. Wakati ukurasa wa 527 wa Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011 linautambua Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Rais Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, utata hasa umejitokeza kwenye Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano Ikulu na Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Rais Ikulu. Kamati yetu inaomba kujua kati ya majina mawili haya lipi jina sahihi la mradi.

AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhika na hatua zinazoendelea za Ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma huko Tunguu. Hata hivyo, tunaiomba Afisi hii izidi kusimamia vyema Mradi wa Maendeleo wa Ujenzi wa Chuo hiki. Aidha, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kukiongezea eneo Chuo cha Utawala wa Umma kwa ajili ya Ujenzi wa Majengo yake kama ilivyowaahidi wajumbe, ili chuo hiki kiweze kujenga majengo ya kisasa ya chuo na nyumba za watendaji wa chuo hicho.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhika na hatua zinazoendelea za Ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma huko Tunguu. Hata hivyo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kukiongeza eneo Chuo cha Utawala wa Umma kwa ajili ya Ujenzi wa Majengo yake kama ilivyowaahidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katuelezea kuwa Chuo cha Utawala wa Umma kwa mwaka wa fedha ujao, kinatarajia kuendelea kuifanyia marekebisho mitaala yake ili iendane sambamba na masharti ya NACTE. Mhe. Mwenyekiti, hii ni faraja kwetu kwani chuo chetu kitatoa elimu bora na itakayotambulika Kitaifa. Lakini pia, itaiwezesha Serikali kutumia gharama ndogo katika kuwasomesha Watendaji na Wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na maelezo hayo, Kamati hii inakisisitiza chuo hiki kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo, baadhi ya mapungufu yaliyotolewa na Bodi ya Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE) ilipopitisha mitaala ya Mafunzo ya Utawala wa Rasilimali Watu "Human Resource Management", ili mafunzo hayo yanayotarajiwa kutolewa na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar yaendane na wakati.

IDARA YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa malengo yanayotarajiwa kutekelezwa na Idara hii katika mwaka wa fedha 2010/2011 ni kuendelea kuratibu utoaji wa mafunzo kwa Watumishi wote wa serikali kwa kushirikiana na nchi na Wadau mbali mbali. Kamati yetu inaunga mkono lengo hilo, hata hivyo, inaishauri idara hii kuwapatia mafunzo maalum Waangalizi wa Afisi na Wakuu wa Vitengo vya Huduma katika Taasisi zote za serikali kuhusu utunzaji na usafi wa mazingira ya afisi, ili kulinda hadhi na nidhamu ya kuitendaji. Kwani imebainika kuwa wafanyakazi wa baadhi ya taasisi hawawajibiki ipasavyo na kupelekea takriban Afisi nyingi za Serikali kuwa haziridhishi kimazingira, kwa lugha nyepesi tunasema ni chafu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutolewa mafunzo hayo Kamati yetu inashauri ifanywe tathmini, na endapo itagundulika kuwa tatizo hili halijasawazika basi kada hii ifutwe na serikali iajiri Makampuni kama zinavyofanya Taasisi za Watu Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza Idara ya Utumishi Serikalini kwa kuona kuwa haja ya kuwa na sera ya muda wa kati ya ulipaji mishahara kwa wafanyakazi wa serikali. Kamati yetu inaunga mkono juhudi hizo, kwani sera hii itaweka bayana masuala ya ulipaji wa mishahara na itasaidia kuondosha malalamiko ya kuwa na wafanyakazi hewa. Hivyo, itaiwezesha rasilimali fedha kutumika zaidi kwa maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika hotuba yake katueleza kuwa Tume ya Utumishi Serikalini katika mwaka fedha 2010/2011 itaendelea kusimamia haki za wafanyakazi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuwathibitisha kazini, kusikiliza rufaa zao, kuwapandisha vyeo na kuwarekebishia mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, tumefarajika na hilo, kwani inadhihirisha wazi kuwa nchi yetu inazidi kutekeleza mikataba na maazimio mbali mbali ya Kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, kwa

kuwarejeshea walimu asilimia 25 ya posho la ufundishaji, yaani *teaching allowance*, katika mwezi wa April, 2010. Hata hivyo, kamati hii inaiomba serikali kuangalia kwa kina marekebisho haya kwani kuna malalamiko kuwa nyongeza ya miaka mitatu, Ambato kila mwalimu alistahiki kupewa, basi hawakupatiwa nyongeza hizo kama taratibu zinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo, Kamati yetu imebaini kuwa bado fursa ya ajira ya mkataba inatumiwa vibaya. Hivyo, tunaishauri Tume ya Utumishi Serikali, kuwa makini wakati inapofanya maamuzi yake na tunaiomba ifuate zaidi Sheria na Kanuni za nchi na isitekeleze majukumu yake kwa kumuangalia mtu usoni mwake au kwa shinikizo "*pressure*" za Kiongozi au Taasisi fulani.

AFISI YA URATIBU WA UCHUMI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Idara ya Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kusimamia vyema majukumu yake na kuiwezesha nchi yetu kushiriki kikamilifu katika mikutano mbali mbali ya Kimataifa, ndani na nje ya nchi na hatimae kutoa maamuzi yanayostahiki kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi maalum kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kwa kuiteua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa mwaka 2009/2010. Kuteuliwa kwake huko kunadhihirisha wazi imani waliyokuwa nayo nchi Wanachama wa Jumuiya hii juu ya uzoefu, uadilifu, umakini, uchapakazi uliotukuka na uzalendo tulionao mbele ya Mataifa mengine.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika hotuba yake katueleza miongoni mwa malengo iliyojipangia kutekeleza Idara hii, ni kuratibu na kufuatilia shughuli za ushirikiano wa Jumuiya mbali mbali za kikanda kwa lengo la kuiwezesha Zanzibar ishiriki kikamilifu na kufaidika na ushiriki huo.

Mhe. Mwenyekiti, ili lengo hilo liweze kutekelezwa ipasavyo, Kamati yetu inaishauri Idara ya Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa kuhakikisha kuwa wale walengwa ndio hasa wanaoshiriki kuiwakilisha nchi yetu. Kwani imebainika kuwa baadhi ya Watendaji hushiriki kwenye vikao pasipo na sifa zinazostahiki. Hii ni kutokana na kuwa kwenye vikao hivyo huamuliwa mambo mazito ambayo watendaji wa kawaida hawatoweza kuyatolea maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, lengo jengine linalotarajiwa kutekelezwa na idara hii ni kuendeleza juhudi za kukuza mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, kwa ajili ya maandalizi ya Tanzania katika mikutano ya ushirikiano wa Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haina pingamizi na suala hili, hata hivyo, inaiomba idara hii izidi kuwa makini na maamuzi inayoyatoa kwa mustakbali mzima wa maendeleo ya nchi yetu. Kwani Jumuiya nyingi tunazoanzisha zinaonekana zipo kibiashara zaidi kuliko kisiasa.

AFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba imeendelea kusimamia utekelezaji wa mafungu mawili ya wizara hii kwa upande wa Pemba, yaani, Fungu 08 – Afisi ya Rais, Baraza la Mapinduzi na Fungu 10 - Afisi ya Rais, Ikulu. Kamati yangu inatoa pongeza maalum kwa afisi hii kwa kutekeleza vyema majukumu yake haya kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katueleza katika ukurasa wa 44 wa hotuba yake kuwa, Afisi hii itaanza matayarisho ya ujenzi wa Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tunaunga mkono lengo hili kwa asilimia 100, kwani miongoni mwa changamoto zinazoikabili Afisi hii ni uchakavu wa jengo la afisi na ufinyu wa nafasi, ingawa jengo hili linafanyiwa matengenezo mara kwa mara. Hata hivyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri serikali kujenga Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba katika eneo lile lile ambalo kwa sasa afisi hii ipo, badala ya kujengwa kwenye kiwanja kilichopo Tibirinzi kinachotarajiwa kujengwa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Afisi ya Afisa Mdhamini.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunamaanisha kuwa afisi ya sasa ya Afisa Mdhamani ivunjwe, ili kipatikane kiwanja cha kujenga afisi mpya na watendaji wa afisi hii wapatiwe nafasi mbadala, ili waendelee na shughuli zao kwa wakati huo ambao itakuwa afisi hiyo imevunjwa. Kamati imetoa pendekezo hilo baada ya kuhisi kuwa eneo la Tibirinzi lililokusudiwa kujengwa Afisi ya Afisa Mdhamini lipo karibu na Ikulu. Hivyo, ni busara kujengwa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuliko kijengwa Afisi ya Afisa Mdhamini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu iliidhinishia Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar jumla ya Tsh. 6,160,000,000/-. Kati ya fedha hizo Tsh.3,410,000,000/- kwa kazi za Kawaida na Tsh. 2,750,000,000/- kwa kazi za Maendeleo. Hivyo, kama tulivyowaidhinishia

kwenye Kamati naliomba pia na Baraza lako tukufu liyakubali makisio haya na kuwaidhinishia Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar na taasisi zake ili wakatekeleze majukumu yao kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, haya ndio maelezo ya uchambuzi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuweza kuyagusia, natumai Waheshimwa Wajumbe wengine wa Kamati hii watayazungumzia pindi watapopata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Kwa hivyo, mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Koani, tunayaunga mkono Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar kwa asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Zakiya Omar Juma: (Mhe. Waziri Kivuli Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi): Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2010/2011 katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu shukrani za dhati, kwa kutujaalia kwa mapenzi yake na huruma kubwa kwetu sisi waja wake kwa kutujaalia hadi leo hii kuturuzuku uhai na uzima na kutukutanisha tena tukiwa wenye afya katika Baraza hili tukufu, ili kujadili mambo muhimu kwa nchi yetu na watu wake, pia kumtakia rehma na amani Mtume wetu Muhammad (S.A.W).

Mhe. Mwenyekiti, ni wengi miongoni mwetu ambao tulikuwa nao hadi asubuhi hii ya leo na hivi sasa tayari wameshatangulia mbele ya haki, wakiwemo wajumbe wa Baraza lako tukufu marehemu Mhe. Soud Yussuf Mgeni pamoja na Mhe. Daud Hassan Daud. Hivyo basi ni wajibu wetu tuwatakie msamaha na tuwaombee dua kwa Mwenyezi Mungu awapokee na awalaze mahala pema peponi amin, na sisi tulionyuma yao tumuombe Mwenyezi Mungu atupe khatima njema *Inshaallah*. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niitumie nafasi hii adhimu na adimu kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wakuu wa kisiasa, Mhe. Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dr. Amani Abeid Amani Karume na Mhe. Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, Maalim Seif Sharif Hamad, kwa ujasiri na upeo wao mkubwa na ukomavu wa hali ya juu wa kisiasa waliouchukuwa na kutuletea maridhiano ndani ya nchi yetu. Kwa kweli wamefanya jambo kubwa na jema hata mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na *Inshaallah* kwa hili iwe ndio sababu ya wao na kila atakayeliendeleza hili katika nchi yetu hii ya Zanzibar, ya kuingizwa katika pepo na Mwenyezi Mungu *Inshaallah*. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze sana Wazanzibari wote kwa jumla kwa ustahamilivu wao na ukomavu wao mkubwa wa kidemokrasia, kwa matatizo mbali mbali yaliyotokea katika kipindi hiki bali yakiwa ni mchakato wa maendeleo na kwa kuwaunga mkono viongozi wetu katika kuleta maridhiano kuelekea kuijenga Zanzibar mpya yenye amani, utulivu na matumaini.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhitimisha shukurani zangu, sasa naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu, kwa niaba ya kambi yangu ya upinzani niweze kutoa maoni juu ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2010/2011.

AFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, hii ni taasisi muhimu ambayo inapanga na kusimamia pamoja na kufuatilia shughuli zote za serikali na watumishi wake. Pia ni chombo kinachomshauri Mhe. Rais katika utekelezaji wa majukumu yake aliyopewa ndani ya madaraka yake ilikufikia matarajio ya wananchi pamoja na kutimiza ahadi alizotoa kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi aliyoinadi. Aidha, ni jukumu la afisi hii pia kushughulikia juu ya mwenendo mzima wa sera za uchumi wa nchi ambao utaleta manufaa kwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, afisi imefanikiwa vyema kuandaa vikao mbali mbali vya Baraza la Mapinduzi pamoja na vile vya Makatibu Wakuu. Aidha, imeweza kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake ndani na nje ya nchi. Ni jambo zuri, lakini bado mahitaji ni makubwa sana na mwendo bado ni wa pole. Hivyo tunaiomba afisi iongeze nguvu katika hili, na kuona kwamba wataalamu zaidi wanahitajika ili maendeleo ya haraka yaweze kupatikana na kwani utaalamu wa kisasa katika fani mbali mbali ni muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Maendeleo ya Marekebisho ya Utuimishi wa Umma umekuwa ni wimbo unaoendelea kwa kipindi chote hiki cha miaka

mitano ya awamu ya sita. Bado hadithi ni ndefu ambayo uhakika wa kumalizika kwake unatia mashaka, kwani "Mtikisiko wa Uchumi wa Dunia" bado haujatulia na mradi huu bado ni wenye kusubiri ufadhili wa Benki ya Dunia. Bado afisi inaendelea kuratibu na kusimamia dhamira hii ambapo ndio kwanza hao wataalamu elekezi na wenyeji wamekamilisha utayarishaji wa rasimu ya awali ya mageuzi hayo ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ni habari njema kuwa sasa rasimu hii imepata baraka za wahusika wote kupitia semina mbali mbali zilizofanyika Unguja na Pemba wakiwemo watendaji wa serikali na Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi, hivyo tunatarajia kuwa jambo hili liko katika hatua za mwisho kukamilika, ili mabadiliko kwa wafanyakazi na watumishi wa serikali yaweze kupatikana .

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kuwa kadiri suala hili linavyochelewa hivyo basi ndivyo wafanyakazi na watumishi wa serikali wanavyozidi kuelemewa na mzigo mzito wa maisha, kwani hali ni ngumu sana kwao kila uchao. Mahitaji muhimu yameongezeka, bei za bidhaa nazo zinapanda bila mpangilio na kwa kweli hali ni ya kukatisha tamaa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwaendeleza wafanyakazi nalo ni jambo la kuwekewa mkakati maalum, ili tuweze kuwa na wataalamu wa kutosha nchini kwetu kwani hali halisi ni kwamba tuna upungufu mkubwa wa wataalam wa kila fani, na huku tukikabiliwa na changamoto nyingi. Hivyo ni vyema kujiandaa mapema ili tuweze kukabiliana na lolote litakalotokea mbele yetu. Kwani Waswahili wamesema kuwa "nguo ya Ijumaa hufuliwa Alkhamis"

TUME YA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi inaendelea kutekeleza wajibu wake wa kusimamia haki na maadili ya wafanyakazi kama ilivyofafanuliwa na sheria ya Tume ya Utumishi. Pia inatarajiwa kutoa Utumishi kwa kuzingatia viwango na haki kufuatana na Sheria na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na shughuli nyingi zilizoelezwa, malalamiko ya watumishi kutotendewa haki au kukosa stahiki zao bado yapo. Aidha, malalamiko ya kukosa ajira nayo yanaendelea jambo ambalo linapelekea wafanyakazi kukosa imani na serikali yao ambayo ndiyo yenye wajibu wa kuwatetea na kuwalinda na kuwahakikishia kuwa haki zao za kiraia na kikatiba zinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwaelimisha wafanyakazi wa serikali juu ya sheria za kazi yaani (G.O), hili ni jambo la busara sana, kwani wafanyakazi wengi hawazielewi kanuni hizi jambo ambalo hupelekea kuwakosesha haki zao za msingi na wakati mwengine kufanya makosa bila ya kujua na kuwapa wakati mgumu katika mazingira yao ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linatakiwa liwe endelevu na semina maalum ziwepo kwa ajili ya wafanyakazi wapya kila unapofanyika uajiri, na ndipo watumishi wapangiwe kazi kwenye maeneo yao. Jambo hili litapelekea kuwepo kwa kiasi kikubwa nidhamu katika kazi na pia kiwango cha uwajibikaji kitaongezeka, kwani kila mmoja atakuwa anaelewa wajibu wake na haki zake.

IDARA YA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jukumu la kuwapatia mafunzo wafanyakazi, pia ni wajibu wa kutafuta nafasi hizo za masomo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kupata uwajibikaji mzuri na wenye ufanisi kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii kwa kushirikiana na Wahisani imeweza kuwapatia masomo wafanyakazi kadhaa nchini India, Japan na Korea ya Kusini katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mshahara tumeelezwa kuwa upandishwaji wa mshahara ulianza tangu mwaka jana kutoka Shs. 80,000/= kwa mwezi hadi Januari, 2010 ambapo ilipandishwa hadi Shs. 90,000/= kwa mwezi. Kuanzia Januari imekua ni Shs.100,000/= kwa mwezi. Suala hili tunaipongeza serikali na ni hatua nzuri, lakini bado tunaiomba serikali kwamba kima hiki kiongezeke angalau iwe ni Shs. 150,000/= kwa mwezi, badala ya Shs. 100,000/= . Ombi hili linatokana na hali halisi ya maisha yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwastaafisha wafanyakazi na watumishi waliofikia umri wa kustaafu kazi, hii ni hatua muhimu sana kwa wale wanaostaafu kwani kwao ndio wakati wa kupata tegemeo la hatima yao ya maisha na mustakbal wao baada ya kustaafu.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema idara ikajipanga vizuri katika kuwastaafisha watumishi na wafanyakazi wa serikali waliofikia umri wa kustaafu, kwa kuwaarifu mapema na pia kuwatayarishia mafao yao na kuwalipa kwa wakati muafaka ili kuwaondoshea usumbufu wa kupata haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, uzowefu ni kwamba wastaafu huwa wanapata taabu na usumbufu mkubwa katika kupata haki yao hii ya kiinua mgongo na wakati

mwengine mstaafu huhangaika hadi mauti kumfika na kiinua mgongo kurithiwa ambapo pia usumbufu mwengine hutokea kwa warathi kuweza kupewa haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa watumishi na wafanyakazi wote wa serikali wanafahamika, basi ni vyema ukawekwa utaratibu mzuri na unaofahamika, pia uwe wa kudumu ili suala hili la haki za wastaafu liweze kushughulikiwa mapema na haki zao zipatikane kwa wakati unaofaa, ambapo mtumishi anayestaafu siku anayoondoka apewe haki zake zote. Hili linawezekana idara ikijipanga vizuri. Aidha, na kiwango cha pencheni nacho tunaomba kipandishwe, badala ya Shs. 25,000/= za sasa hivi angalau kifikie Shs.75,000/= kwani kiwango kilichopangwa ni kidogo mno.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uajiri na kujaza nafasi zilizoachwa wazi na wastaafu kwa mujibu wa mahitaji ya mawizara na serikali ni kwamba, msisitizo maalum uwekwe katika zoezi hili, ili uzingatie maeneo yote ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na kuondosha malalamiko ya kila siku, kwani kumekuwepo na dhana ya ubaguzi juu ya suala hili la uajiri.

Mhe. Mwenyekiti, wajenzi wa Zanzibar yetu ni sisi Wazanzibari wenyewe na Zanzibar ni Unguja na Pemba. Almuradi vigezo na viwango vya wafanyakazi vinavyotakiwa viwe vimefikiwa na kutimia kwani kila mmoja wetu ana mchango wake katika ujenzi wa nchi yetu ili maendeleo yaweze kupatikana, “Inawezekana sote tutimize wajibu wetu”.

IDARA YA HUDUMA YA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Huduma ya Rais, miongoni mwa kazi zake ni pamoja na kutoa huduma bora za makaazi, chakula pamoja na mahitaji muhimu yakiwemo ya usafiri kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na wageni wake, pia kufanikisha shughuli zote za kitaifa na kimataifa kupitia ofisi ya faragha.

Mhe. Mwenyekiti, katika kazi zake za kufanyia matengenezo majengo ya Ikulu, idara imefanikiwa kukamilisha matengenezo makubwa katika Ikulu ya Kibweni. Kwa kiasi cha kuridhisha Ikulu ya Mnazi mmoja pamoja na Ikulu nyengine. Aidha, kuweka vifaa ndani kwa majengo ya Pemba, Dodoma na Dar es Salaam pamoja na kununua samani mpya kwa ajili ya kumbi za Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi ambayo idara hii imeyafanya ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake, lakini bado hali inatakiwa iimarishwe zaidi, hasa katika majengo ya Ikulu zetu kwa kuitafutia na kuiunganishia mitambo ya kiusalama, ili kuimarisha ulinzi wa kisasa, kwani

utaratibu wa kulinda kwa bunduki pekee ni wa kizamani. Kwa hivyo, tujitahidi kuwa na taratibu mpya na za kisasa za kiulinzi kwa kutumia kamera za kisasa za (*CCTV*), utaratibu ambao ndio unaotumika ulimwengu.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo tunaishukuru idara kwa juhudi na hatua kubwa iliyofikia, kwani kilichofanywa ni chenye kuonekana na si hadithi ya maandishi, tunawapongeza sana.

IDARA YA MAWASILIANO NA HABARI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano na Habari katika kipindi hichi imeweza kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za habari na mawasiliano, pamoja na kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi katika dhana ya kupanua wigo wa ushirikishwaji wa wananchi. Aidha, kutambua haki ya wananchi kupatiwa taarifa juu ya mambo mbali mbali ya serikali na utekelezaji wake wa misingi ya demokrasia na utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, Idara katika utendaji wake inafanya kazi kwa karibu na maafisa wa mawasiliano wa wizara na taasisi mbali mbali za serikali ya SMZ, pamoja na kutoa machapisho mbali mbali yanayoonesha shughuli za kimaendeleo zilizofanywa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tuliweza kushuhudia hata mapokezi ya waya wa umeme huko Tanga, na upokeaji wake uliofanyika huko Mkumbuu kisiwani Pemba, pamoja na mengine mengi ambayo Mhe. Rais ameyafanya. Suala hili tungeliomba liendelee.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nadhani kuwa idara hii ingelifanya ni kufuatilia yale mambo ambayo Mhe. Rais katika shughuli zake za kawaida, amekuwa akiyatolea ahadi na kuhakikisha kuwa yanafuatiliwa na yanakamilika kwa wakati kama yalivyoahidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haileti sura nzuri hata kidogo kuwa Rais wa nchi anatoa ahadi au agizo halafu likawa halitekelezwi! Mwaka jana nilikumbusha kuhusu ahadi ya Mhe. Rais ya kutengenezwa kwa barabara ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii huko Maruhubi ambayo ni ahadi tangu tarehe 22 Januari mwaka 2009 na hadi leo hii hakuna chochote kinachoendelea.

Hivyo katika utunzaji wa kumbukumbu na masuala haya yawemo, ili yaweze kufuatiliwa na pia utekelezaji wake uonekane, maana kwa sasa ilikuwa tuzungumzie mengine. Kwa hivyo, tunaiomba wizara kupitia idara yake hii kulishughulikia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuyatekeleza na kuyafanikisha haya, ndipo hapo tutakuwa tunaonesha uwajibikaji na pia kuyaenzi maagizo ya viongozi wetu, ndipo wananchi watakapofahamu yale Rais wao anayoyafanya kutokana na ahadi alizotoa.

AFISI YA URATIBU WA UCHUMI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Mhe. Mwenyekiti, kazi za afisi hii ni kutoa ushauri wa Kiuchumi na Kuratibu shughuli za Uhusiano wa Kimataifa na kufuatilia masuala yatokanayo na mazungumzo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Viongozi wa Nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayotembelea hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia afisi inaratibu mambo ya Ushirikiano wa Jumuia za Kikanda, ambapo Tanzania ni mwanachama, ili kuitayarisha Zanzibar iweze kushiriki katika Jumuiya hizo. Kwa lengo la kuendeleza juhudi za kukuza mashirikiano baina ya Zanzibar na Bara, kwa ajili ya kufanya vikao vya pamoja kwa maandalizi ya Tanzania kushiriki kwenye Mikutano ya Ushirikiano, kuendeleza juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuimarisha uhusiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa.

Pamoja na vikao na mikutano mingi, ambayo Zanzibar huwa inashiriki huku ikiwa imefunikwa mwamvuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, bado tunatujiulize hasa Zanzibar ni lipi tunafaidika nalo. Vile vile kuna tatizo gani kwa Zanzibar kuweza kushiriki yenyewe kama nchi kama tulivyoungana mwaka 1964. Kwani utaratibu huu ndio unaotuongezea kero kila uchao.

Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi tu yamefikiwa makubaliano baada ya majadiliano makali kuhusu Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi pamoja na Nchi za Ulaya *(EPA-Economic Patnership Agreement)*, ambao utasainiwa mwezi Novemba mwaka huu. Jee, nafasi ya Zanzibar ni ipi baada ya makubaliano hayo? Vile vile na masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan suala la Soko la Pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuru ya Muungano, ambao ndio wenye uanachama wanashukuru sana kwamba katika hili suala la ardhi halimo, kwani ndio sehemu hatari zaidi kwa nchi yao. Aidha wakasema kuwa nchi kama Angola, Congo na Tanzania ni nchi tajiri katika Bara la Afrika kuliko hata nchi nyengine za Ulaya na pia zinazo rasilimali nyingi.

Katika suala hili wenzetu wameonesha wazi kuwa suala hili ni kama kujitia kitanzi, na kwamba wamefanya makosa makubwa kujitumbukiza kichwa kichwa. Haya aliyatamka kiongozi, Bwana Hans Kitine katika kipindi maarufu

cha Channel 10, Jee! Tutafika? Vile vile wakasema pia kwa hali ilivyo ushirikiano huu hautufai!

Mhe. Mwenyekiti, walichokisema wenzetu ni sahihi kabisa kwamba ni vyema kutizama maslahi yetu kwanza kabla ya kujitia tu kwenye mambo, ambayo baadaye tunajikuta na majuto makubwa. Lakini wenzetu nao tunapolalamika kuwa Zanzibar haitendewi haki kwa kuondolewa kuwa mwanachama kamili wa jumuiya hii, watuelewe kwamba kila mmoja miongoni mwetu huwa anataka kuchunga maslahi yake kwanza. Zanzibar kama nchi nayo hufanya ambavyo na wao wamefanya isionekane ni ukorofi au ikawa nongwa *(Makofi)*.

Kuhusu Mahusiano ya Kifedha ndani ya Jamhuri ya Muungano Waziri Anayeshughulikia Mambo ya Fedha na Uchumi, ametuambia kuwa kuna mambo sita ambayo yameweza kupatiwa ufumbuzi kupitia vikao vya kutatua kero na mengine yanaendelea kujadiliwa ili kupata ufumbuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunapongeza hatua zilizofikiwa japokuwa jitihada kubwa zaidi na ujasiri unahitajika katika hili. Kuhusu mambo yaliyokubaliwa kwa mtizamo wetu ni matatu tu na wala sio sita, ambayo kwa mujibu wa kitabu chetu cha Hotuba ya Bajeti ya Serikali, yapo katika ukurasa wa 76 na 77 kwenye vipengele (d), (e) na (f). Lakini kuna mambo mengine matatu ambayo tunadhani kuwa bado hayajakaa sawa pamoja na kuambiwa kuwa yamepatiwa ufumbuzi *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Ugawaji wa Mikopo ya Kibajeti *(General Budget Support- Credit)* ni kwamba tokea 2003/2004 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata mikopo ya masharti nafuu. Lakini Zanzibar haikuwa ikinufaika, pamoja na kwamba wenzetu wanaelewa kuwa Muungano upo. Hii imekuwa ni tabia iliyojengeka kwamba Zanzibar mpaka tuombe, hili halitupendezi na inaonesha kutokuwepo kwa nia njema kwa wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, kumbe hata hivyo wenzetu waliona kuwa Zanzibar haina haki mpaka pale yalipofanyika majadiliano, ndipo ilipoonekana kwamba kumbe tuna haki. Kutokana na hali hiyo ndipo kuanzia 2009/2010 Zanzibar nayo ikaanza kupata haki hiyo ya kufikiriwa, sasa pia tushirikishwe katika kutafuta hiyo mikopo kwa wahisani mbali mbali. Hata hivyo, tunalojiuliza ni hii asilimia 4.5 imetokea wapi na ni kigezo gani kimetumika kuipata asilimia hiyo. Jee, katika kuitafuta hiyo mikopo nayo tuitafute kwa asilimia hiyo ya 4.5?

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Mgawanyo wa fedha zitokanazo na misamaha ya madeni, ambacho ni kipengele kimoja miongoni mwa vile tulivyoambiwa

vimepata ufumbuzi, halina maelezo yanayojitosheleza, kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepata fedha hiyo na hivyo suala hili limetatuliwa! Sasa tunajiuliza kivipi? Kwa utaratibu upi na ni kiasi gani cha fedha hizo zilizopatikana? Aidha tunataka kujua ni kwa kila baada ya muda gani fedha hizo zinapatikana, inaonekana hapa kuna mambo yaliyojificha hivyo ni vyema suala hili likawekwa wazi, ili kila mmoja wetu akaelewa.

Vile vile kuhusu suala la uwezo wa SMZ kukopa ndani na nje ya nchi na kwamba kimsingi limepatiwa ufumbuzi na SMZ inakopa *BoT* na Wizara ya Fedha na Uchumi ya Jamhuri ya Muungano! Tunachojiuliza hapa ni kwa nini tupangiwe pa kukopa na ilhali deni tutalipa sisi? Aidha masuala ya uchumi si mambo ya muungano sasa kulikoni? Hiki ni kiini macho, na kwa kweli ni kuizuilia Zanzibar haki yake ya kujenga uchumi wake kwa vile inavyoona wenyewe inafaa.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi hapa tungeelezwa kuhusu haki ya Zanzibar itokanayo na mchango na hisa zake, ambazo zilianzisha Benki Kuu (*BoT*) tangu mwaka 1965 ilipovunjika Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki *(East Africa Currency Board)*, ambapo hisa yetu kwa mujibu wa mchango ni asilimia 11.02. Hivyo suala sio Zanzibar kukopa *BoT*, bali ni kupewa haki yetu ya fedha kwa faida ipatikanayo *BoT*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Miradi ya Zanzibar, ambayo iliidhinishwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hadi sasa ni mradi mmoja tu, kati ya mitano ndio uliotekelezwa kwa kisingizio cha fedha.

Aidha, katika Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa pwani ya Barahari ya Hindi, Mhe. Waziri anatuambia kuwa ilianzishwa kwa madhumuni ya kuimarisha Uhusiano wa Kiuchumi na Kibiashara, ili kuimarisha historia iliyojengeka baina ya nchi hizo kwa karne nyingi tokea kuanzishwa kwake. Sasa chakujiuliza ni kwa nini Zanzibar imetolewa kuwa mwanachama kamili? Tunamuomba Mhe. Waziri atupe maelezo yanayoeleweka *(Makofi)*.

Ushauri wangu katika hili kwanza, kwa kuwa Zanzibar iliungana na Tanganyika kama nchi kamili, basi ni vyema wenzetu wakaheshimu hilo. Hivyo Zanzibar iwe na haki ya kushiriki kama nchi kamili katika Jumuiya yoyote itakayo ikiwemo hiyo ya Afrika Mashariki. Aidha, kwakuwa mambo ya uchumi hayamo katika mambo ya muungano, basi Zanzibar iwe na haki kamili ya kushughulikia masuala yake ya kiuchumi bila ya kuwekewa pingamizi au masharti yoyote.
Mhe. Mwenyekiti, ili kuondokana na manung'uniko yatokanayo na muungano huu, ni vyema pande mbili za muungano zikae na kuzungumzia matatizo

yaliyopo kupitia mkataba wa awali (*Articles of Union*) na kurekebisha kasoro zilizopo, kwa lengo la kuimarisha muungano ambao unahitaji kuwepo kwa ridhaa ya pande zote mbili.

KITENGO CHA USALAMA (*GSO*)

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kubwa la kitengo hiki ni kufanya upekuzi kwa watumishi wa serikali na waajiriwa kila unapofanyika uajiri mpya. Aidha kufanya ukaguzi katika majengo na afisi za serikali na kutoa ushauri kwa mujibu wanavyoona inafaa kwa usalama na pia kuhakikisha kuwa siri za serikali zinalindwa na kudhibitiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa ni wajibu wa kila mtumishi wa umma kuzingatia na kudhibiti usalama na siri za serikali pamoja na taasisi zake. Lakini ni dhahiri pia kuwa ni jukumu la serikali pia kujenga hayo mazingira na kuwajenga watumishi kiitikadi, ili kufanikisha hilo. Itikadi ambayo huandaliwa na kujengwa kwa watu wote wa nchi husika, ambao hutanguliza uzalendo wao mbele kuliko kitu chochote kwa maslahi ya nchi yao na mambo mengine hufuata nyuma ikiwemo ya itikadi za kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu unaoendelea hivi sasa unawakosesha imani wananchi, kwa kuwa itikadi za kisiasa zinaonekana kutawala na hivyo kukosesha haki wale wadhaniwao kuwa na itikadi tofauti na kujiona kama ni raia wa daraja la pili.

Katika kuhakikisha tunajenga itikadi ya Zanzibar mpya, tuone kuwa hiyo ni kasoro na kitengo hiki kina wajibu wa kubadili mifumo yake, ili iweze kuwajenga imani wananchi na nchi yao, viongozi pamoja na serikali yao.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuitetea, kuilinda na kuipigania nchi yetu ya Zanzibar kimamlaka, kiuchumi pamoja na rasilimali zake na watu wake ni jambo la wajibu mkubwa kwetu pia kunahitaji umoja na mashirikiano yaliyo thabit. Aidha kunahitaji kuwa mashirikiano yaliyo thabit kwa viongozi pamoja na wananchi kwa jumla, tukiongozwa na nia njema, ambayo inatawaliwa na uzalendo kwa maslahi ya Wazanzibari kwanza na kuona kwamba maslahi binafsi tunayapa mgongo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuelekea kuijenga Zanzibar mpya, ni vyema tukaacha tofauti zetu zote na tukawa kitu kimoja, ili tuweze kuijenga nchi yetu na

kuiletea maendeleo ya haraka na kurejesha hadhi yake na kudumisha amani tuliyoirithi kwa mababu zetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio yangu kuwa mchango huu wa maoni na ushauri tulioutoa, utachukuliwa na kuzingatiwa kwa kufanyiwa kazi ipasavyo, ili lile lengo la mafanikio liweze kufikiwa kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake pamoja na vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, kwa niaba ya Kambi yangu ya Upinzani. Aidha nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza.

Mungu ibariki Zanzibar na wanaoitakia mema Zanzibar pamoja na Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano ya hotuba hii na kama tulivyokubaliana kila atayechangia atatumia muda wa dakika 15.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi ya mwanzo kuchangia hotuba hii muhimu ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi, Katibu Mkuu wa Afisi ya Rais pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kutuletea hotuba hii, ambayo tunasema baada ya miaka 10 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anahitimisha katika Baraza hili muhimu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli natoa pongezi zangu dhati hasa nikizingatia kwamba nimefanyanaye kazi kwa karibu kwa muda wa miaka 10 akiwa Rais wa nchi hii *(Makofi)*.

Lakini nampongeza kwa muda wa miaka mitano ya kipindi cha 1995 mpaka 2000 alipokuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi tulikuwa pamoja ndani ya Baraza hili. Kwa hivyo, ninampongeza sana kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa Awamu hii ya Sita *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna mtu mbaya katika ulimwengu huu kama mtu ambaye hana shukurani na wala hakuna mtu mwenyekulaaniwa na Mwenyezi Mungu kama huyo, yaani tulikotoka na tulipo kwenye Baraza hili la Wawakilishi. Kwa hivyo, sijui kama atatokea Mjumbe mmoja wa Baraza hili tukufu na kusema kwamba Rais wetu hajatufanyia mema, basi mtu huyo anakwenda motoni *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli ninaamini kwa dhati kabisa tulikuwa mbali sana na tulipo hivi sasa ni karibu. Kwa maana hiyo, niseme tu kuwa ninampongeza Rais wa Zanzibar, Mhe. Waziri Kiongozi, Mawaziri wote, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote katika sekta tofauti za nchi yetu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mahusiano mema ni zuri sana katika ulimwengu. Mwenyezi Mungu anapenda sana watu kuwa na mahusiano mema ikiwa familia, jirani na wengineo na hapo ndipo maendeleo ya nchi yanapokuja. Kwa hiyo, Mhe. Rais katika wizara yake hii ameweka Kitengo Maalum cha Mawasiliano mazuri na nchi za nje na kimeleta faraja *(Makofi)*.

Tukifungua kitabu hiki chetu cha hotuba ya bajeti kwenye ukurasa wa 49 mpaka 50 tukiacha huu mwezi wa Juni, Mhe. Rais wa Zanzibar amekutana na wageni 37, ambao ni mashuhuri kutoka nchi mbali mbali pamoja na mashirika ya kimataifa.

Vile vile katika huu mwezi wa Juni nimewaona wengine kutoka China, ambao walituletea gari aina ya *Bus* kwa ajili ya Huduma ya Damu. Kwa hivyo, sitaki kuzitaja nchi hizo pamoja na mashirika hayo kwani nikiyataja muda utapotea, isipokuwa nilete mahusianao hayo yamezaa nini.

Mhe. Mwenyekiti, mahusiano haya mazuri aliyoyatandika Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kupitia kitengo hiki pamoja na watendaji wake, kwa kweli kimeleta faraja zifuatazo:-

Kwanza baada ya mazungumzo mazuri ya kutafuta wafadhili mbali mbali, kwa sababu kuna usemi mmoja unaosema “kuomba vibaya”. Lakini kuomba kwa nia njema si vibaya na neema ile ikawanufaisha watu, basi wewe ni mtu wa peponi *(Makofi)*.

Mhe. Rais wa Zanzibar amepata miradi mikubwa sana ya maji katika nchi yetu, ambayo ninaweza kusema kwamba mimi tokea mwaka 1995 niko kwenye Baraza hili nilimegeuzwa jina na kuitwa Ali SEMUSO, yaani nikisimama kuchangia kuhusu Wizara ya Maji, basi naitwa jina hilo.

Kwa sababu nilikuwa na mradi mzuri ambao ni mkubwa, lakini nasema matunda yake hivi sasa wananchi wangu kwa asilimia kubwa watafaidika kwa muda mdogo baada ya kuunganishwa bomba la mwisho. Lakini niseme kwamba umezaa matunda.

Mradi wa Maji katika Mkoa wa Mjini pamoja na vijijini hali imebadilika na wananchi wamefaidika kwa asilimia kubwa sana. Kwa maana hiyo, tumpongeze sana Mhe. Rais pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi hii nzuri, Mwenyezi Mungu amjaalie apumzike vyema na wala tusimbughudhi. Jambo la msingi tumuunge mkono na Mwenyezi Mungu atamlipa mema haya leo na kesho tunakokwenda *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo kubwa ambalo limetokea katika nchi yetu kuliko historia ya umeme kutoka kwetu Tanga mpaka Pemba. Kwa karne zilizopita tulishuhudia Pemba hawana umeme wa uhakika, yaani wanatumia umeme kutokana na vinu vinavyotumia mafuta ya *IDO*, mara mafuta yamekwisha na umeme hakuna kisa. Kwa mfano, mtu anapotoka Unguja kwenda Pemba anapanga mashauri, anaanza kuuliza *line* ipi inazimwa A au B, kwa sababu wakati huo nilishuhudia mwenyewe.

Vile vile kwa bahati nzuri huu umeme kutoka Tanga, wakati ulipowashwa nilikuwepo Pemba kwa muda wa wiki moja, basi nilimshukuru Mwenyezi Mungu, kwani sikupata shida.

Kwa hivyo, hali hii yote inaonesha kwamba utendaji mzuri, busara pamoja na mahusiano mema na wenzetu nje. Kwa maana hiyo, tumpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hili *(Makofi)*.

Ikiwa watu wa Pemba hawakushukuru na pamoja na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, basi sijui niseme ni katika kundi gani, sijui hiari yao. Lakini naamini kitendo hiki kama ingekuwa amekifanya kwenye jimbo langu, basi ningeitisha mkutano mkubwa wa hadhara kwa ajili ya kumpongeza.

Kwa hiyo, wenye majimbo Pemba hiari yenu. Kwa kweli kutokana na hili lazima tukae na kufikiri hatua hii si ndogo katika maisha ya binadam, yaani tumpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu kukosekana kwa umeme katika Kisiwa cha Unguja kwa muda wa miezi mitatu. Kwa kweli Mhe. Rais wa Zanzibar alikwenda mbio kwa juhudi zote, watu walikuwa wakisema Mhe. Rais amestarehe kwake. Kutokana na hadhi yake ya Rais na yetu sisi ni tofauti, kwani anapotakiwa kukaa lazima pawe na usalama zaidi kuliko atakapokaa Ali

Suleiman Ali (Shihada), kwani anaweza kujikinga mwenyewe, lakini Rais ndio roho ya nchi yetu.

Kwa hivyo, kama mtu anao uwezo wa kumiliki *generator* anaweza kutumia, kwa sababu hakukatazwa mtu na watu walikuwa wakiwasha *generators* kutwa kucha. Lakini tuseme kwamba juhudi aliyoifanya imezaa matunda mapya, baada ya kukosa umeme kwa muda wa miezi mitatu, basi jana *generators* zimeteremshwa 36 kwa ajili ya akiba, wakati wowote inapotokezea dharura, huduma ya umeme itaendelea na wala hakuna wasi wasi. Kwa maana hiyo, tumpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ni visiwa tunategemea usafiri wa gati. Nashukuru Gati ya Wete, Wesha na Mkoani limejengwa banda zuri pamoja na Wete, kuliko hapa Unguja, yaani ukienda hapa unasumbuka. Lakini ukiingia kule unahakika upo pahala pa usalama. Kwa mfano, boti imekukimbia unaweza kulala hapo bila ya wasi wasi *(Makofi)*.

Kwa hiyo, yote haya ni maendeleo yake, busara pamoja na uwezo aliomjaalia Mwenyezi Mungu kwamba tutafute kitu cha kuwanufaisha wananchi wetu *(Makofi)*.

Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar hasa baada ya umalizaji wa ujenzi wa Gati ya Zanzibar pamoja na vifaa vyake vya kufanyiakazi. Kwa kweli hivi sasa inafanyakazi vizuri sana. Kwa mfano, baada ya kutumia muda wa masaa matatu, basi inaweza kutumia dakika 20 au 30 na watu wameshamaliza kazi na meli kuondoka. Kutokana na hali hiyo, inaonesha kwamba yote ni busara pamoja na taratibu zake za kuhangaika kwa ajili ya kutafuta maendeleo ya nchi hii *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inategemea sana viwanja vya ndege. Kwa kweli watalii wanapotoka kwao wanategemea sana usafiri mkubwa kutumia anga. Kwa hivyo, hivi sasa kwa asilimia kubwa sana tumepata faraja uwanja wetu umefanyiwa wasawazisho makubwa, yaani umekuzwa zaidi na unaendelea kukuzwa na tunaendelea katika mazingira ya kileo.

Mhe. Waziri, ametueleza kwamba pamoja na juhudi zote hizo yale mambo ya majengo yote yaongezewe ufanisi wa kileo, kwani hatutaki wageni wakae pale na kupigwa na jua na mvua, yaani kila kitu kiwe katika hali nzuri. Hata hivyo, maendeleo yamekua na mtu ambaye ameondoka kiasi cha miaka mitano au kumi iliyopita, basi atakapokuja ataona kweli Zanzibar imebadilika.

Sasa kipindi chote cha miaka kumi ya Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Mawaziri wetu, kazi kubwa wameifanya ya usimamizi mzuri wa kuendele na shughuli zetu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, barabara zetu ilikuwa mtu anaweza kutoka mjini kwenda Makunduchi, basi analia au anakwenda Nungwi anapanga mashauri ama anakwenda kwetu Matemwe kwa Mhe. Ame Mati Wadi anapanga mashauri *(Makofi)*.

Lakini ndio yale niliyosema kama mimi ndio Mhe. Ame Mati Wadi ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe, *Wallahi* ningeitisha mkutano mkubwa kwa ajili ya kumpongeza na kumwita Mhe. Rais tena ninazo sababu zangu tatu za msingi.

Kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar jitihada zake alizozifanya kwa barabara ya Mshelishelini mpaka Pwanimchangani, wananchi wako tayari hata leo kufanywe mkutano kwa ajili ya kumpongeza Mhe. Rais, yaani watu hawakutegemea *(Makofi)*.

Vile vile barabara ya kutoka Kiwengwa au Pongwe mpaka Matemwe ni suala kubwa ambalo ni la kupigiwa mfano, ambapo Mwakilishi, Mbunge pamoja na wananchi kwa jumla washerehekee. Sasa katika kusherehekea umwite yule aliyekufanyia shughuli ile kwa ajili ya kumpongeza, namuonesha njia hiyo *(Makofi)*.

Jengine kuliko hilo barabara ya kutoka Matemwe mpaka Mkwajuni laini. Kwa kweli gari zinakwenda mpaka zinagongana njiani kutokana na mwendo wa kasi na Mwenyezi Mungu atunusuru. Kwa hivyo, yote ni maendeleo ya miaka kumi ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar. Mhe. Rais amefanya mengi na tukiwa na kinyongo kwenye roho zetu tunakwenda motoni *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu vituo vya afya *mashaallah*, ukienda Hospitali ya Mnazimmoja. Kwa mfano, juzi tuliingia na Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, wakati tulipotembelea Mkoani katika Abdalla Mzee Hospitali kwenye Kituo wanachoishi Madaktari wa Kichina, basi ukiingia hutaki kutoka na wengine tuliomba ile ramani tuipate kwa ajili ya vijiji vyetu, kwani wako tayari kutoa ushauri.

Kwa sababu wamejenga vizuri sana na wala hawataki kuondoka kwenye eneo lile, kwani wanafanyakazi vizuri, yaani wameweka sehemu ya viwanja vya michezo, kama vile *basketball*, *tennis table* na mambo mengine na yale ndio maendeleo. Kutokana na hali hiyo, lazima tumpongeze Mhe. Rais na haya yote

yanatokana na Kitengo cha Uhusiano wa Kimataifa na mambo yanakwenda vizuri *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano hivi sasa ukienda Hospitali ya Mnazimmoja mabadiliko yaliyotokea si madogo. Kwa kweli huduma zimekua nzuri kama vile kwenye macho, sehemu ya koo, masikio na pua, pia kuna kifaa ambacho kinaitwa *CT Scan* pamoja na mambo mengine. Pamoja na hayo, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, basi haya niyaeleze na nitakuja kuyaeleza zaidi katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Lakini tumpongeze kama hakuna mawasiliano mazuri au utashi wa kufuatilia yasingepatikana. Kwa kweli tumpongeze kwa moyo mmoja, yaani kwa asilimia mia moja sote katika Baraza hili na wananchi kwa jumla *(Makofi)*.

Tukiangalia suala la Sekta ya Elimu, vikiwemo Vyuo Vikuu, skuli pamoja na mambo mengine. Mhe. Rais wa Zanzibar amejitahidi na anaendeleza jitihada yake na tunaona. Kwa mfano, leo ukienda Tunguu pamebadilika pamoja na sehemu nyengine mbali mbali. Kwa hivyo, hii yote ni faraja kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Siku ya Wafanyabiashara tulialikwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukudhurie Bwawani, Mhe. Rais alisema jambo kubwa sana, kwamba Wazanzibari changamkieni biashara na wala msingojee wageni, kwa ajili ya kuchukua mali ambazo zinazalishwa hapa. Kwa sababu wageni wanatoka kwao tunaamini kuwa ni matajiri, kumbe si matajiri isipokuwa ni utaratibu tu.

Sasa Mhe. Rais wa Zanzibar alisema hivi kwamba Wazanzibari mnazo benki, basi zitumieni. Kwa mfano, benki hizi zinaweza kukukopesheni kama mtakuwa na miradi ambayo mtaweza kuiendesha na kuweza kutajirika katika maisha yenu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeyaona, kwa sababu hivi sasa ndugu yetu Ahmad Yahya si vibaya kumtaja wa SHA. Kwa kweli ndugu yetu amefungua skuli ya kupigiwa mfano katika nchi yetu hii hata Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hawana *(Makofi)*.

Kwa hivyo, hii ni hatua kubwa sana kwa Mzalendo wa nchi kuweka rasilimali kama ile kwa manufaa ya Wazanzibari. Kwa kweli ninampongeza kwa asilimia mia moja, kwani ni jasiri tena ni mwelekevu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kuhusiana na suala la Sekta Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia basi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Lakini jengine sekta binafsi, baada ya kuingia katika sehemu hiyo alisema jengine mahoteli na wanaoweza kujenga vituo vya Petroli wajenge, wamo humu watu wamejiimarisha kwa utundu wao na uwezo wao, hawana pesa, hawana waliponyang'anya lakini utaratibu wa kisheria ya mikopo tu. Mimi najitangaza kwamba Shihata kaweza na wengine nawaomba waweze. Manufaa yatakayoingia pale yanaingia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niseme kwa dhati kabisa, muda mdogo lakini haya, naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nadhani robo saa huwenda pengine nisiimalize.

Kwanza nataka nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Waziri wake Dokta Mwinyi na watendaji wote katika wizara hii kwa kutuletea hotuba hii fupi lakini inayoeleweka na kila mmoja wetu kwa urahisi.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nitakwenda katika Tume ya Utumishi Serikalini. Lengo moja la tume ya Utumishi serikalini kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 wanasema wamejiwekea lengo la kuelimisha wafanyakazi, kanuni za utumishi serikalini yaani *General Orders*.

Mheshimiwa ni habari njema, lakini mimi uzoefu nilionao kwamba hii *General Order* hao wanaoifahamu ndani ya serikali hawaifuatil, haiheshimiwi wala haifuatwi. Ni habari njema kuambiwa kwamba watu wanataka kuelimishwa. Labda sasa kutakuwa na muamko mpya, lakini Waheshimiwa mambo haya yanaonekana kama ni mambo ya ukoloni. Kuheshimu sheria za kazi, kuheshimu Kanuni za Utumishi inaonekana kama ni tabia za kikoloni.

Ukitaka ushahidi pia katika sehemu za kazi, nenda kazini saa 4: Afisini unaweza katika jengo ukakuta wafanyakazi wawili au watatu, watu wanapiga hadithi za ulela ulela, upandishwaji wa vyeo hivyo hivyo inawezekana mtu akaajiriwa miaka mitatu utamkuta kapata *promotion* aliyekaa miaka saba hapati kitu tena pengine ana elimu kubwa zaidi. Ndio nikasema kanuni za Utumishi Serikalini hazizingatiwi.

Mheshimiwa kuna watu wamepewa likizo bila ya malipo huu sijui mwaka wa ngapi, wala hawana sababu zozote masikini za Mungu basi tu, kuoneshana uwezo. Kwa kweli Kanuni za Utumishi serikalini hazifuatwi hasa ulipoingia mfumo wa vyama vingi. Lakini sasa hivi hali yetu nzuri na tumefika pahala haya majadiliano yametuweka pazuri. Mimi Mheshimiwa naomba wale watu wote waliopea likizo bila ya malipo kwa sababu tu za kisiasa warejeshwe kazini hasa walimu.

Sasa hivi Alhamdulillah Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake katupeleka pazuri, chuki imeondoka na imani imetawala. Kwa hivyo naomba wale watumishi wa serikali wote waliopewa likizo bila ya malipo kwa sababu tu ya kisiasa pengine huyu mfuasi wa chama fulani au kwa sababu tu ya fitina ya mjomba, shangazi, warejeshwe tena kazini. Mambo haya tena jamani tufunge ukurasa uliopita tufungue ukurasa mpya. Hilo ni jambo ambalo linanitia faraja lakini pia linanipa masikitiko.

Mimi nnayo Kanuni ya Utumishi serikalini nimeinunua zamani kwa Shs. 10,000. lakini kila nikiisoma na nikiangalia mambo yalivyo nnacheka hasa. Unaweza ukamkuta mwalimu kafanya kazi miaka miwili au mitatu utamkuta mwalimu mkuu, tena utakuta kuna walimu wazuri wazoefu ni walimu wa kawaida zamani haikuwa hivyo. Zamani mwalimu mkuu ulikuwa huwezi kupata cheo kwa miaka miwili ukawa mwalimu mkuu, hapana. Lakini sasa hivi tunakwenda tu mtu ukikazana kidogo, ukivaa shati la kijani tena wewe ndio tayari hapo unafaa. Sasa huko tena tutokeni jamani eeeh! Nchi hii sasa inataka maendeleo.

Jengine nije katika Idara ya Utumishi Serikalini. Idara hii mimi naipongeza kwa kutupunguzia tatizo katika Wizara ya Elimu Ahamdulillah sihaba wameajiri walimu lakini bado wale walimu hawakumaliza. Kwa kuanzia Wizara ya Elimu waliajiri walimu wa cheti 2007 na 2008 wakasema watafuatia. Lakini hata hivyo hao wa 2008 wenye jambaa zao wanavutwa kisiri siri wakiajiriwa. Waliokuwa hawana jamaa zao serikalini basi masikini za Mungu ndio wamo tu wanasota.

Sasa mambo kama haya ndiyo nikasema si mazuri katika nchi. Hivyo mtu mpaka awe na jamaa katika serikali ndio apate fursa kwa sababu mtu mnyonge tu masikini ndio akose fursa.

Mimi naomba Mhe. Waziri uiharakishie Wizara ya Elimu kuwamaliza hawa walimu wa 2008 wa cheti kwa sababu bado upungufu wa walimu tunao hasa katika Wilaya ya Mkoani na Micheweni kama inavyojulikana na Wilaya nyengine. Baadaye ningeomba tuendelee na Wilaya nyengine. Kwa sababu

Wizara ya Elimu ilijipangia kwanza kumaliza Wilaya ya Mkoani na Micheweni, imechukua nusu, hawajamaliza kazi. Kwa hivyo naomba tumalize halafu tuangalie na Wilaya nyengine. Lakini Mheshimiwa tunawaweka sana wahitimu, matokeo yake wahitimu wenye elimu za juu wanakwenda Bara. Sasa sisi itakuwa kama tunasomesha watu halafu wanakwenda kunufaisha nchi nyengine.

Mimi nadhani hii si sekta ya kuifanyia mchezo, mtu kumsomesha tokea darasa la kwanza mpaka akamaliza Chuo Kikuu au akamaliza diploma au Cheti ukifanya hesabu shilingi ngapi za serikali tulizozitumia. Halafu mtu huyu unamuachia mtu mwengine anamchukua anakwenda kumtumilia tu. Inakuwa sisi tunajifunika jua kwa chungia. Maana ukijifunika jua kwa chungio sidhani kama kunatija yoyote.

Ukiacha elimu vile vile na Wizara ya Afya. Wizara ya Afya pia kuna wahetimu tokea mwaka jana, wameajiriwa baadhi ya kada fulani mpaka leo kada nyengine wananung'unika, wanasikitika, wanahangaika. Wengine utawakuta wanakwenda kwenye maboti wanakwenda Tanganyika kutafuta kazi. Kwa kweli inakuwa tunaleta matatizo. Naomba serikali pamoja na umasikini wake lakini hasa sekta mbili sekta ya afya na uwalimu mimi nadhani hizi tungezipa ipaumbele, wahitimu wakimaliza tu serikali ikafanya mipango vijana haraka haraka tukawaajiri ili kuweza kuwadhibiti wasitukimbie. Kwa sababu ndio sekta nyeti katika nchi yetu, tusiwaweke muda mrefu vijana wakatukimbia.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika hii Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano. Hapa mimi nina suala moja. Katika kitabu ukurasa wa 31 kuna paragrafu imeeleza "Miradi ya Zanzibar ambayo iliwasilishwa *East African Community* ili iweze kutekelezwa kikanda inaendelea kupatiwa mazingatio mazuri". Kwanza ningependa kujua hiyo miradi iliyopelekwa ni miradi gani. Maana hii ni hotuba ya bajeti hakuna haja ya mafumbo mafumbo, bajeti inataka uwazi. Hapa haijatajwa ni maradi gani iliyopelekwa katika Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tutajiwe miradi hii ni miradi gani, itagharimu kiasi gani, itakuwa wapi. Inategemewa mambo yakenda vizuri itaanza lini. Hayo ndio maelezo ya kuyaleta katika Baraza hili tukufu. Lakini mambo ya mafumbo yanakuwa si pahala pale mahali kama hapa, hili itakuwa hata mara ya pili tutakuja kujjbu nini hapa. Hotuba ijayo mwakani ikiwa suala kama hili lipo ikiwa utekelezaji haupo hata na sisi itakuwa hatuna nafasi ya kuhoji. Bajeti ni vizuri impe nafasi Mwakilishi kutathmini hotuba ya mwakani yale aliyepewa mwaka uliopita. Sasa hapa tutakosa kutathmini, tuwe wazi tuambiwe ni miradi

gani, mingapi, itagharimu kiasi gani, inategemea miradi hiyo kuwa wapi na wapi. Hayo ndiyo maelezo ya kibajeti.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije katika Idara ya huduma ya Rais. Kitabu cha hotuba kimetueleza majengo mengi mara hii yamefanyiwa ukarabati, ni habari njema. Mheshimiwa kwa heshima zote namuomba Mheshimiwa Waziri lile jengo la Ikulu ya Mkoani Mkano hata kama hakuna nia ya kulitumia tena basi naomba tulitunze iwe kama kumbukumbu, lakini tusiliwache likaanguka. Kwa sababu ni pesa nyingi za serikali zimetumika, lina site nzuri, ipo siku tunaweza tukatamani tukasema turudie kulitumia, lakini sasa hivi limekaa ovyo, linatia aibu. Hata ile nyumba ya mwanzo wanayokaa walinzi haina milango, haina madirisha. Haina haiba hasa hata ukiambiwa kwamba hapa ni pahala wanapokaa viongozi wa nchi. Mambo mengine ni madogo lakini yanafedhehesha katika nchi kuambiwa ndio Ikulu. Hiyo Ikulu yenyewe utaona kuna mapazia sijui mapazia ya magunia ni mambo ambayo yanafedhehesha kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika Kitengo cha Usalama wa Serikali (GSO). Siku za nyuma kitengo hiki kilikuwa na kazi kubwa ya kufanya upekuzi kwa vijana wanaokwenda kusoma hasa Vyuo Vikuu. Nadhani kazi hii imewashinda kwa sababu sasa hivi vyuo vikuu vipo vingi. Huwenzi kumzuia mtu sasa hivi usisome hata ukifanya miujiza gani. Ukimzuia asiingie SUZA utakwenda kumkuta yupo *University* nyengine. Sasa hivi *university* zimezagaa kama uyoga. Nadhani hapa hawana kazi tena ya kudhibiti watu wasisome. Maana zamani ilikuwa mpaka uulize baba ako alizaliwa wapi, alikuwa chama gani, ulikuwa wewe ni nani. Yaani maswali yanakuwa mengi utakuta vijana wengi wanakosa kusoma. Ilikuwa siku zile vyuo vikuu ni vichache vya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo vikuu vingi na vijana ikiwa hawapewi fursa basi mtu yupo tayari kuacha kazi ili akasome. Anachukua likizo, anakwendakujisomesha mwenyewe, wameamua vijana juu ya hili. Hapa wameshindwa (GSO) kudhibiti watu wasisome. Maana zamani kulikuwa kuna watu fulani wasome na watu wengine wasisome, lakini hapa wameshindwa kabisa kabisa. Sasa hivi zaidi ni kwa wafanyakazi wale walioajiriwa. Suala langu je, katika kufanya *vetting* hawa wafanyakazi wamefanya tathmini kuna faida gani iliyopatikana kwa kipindi chote tokea kuanzisha (GSO) na kuna hasara zipi zilizopatikana. Maana mambo haya ni lazima tuyafanyie tathmini, tusiendelee na mambo yanayotutia hasara katika nchi halafu tukaendelea kuyashikilia tu. Kama kunahasara tukigundua wafanyakazi wanatukimbia basi tuache, tusishikilie mambo ambayo hayana faida na kama kuna faida basi tuendelee**.**

Mwenyekiti, jengine lilonishtua ni katika kuona wageni waliotembelea Zanzibar. Kuna jaduweli hapa linaonesha wageni mbali mbali waliotoka nje ya nchi na kuonana na Mhe. Rais wa Zanzibar. Hapa mgeni Rais ni mmoja tu kutoka Kenya (Mwai Kibaki) lakini wote waliokuja ni mabalozi, wakurugenzi. Yaani katika kipindi cha mwaka mzima Rais ni mmoja tu aliyeingia Zanzibar hajaingia Rais mwengine. Kwa maneno maraisi wote wanaoitembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanamalizikia Bara.

Hali hii inatutisha kwa sababu muungano ni sehemu mbili Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Sasa kuona kwa mwaka mzima raisi mmoja tu tena ni jirani yetu kutoka hapo Kenya. Wageni wengine wakija mkiwa mnataka kuonana nao mnaambiwa atakuwa katika Hoteli ya Movipic mwende mkaonane nae huko huko. Hii inakuwa haileti heshima kwa upande wetu wa Zanzibar . Hili nadhani nalo kama mkikaa na Serikali ya Muungano mseme kwamba Wawakilishi wetu hili hawalifurahi hata kidogo. Ikisemwa kwamba wawakilishi wetu hawalifurahii ina maana ndio wananchi wetu hawalifurahii hata kidogo.

Zamani hapa wakati wa Rais Mzee wetu Aboud Jumbe hawa mpaka Pemba walikuwa wakitembezwa. Haidhuru maendeleo yake madogo lakini walikuwa wakitembezwa mpaka Pemba walikuwa wakija wageni kutoka nje. Lakini leo mwaka mzima anakuja Mwai Kibaki kutoka Kenya, ndio Rais mmoja tu.

Jengine katika ushauri ambao ningeshauri, pamoja na kuoneshwa idadi ya wageni walionana na Rais, lakini bora katika bajeti ijayo *Inshaallah* pengine watakaobahatika kuwemo pengine *Inshaallah* Dokta Mwinyi utaendelea kuwemo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hata kama itakuwa itatawala CUF *ishallah* nategemea utakuwemo. Si tunategemea kura ya maoni tunasema *yes* bwana, tuingie serikali ya kitaifa, nina hakika kwa ujasiri wako hutoachwa.

Kuna kitu kimoja mimi napendelea tukianzishe tuweke daduweli nchi alizotembelea Rais wetu au viongozi wetu. Tusioneshe wageni waliokuja kutoka nje tu lakini tuoneshe na viongozi wetu waliokwenda nje na *cost* zao. Kwa sababu tutapata kujua je, viongozi wetu kwa mwaka huu wamekwenda nje, wametumia dola elfu 10, lakini je, wameingiza matunda kiasi gani. Maana ni lazima sasa tutathmini ziara za viongozi. Bara wenzetu wameanza kupiga kelele kwa ziara za viongozi kwamba zimekuwa nyingi matunda madogo. Lakini na viongozi wanajitetea wanasema matunda yapo makubwa. Kwa hivyo na sisi tunataka tupate fursa ya kuona viongozi wetu wamefanya ziara ngapi wametumia kiasi gani cha fedha lakini katika ziara zao wameweza kupata kiasi gani. Fursa hii katika Baraza tunaikosa. Bungeni wenzetu hii fursa wanaipata maana unakuwa unasikia kunakuwa kuna hoja nzito kuhusu ziara za viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru maneno ya kumalizia nataka niseme kwamba narudia kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hasa kwa suala hili la kutuweka pamoja Wazanzibar, tukawa kitu kimoja, tukasahau tofauti zetu, tukazika chuki zetu na Ishallah Mwenyezi Mungu ajaalie Rais atakaekuja awe na niya ya kuendeleza haya. Rais aliyekuwa na nia ya kuja kuendeleza mifarakano, Rais aliyekuwa na nia turudie ile ile ya chama kimoja ishallah Mwenyezi Mungu amjaaliye huyo asipite. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikushukuru sana, nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea hotuba hii. Vile vile nimshukuru sana Dokta Amani Karume kwa kusimamia ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa uwadilifu na uangalivu na kwa utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, sote tumekuwa mashuhuda, tumeangalia jinsi gani ilani hiyo ilivyotekelezwa katika awamu yake ya sita. Mambo mengi Mhe. Dokta Karume amefanya *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu ambariki. Unapokuwa kiongozi kuna mambo hata na sisi Wawakilishi tunayoyaahidi majimboni basi tunatahadhari nayo sana. Kwa sababu tunakwenda huko kwa *Allah* angalau uweze kufika asilimia 50 mpaka 70 kidogo yaliyobakia Mwenyezi Mungu atakusamehe. Lakini kuliko kusema nina ilani yangu lakini utekelezaji wake haitekelezi Mwenyezi Mungu atakuhukumu.

Mhe. Mwenyekiti, Dokta wetu ametimiza ahadi zake na muda ukifika anakwenda kupumzika kwa usalama usalimini, hana deni isipokuwa deni jengine analijua mwenyewe Mwenyezi Mungu na mja wake. Na *ishallah* na hilo Mwenyezi Mungu atamsamehe. Amina

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika kuchangia baada ya kumuombea dua Mhe. Rais baada ya kutuletea neema hiyo ya ilani na *Ishallah* na Chama cha Mapinduzi nacho kitashinda.

Mhe. Mwenyekiti, nende katika ukurasa wa 10 kifungu cha 17. Haya kwa kweli ni moja katika matunda mazuri sana kuona Mhe. Waziri ameliona suala hili kuwa tumechoka kurithi majumba mabovu sasa tunakwenda katika milinia iliokuwa nzuri na kuwa na afisi nzuri ambazo zina modan ya kisasa. Hilo moja tunawasifu sana na ni moja katika kuonesha jinsi gani ilani ya Chama cha Mapinduzi utekelezaji wake. Kifungu hichi nacho kinaonesha dhahiri kuwa kinaendelea kutoa viwanja vijengwe maofisi mazuri ya kileo na ya kisasa na yenye umadhubuti lisiwe kama lile la Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, majengo yatakayotengenezwa sasa hivi yatakuwa ni madhubuti yenye makandarasi wazuri, washauri wazuri. Hili nalo Mhe. Waziri uwe muangalifu sana kutokana na hii hali ambayo kuwa unatoa viwanja basi na majengo yaende na modan ya kisasa ili yaweze kuimarika vizuri yaweze kuhudumia wafanyakazi bila ya kuja kutokea ajali baadaye.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia ukurasa wa 12 Tume ya Utumishi. Kwa kweli niwapongeze sana Tume ya Utumishi ya Serikalini. Nimeona vizuri jinsi wanavyosikiliza zile kesi na katika kuwapandisha watu vyeo kwa *standard* zao zinazohusika na rufaa jinsi gani. Mimi ninachowaomba Tume waendelee kuwaelimisha wafanyakazi wa zamani na wafanyakazi hawa wapya wa sasa hivi. Kwa sababu kuna wengine wanashindwa kufahamu wapi vilio vyao vinavyotokezea makazini pa kwenda kuvipeleka.

Hata mimi nisingekuwa najua kusema ukweli, lakini nimeona humu nimejua baadae kama nitaajiriwa nikiacha uwakilishi sasa najua likitokezea tatizo la muajiri wangu wapi niende. Na hivi ndivyo inavyotakiwa. Na inaonesha Tume imepangika na ina wataalamu wazuri, ina *experience* ya watu, hususan Mwenyekiti wake, ana *experience* nzuri, muadilifu mzuri, amepita sekta mbali mbali. Nampa hongera sana kutokana na utendaji wake mzuri sana *ishallah* na yeye Mwenyezi Mungu amjaaliye ili aendelee na uadilifu wake mzuri, awasaidie watu ambao wanapata tabu katika makazi yao. Kuna mwengine anaweza akashtakiwa na muajiri wake lakini baadaye kesi akishinda akirudi ananyimwa mafao yake au anafukuzwa kazi kabisa. Hilo nalo wanaliona kwa vizuri panapostahiki hukumu wao wanatoa hukumu, panapostahiki kumrudisha mtu wanamrudisha, panapostahiki kupewa mafao yake anapewa, yalipopungua wana uwezo wa kufanya azidishiwe, Mwenyezi Mungu ndiye atakayekulipeni sisi kazi yetu kupigieni debe tu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 13 Idara ya Utumishi serikalini. Kwa kweli hili suala mimi kila nikisema na wenzangu wengine wamesimama hapa wameeleza vizuri kwa kweli tuna upungufu kwa wafanyakazi katika sehemu zetu au taasisi zetu. Mimi kilio changu siku zote na sitochoka kusema kuhusu habari ya Wizara ya Afya bado wapo haba. Hili nitaendelea kulisema na sitochoka kulisema nitalisemea kwa nguvu zangu zote. Kwa sababu ile hali naiyona kule hospitalini kila siku kukicha utakuta nesi pengine mmoja au wawili au utakuta nesi mmoja odali mmoja au wanafunzi wawili wanaosaidie ile kazi. Suala Tume tunaiomba jamani kama kuna utaalamu umeshakamilika utaalamu kama uchunguzi waliokuwa watu hewa umeshapita sasa hivi watu hewa tumeshawajua, kilichobakia tuzibeni mapengo.

Pamoja na hali yetu ya uchumi pamoja na hiyo tujisaidie ili tuweze kukidhi haja ile hali halisi. Wizara ya Afya jamani tunapoteza bure, tunasomesha kwa nguvu zetu zote hatimaye mwenzangu kasema wanahangaika na maboti sasa hivi wanafunzi wanakwenda kutafuta kazi katika sehemu nyengine. Hili suala jamani hetu tunaomba litizamwe kwa uangalifu Tume jamani fanyeni kazi yenu. Humu sikuona nafasi ngapi humu hazikutajwa lakini mnazijua nyie. Tunaomba ishawishini serikali sasa hivi muajiri, tunao watoto wazuri sana tu. Tunaomba hataka sana jamani tuzibe yale maeneo yaliyokuwa muhimu sana.

Juzi tunashukuru sana sehemu ya Sekta ya Elilmu kama kule kwetu Wizara ya Elimu imeajiri Kaskazini baadhi ya mapengo. Maana kulikuwa kuna upungufu mkubwa kwa sababu wengi wamegundulikana wanakaa mjini lakini akifika kule hata kile kipindi cha kwanza cha kusomesha kinampita, mtu anaingia saa 5 kutokana na tatizo la usafiri. Lakini sasa hivi alhamdulillah tumepewa fursa kule sasa hivi nafikiri Mkoa wa Kaskazini tutakuwa nambari *one* kutoa watoto wengi wanaopasi. Hilo nalo ni moja la kutoa pongezi.

Nikiingia ukurasa wa 17, nimefurahi sana kuona mishahara imepanga tumefikia laki moja. Nayo inastahili sifa Mhe. Waziri umejitahidi sana jitihada haipunguzi kutoa sifa mtu. Lakini pamoja na hayo tuangalie na hizi kodi kama wana kodi katika wafanyakazi hebu tuangalie upya ili angalie angalau na senti. Kwa sababu unaweza ukapandisha mshahara lakini kodi ikawa kubwa, ukakuta tukawa tunamuuliza pale pale.

Vile vile tuangalie na hii kupanda bei kwa vyakula, hetu tuiangalie, inawezekana hii laki moja ikatosha kama haya mengine yatapunguzwa. Lakini hii kama mambo mengine hayakupunguzwa basi na hii fedha laki moja haitotosha. Kwa hiyo mimi nakuelezwa Dokta *ishallah* Mwenyezi Mungu atakurejesha tena kwenye jimbo lako hili liangalie na hii ndio tiketi yako ya kukurejesha jimboni kwa sababu asilimia kubwa wamo watu kule wafanyakazi, sasa hii hapa wewe ndio ya kuweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri alione sana suala hili ili aweze kuwasaidia wananchi wake katika jimbo pamoja na jumla Wazanzibari wote. Sina mantiki hiyo kwamba nampigia debe lakini haki yake dokta niiseme tu. Penye haki lazima tuzungumze.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kitengo *GSO*. Mhe. Mwenyekiti hii *GSO* watu wengi wanapiga kelele, lakini hiki kitengo ni kizuri sana. kumpekua mtu hakuna uharamu wowote. Kwa sababu kila mtu anakuwa na nafsi yake ndani ya nafsi ya roho. Kuna wengine anataka ile *department* ya wizara ile ende akafanye kazi kwa uadilifu na kwa vizuri kabisa. Lakini kuna wengine

wanakuwa nafsi yake haimo, lazima *GSO* ikuone bwana, lazima ikutafute *good history* yako ikoje. Binadamu ndio tulivyo hii tusiikatae *international* ipo jamani tusifikiri kwa Zanzibar tu.

Nakupeni mfano, tizameni Kiwanda cha Sukari kiko wapi sasa hivi, watu walikitia mitaimbo na ndio *GSO* wameikwepa pale. Nasema mimi amekwepa hakupitia bahati mbaya kaenda kutia mitaimbo.

Kwa kweli hiki kinastahiki sifa, tuwaongezee tu uadilifu, tuwape vitu vya kisayansi kama hawana, isiwe mtu anaangalia kwa macho tu, aangalie hasa na vitu vya *electronic* na ndio inavyotakiwa. Ni lazima tutanue kabisa, hakuna vyombo tuwape, ndio. Kwa hivyo, kitengo hiki Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akiendeleze vizuri asikiache ng'o ili kuwe na muwafaka mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nirudi tena. Mhe. Waziri nimejaribu kuangalia mote humo sasa kama suala hili ni pahala pake itakuwa fawahisha, kama si pahala pake basi nakuomba unijibu kwa vizuri.

Nimeangalia kwa haraka haraka humu na macho yangu leo sikuvaa miwani kuna hili suala la gari ya Afisi ya Waziri Kiongozi sijaliona na nitaendelea kulisema kwa nia nzuri Mhe. Waziri. Benzi ile imepitwa na wakati, benzi jana nimeona inavujisha na mafuta sasa hivi, *hydraulic* inatoka na mafuta jana shahidi wangu Mhe. Ame Mati Wadi tulikwenda tukayanusa pale, tukaikuta *diesel* bado inamwaga.

Mhe. Waziri huyu ni *chief* bwana, lazima tumpe heshima yake kubwa, gari apate ile inakwenda na wakati. Isijekuwa leo benzi ile inanoki njiani *Lailahailallah Muhammad Rasulullah*, Mwenyezi Mungu aepushie mbali, sijui waandishi wa habari watatusemaje. Itakuwa ni aibu, hata wewe unataka kuitafuta gari ya nyuma yake tena hiyo ndio vichekesho tena inaitwa *land cruiser* lile, hata ukibadilisha namba umuwekee kwa kweli itakuwa haistahiki sifa.

Humu nimeona gari nyingi umesema, sijui gari tatu sasa kifungu hiki na mimi ndio nikaona nikipatize hapa hapa. Nimeona ma-*cruiser* matatu umepata, lakini hiyo sikuiona. Kwa hiyo hili nalo naendelea kulisema Mhe. Waziri tumuenzi Mheshimiwa wetu naye, tumpe gari nzuri inayokwenda na wakati asaakun-kheir pengine huko mbele Mwenyezi Mungu muweza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache sitaki nikupunguzie. Lakini kuna jambo moja tumelisahau. Mhe. Rais katuwekea katika mji wetu jambo zuri sana tena kubwa. Bustani yetu ile ya Forodhani, imekuwa sasa hivi ni kivutio cha watalii.

Watu wanakuja hapa si kituo cha urojo bwana. Watu wanakuja pale wanapiga picha wanakwenda kuonesha nje huko anasema hii ni Zanzibar. Sasa hili ni moja ambalo katuwekea zawadi kubwa Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, ninao wakati kidogo. Siku moja tulikwenda Burundi na siku hiyo nashukuru nililala masikini nikaamka tajiri. Lakini kumbe Mhe. Rais alikuwa na azma kule Burundi kuwa akifika kwao Zanzibar akifanye kitu hicho, ndio kama nilivyosema nafsi ya mtu huwezi kuijua na ni kweli. Uwanja wa Burundi tuliposhuka pale hatukuamini kama tumeshuka katika uwanja wa ndege, tulisema ndani ya zulia kwa sababu ile ndege haikupata hata mtikisiko.

Leo Alhamdulillah uwanja huu hapa wa Zanzibar keshokutwa tunamaliza tutashuka vile vile. Ile azma ya Mhe. Rais Dr. Amani Abeid Karume kwa kuisimamia ilani yake ya Chama cha Mapinduzi ndio kaamua kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsane sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii ya kuzungumza na ninaomba kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulika na Masuala ya Fedha na Uchumi kutokana na hotuba yake nzuri ambayo aliifupisha na tumeielewa.

Vile vile naomba kumpongeza na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kutokana na uongozi wake wa muda wa miaka 10 ambayo ameongoza kwa awamu ya sita kwa busara na kufikia hatma nzuri. Sifa nyingi nimezisikia hapa toka asubuhi leo baada ya kuja bajeti hii akisiwa Mhe. Rais Dr. Karume. Basi nilitamani kuona angalau anapewa miaka miwili tu amalizie yale aliyoyaacha. Kutokana na sifa zile nafikiri ingestahiki apewe muda wa nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 9 utaona kuna suala la Kuimarisha Miundo ya Utumishi, kuanzisha sera ya muda wa kati ya ulipaji mishahara, kuanzisha mfumo mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu na mengineyo ukiendelea mbele pale. Sheria mpya ya utumishi wa umma na sera ya utumishi wa umma zimeshatayarishwa na zinategemea kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi mapema katika mwaka ujao wa fedha ili utekelezaji wake uanze.

Kwa keli hili mimi ningefurahi sana kama lingefanyika katika awamu ya sita na sio katika awamu ya saba. Ni suala muhimu sana na lilitaka lifanyiwe kazi mapema iwezekanavyo ili yale matatizo madogo madogo yanayojitokeza kwa

watumishi wa umma yakaondoka. Lakini *Inshaallah* tutarajie kwamba, awamu ya saba itakapokuja watayazingatia haya na kuyafanyia kazi.

Vile vile katika ukurasa wa 10 nimeona katika kifungu cha 17 kwamba, serikali imeipatia Afisi ya Baraza la Mapinduzi kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa afisi zake hapo Mazizini. Hapa mimi ningefurahi kama ujenzi huu kama ungelifanyika katika kipindi hiki cha awamu hii ya sita. Lakini kwa bahati mbaya kitafanyika katika awamu ya saba.

Hii ni ishara nzuri sana kuona kwamba upo umuhimu wa kuanzisha majengo mapya katika afisi zetu, badala ya kung'ang'ania zile afisi kongwe ambazo sasa hivi ni fingu na vile vile hazileti sura nzuri za kuonesha hali halisi ya nchi ambayo imejitawala.

Mfano mzuri ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejenga afisi yake katika maeneo ya kule na ningeomba kwamba wizara zote za serikali zikaiga mtindo ule wa kuwa na afisi ambayo inakwenda kwa mujibu wa wakati wa karne hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ukurawa sa 23, Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huu na wa 24, 25, 26, 27, 28, 29, 30, 31 imeelezea masuala ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa. Pameelezwa vizuri sana namna tunavyofanya kazi na wenzetu baina ya sisi na washiriki wetu katika ushirikiano wa kikanda ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama. Sisi tuko kama ni sehemu moja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania.

Katika maelezo haya hatukuona ni mahamiano gani tumefahamiana kwanza sisi kama Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu masuala mazima ya mazungumzo haya. Tumo katika *EC*, tumo katika *SADC*, tumo katika *Indian Ocean Ream*. Sasa mpaka dakika sasa mpaka dakika hii *SADC* ambayo jumuiya ya maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika imeanza kazi zake kwa muda mrefu si muda mfupi na hatujapata maelezo ya kiini hasa katika hotuba hii, kwamba kama Zanzibar tumefaidika nini katika masuala ya *SADC* kiuchumi au kiuhusiano wa kimataifa mpaka dakika hii, Zanzibar imefaidika nini. Au Zanzibar itafaidika nini *in future* kuwemo katika *SADC* kama si mmoja kwa Tanzania.

Vile vile katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki mpaka sasa hivi katika hotuba hii tumeshindwa kufahamu hasa yale malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na faida gani itapatikana katika *East Community* kama Zanzibar.

Sehemu moja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na vipi tutafaidika na *free trade area,* soko kuu la biashara. Vile vile hili hatujaliona, ile mikutano na mambo mengine. Wasi wasi wangu ni kwamba, sisi Zanzibar tunashiriki katika vikao hivi mimi nakumbuka nipo katika Jumuiya ya Wafanya Biashara nilishiriki vikao vingi vyote vya *East Community* na vya *SADC* ili kuona namna gani Zanzibar itafaidika katika masuala haya.

Zanzibar kama ni kisiwa utaona uchumi wake na mambo yake tofauti kidogo na nchi nyengine zilizomo katika *SADC* kama vile Mauritius na Madagascar. Sasa kama Zanzibar *what is our future* katika masuala haya ya mashirikiano na uhusiano wa kikanda kiuchumi? Hili ni suala muhimu sana la sisi kuweza kueleweshwa na kujua sio kupitisha juu juu tu kama tunapiga *brush* kwenye *cote* ya mwisho.

Jumuia ya Afrika Mashariki ikiwa ina manufaa na Zanzibar ni manufaa gani? Katika Mfuko wa Jumuia ya Afrika Mashariki naelewa kama iko miradi mingi ambayo imezungumzwa itasaidia, watu wameshapanga barabara za kutoka sehemu fulani kwenda fulani, reli kutoka nchi kadhaa kwenda nchi kadhaa, na haya ndiyo yaliyotia hamu hizi nchi za Rwanda na Burundi kutaka kujiunga na hii *East African Community*.

Lakini kujiunga Burundi na Rwanda kama Zanzibar, kama ni nchi katika nchi. Mimi nataka kujua, sisi kama Wazanzibari tuna mgao gani katika suala zima la Muungano wa Tanzania kwenye *East African Community* na kwenye *SADC*. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri atueleze ile miradi ya Zanzibar ambayo inapokelewa katika *East African Community* itafanyiwa kazi na hiyo ni moja katika *benefit* ambazo kuwa tutaona kwamba tumepata *benefit* gani katika suala la Zanzibar.

Suala la *free trade area* mimi nina wasi wasi mkubwa sana. Suala la *Uni Visa* vile vile hilo linanitia wasiwasi sana. Sisi Zanzibar kama kisiwa uchumi wetu unazingatia sana katika masuala ya utalii, biashara na tumezungukwa na bahari. Kwa hivyo, *alakullihali* tutakuwa tunahitajia pia yale mambo ya kibahari. Na ndio maana tukawa katika hii *Indian Ocean Ream* tunazo *benefits* nyingi sana. sasa lakini bahati mbaya *where going there is not Zanzibar*, tunakwenda kule *as Tanzania*. Sasa katika Tanzania tuna asilimia ngapi au tuna kitu gani cha kushika.

Hivi kuna *visa* wanakuja watalii Zanzibar lakini *visa* zao wanachukulia katika balozi wa Tanzania na nchi mbali mbali, wakifika Zanzibar hapa wanagongewa wanaondoka. Hapo sielewi mgawanyo wa hizi fedha, kama zinakuja Zanzibar au vipi. Lakini hilo sasa hivi tuko Tanzania, kama mfano tukishaingia katika

East African Community akitua mtu pale Nairobi akipigiwa muhuri akaambiwa sasa hivi tayari ni *Uni Visa* hiyo, akifika hapa Zanzibar anashuka anakwenda zake na sisi tutakuwa tunapata nini. Na mimi nitapokwenda nchi nyengine nitakuta *visa* katika nchi ile nalipia hapa katika ubalozi pesa itakwenda kule.

Kwa hivyo, *I don't know,* sisi kama tutakuwa tumefika kiasi gani au tutafaidika kiasi gani. Sasa mimi ningeona kwamba hayo pia ni ya kuzingatia, lakini kubwa zaidi sisi kama Zanzibar tumejitayarishaje kukabiliana na changamoto hizi? Na kitengo hiki ndio kiko kwa Mhe. Rais, sasa sisi tumejitayarisha vipi kiuchumi *whatever* kuona kwamba sisi tunakabiliana na hali hii na Zanzibar inafaidika kuingia katika *East African Community* inafaidika kuingia katika *SADC*.

Nilieleza hapa juzi kwamba *the only thing* kitu ambacho kinaweza kutusaidia sana ikawa sisi tutakuwa ni *the only in East Africa, in the only in SADC, free port area.* Lakini ukianza kusema kwamba tutakuwa katika *free trade area*, bidhaa zote zinazozalishwa kutoka Afrika ya Kusini mpaka Zambia zitakuwa zinakuja Zanzibar kuuzwa lakini sisi hatuna cha kuwauzia wao. Kwa hivyo, yale masuala ya kupunguza ushuru kidogo kidogo au wote, sisi hautatusaidia sana mpaka pale ambapo tutakuwa tumejitayarisha kuweza kuwa na *production* ya kutosha ya kuweza kuuza kwa wenzetu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nikitaka maelezo mafupi tu, wala si mengi, wala si makubwa, kuona *benefits, advantages* na *disadvantages* za sisi Zanzibar kujiunga moja kwa moja bila ya kupitia Tanzania na tuko katika Tanzania. Tuna finyangwa finyangwa vipi na tutafaidika vipi na masuala haya. Haya ni masuala muhimu sana na nafikiri kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar mwenyewe anayasimamia haya, basi yatakuwa na maelezo ya kina na tutapata mwisho wa bajeti hii.

Vile vile namuunga mkono kaka yangu Mhe. Haji Faki Shaali pale kwamba, tunahitajia kweli kuona ziara ya Mhe. Rais za nchi za nje. Hizi ni ziara muhimu sana. Sisi tunaamini kwamba Rais wetu anaposafiri kwenda nchi za nje anakwenda kutafuta manufaa makubwa ya nchi yetu. Kwa hali hiyo ipo haja ya kujua Mhe. Rais amekwenda katika nchi ngapi kwa mwaka na ameweza kuleta faida gani katika ziara zake. Hayo yatapata kutusaidia na kuweka *credit* zake ziwe katika uwazi na watu wote waweze kuzielewa. Hapo tena pongezi zitazidi kwa Mhe. Rais.

Baada ya kusema hayo naomba kuchukua fursa hii kumshukuru tena Mhe. Waziri kutokana na kazi yake nzuri aliyoifanya. Vile vile nampongeza Mhe. Rais kwa kuongoza kwa muda wa miaka kumi, tunamuombea kila la kheri *Inshaallah*. *Wabillahi Toufiq*.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kwa mchana huu wa leo wa mwisho ya kuchangia kidogo katika bajeti hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Nadhani kwanza nianze kumshukuru *Allah* kwa kutuweka hai tukawa wazima. Pia nimshukuru na nimpongeze Mhe. Rais kwa maneno machache, kwa sababu nitakalosema lolote sitamfikia Mhe. Ali Suleiman Ali. Kwa hivyo, mimi namshukuru kwa maneno machache kwa kuweza kuiongoza Zanzibar katika kipindi cha miaka kumi na sasa anamaliza kipindi chake kwa salama na kutupeleka pahali pazuri zaidi. Nawaomba wale ambao watafuatia ambao tayari wameshatangaza nia zao, kuwa na nia njema na Zanzibar na Wazanzibari, ili Mwenyezi Mungu atupe baraka zake na atuwezeshe kufikia katika kile kiwango cha wenzetu wanakofikia na kuweza kupata maendeleo halisi.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba mimi nichangie kidogo tu katika Idara ya Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu zilizotajwa na wenzangu, kwamba Tanzania au Zanzibar sasa hivi sio peke yake, inakwenda na Jumuia ya Afrika ya Mashariki, inakwenda na *SADC*, inakwenda na *African Union*, inabidi sasa tuangalie upya muda wa utekelezaji wa mipango yetu, ili ulingane na hali halisi zinaavyokwenda.

Kweli Mhe. Mwenyekiti, tuna mipango mingi na mizuri, lakini muda wetu wa kutekeleza mipango yetu unakuwa ni mrefu sana na kwa hivyo wenzetu wanatuacha nyuma. Sasa tukisema sisi tulipewa karibu miaka miwili sasa, sikumbuki vizuri lakini nafikiri ni miaka miwili sasa hivi toka tulipopewa ile semina ya ule Mradi wa Maendeleo ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma. Lakini katika kitabu hiki kama alivyosema mwenzangu hadi hivi leo tunamaliza mwaka huu wa 2010 hakuna jambo ambalo limefikiwa lililokuwa la msingi.

Kwa hivyo, tunasema ule muda wa utekelezaji wa haya mageuzi ukichukua muda mrefu zaidi kuliko hivi tunavyokwenda. Ina maana tutawekwa nyuma na hizo ajira ambazo sisi tunatengeneza zitaweza kuchukuliwa na wale ambao wanajitayarisha vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika jambo kubwa au kazi kubwa ambayo ingelikuwa imo katika dira ya Idara ya Utumishi ni uendelezaji wa nguvu kazi (*Main Power development*). Sasa tukiangalia hali inavyokwenda, hata hiki kitabu chetu ukiangalia kiambatanisho ‘D’ utaona kuna jedwali ya wale wanaosoma nje tu peke yake. Lakini ilikuwa jedwali hii itoke labda miaka kumi iliyopita. Bado Zanzibar haijawa na vyuo vyake wenyewe. Kwa wakati

huu tulioano, jedwali hii itakuwa haijakamilika kwa sababu lazima ilikuwa component ya vyuo vya Zanzibar iingie.

Kwa sababu vyuo vya Zanzibar sasa hivi vinatengeneza nguvu kazi. Kwa hivyo, tuitie humu ili tulinganishe hali tuliyokuwanayo huko nyuma ya kwamba vijana wetu wote walikuwa wakienda nje, lakini sasa tuna vyuo vyetu na sisi tuna-*train* vijana wetu wenyewe. Sasa mtu analinganisha mara moja kwamba, hawa ndio vijana wetu wanaosoma Zanzibar katika vyuo vikuu vyetu na hawa ndio wanaokwenda nje kwa sasa na ile asilimia itaonekana jinsi gani maendeleo yalivyokwenda.

Lakini vile vile la pili itasaidia kuweza kupanga nguvu kazi kwa wale watu wa Idara ya Utumishi. Kuona kwamba *out put* ya mwaka huu 2010 kutoka Tunguu, *SUZA*, Chukwani, Chwaka Chuo cha Maendeleo ya Fedha, tuna *out put* kwa hivyo sisi tunapanga hii. Kwa hivyo, tunaomba kwamba tuwe *broad* zaidi katika kufanya ile mipango yetu na kuona kwamba nguvu kazi inayotoka sasa hivi tunaipangia mipango kabisa. Kwa sababu kesi hizo zinazotajwa ni za ukweli kabisa kwamba vijana wanamaliza kusoma wanapanda boti na kuelekea mbele ya safari.

Huwezi kuzuia mkumbo huo kwa sababu nchi ndogo zinakwenda. Hata jana Mhe. Waziri mwenyewe aliyetoa *speech* ya leo alitwambia habari ya baadhi ya nchi. Lakini tukiweza kuwa-*maintain* kwa kiwango fulani tutajua ile *immigration* yao inavyokwenda. Lakini ikiwa *record* zetu hatuna vizuri hata ile *immigration* yao inavyokwenda haina. Kwa sababu hao wenzetu wanatoka lakini na wao wanajua taarifa zao kwamba tumepoteza madaktari wangapi, wataalamu wangapi, kwa hivyo wanazidisha hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi ndogo sana ukilinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara. Ni ndogo pia ukilinganisha na hata hiyo Burundi na Rwanda. Kwa sababu sisi tuna bahari iliyotuzunguka, kwa hivyo, tuna *limitation* katika baadhi ya mambo ambayo ilikuwa huko katika nchi za Bara inakuwa *limitation* zile zinakuwa hazipo. Sasa mimi ningeliona kwamba, tukaweka kipaumbele katika baadhiya fani. Ukitizama hii jedwali ya wanaosoma nchi za nje yote hukuti kijana anayeambiwa kafanya *engineering*. Hamna hii yote iliyoandikwa katika kiambatanisho ‘D’.

Chuo chetu cha *SUZA* hakijatoa fani ya *engineering*, cha Tunguu hakina fani hiyo, Chukwani hakina fani hiyo, tunaitegemea Mbweni baada ya muda kama tulivyoipitisha hapa kwamba itatoa lakini bado mahitaji ya ma-*engineers* (wahandisi) ni kubwa na ni muhimu sana. kwa hivyo, tungelielekea huko tukaanza kusomesha vijana katika fani ya uhandisi. Hata huo mwelekeo wa

kupeleka vijana nje katika fani ambazo zinapatikana ndani ya nchi tungeliuondoa lakini tukapeleka wale ambao fani zetu hazimo ndani ya nchi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tumezungukwa na bahari lakini katika fani hizi hukuti watu wanaosoma *Marine Science*. Kwa hivyo, hakuna mwelekeo wowote kuwa Zanzibar tutaelekea wapi katika fani hizi za bahari. Hakuna fani wanayoita *fisheries*, tunataka kwenda katika uvuvi wa Bahari Kuu lakini wataalamu wako wapi wa kuweza kwenda hivyo? Kwa hivyo, tubadilishe mwelekeo wa kupeleka wataalamu. Sasa idara hii ndio itakayoiongoza pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ikitizama *main power* inayotakiwa, ndio itakayoongoza katika kuona kwamba vijana wetu wanapelekwa kwa njia hizo.

Suala la pili Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo kuhusu viwango vya mishahara. Kama Idara ya Utumishi ilivyo, haidhuru Waziri wa Fedha yeye anajitetea, lakini yeye ni sehemu ya ile *system* yote ya upangaji mishahara. Idara ya Utumishi iwe na vigezo vya kupanga mishahara kwa watu woe wa ngazi ya chini na wataalamu, ulinganishe na maeneo mengine na hoja ya soko lilivyo. Lakini tukisema tunatoa tu mshahara huu huwezi

Mhe. Rashid Seif Suleiman: (anaendelea) lakini tukisema tu tunatoa mshahara huu, yaani mtu hata hawezi kujikimu kwa mshahara huo tatizo lipo.

Kwa hivyo, ninaomba sana idara hii pamoja na mageuzi yanayofanywa. Lakini Idara ya Utumishi kitu ambacho ni muhimu sana ni kupanga viwango vya mishahara. Kwa sababu kwanza vitatoa uwezo ya yule mtu kuweza kujikimu kwa ule mshahara unaompa. Pili katika fani za taaluma zitaweza kulingana angalau kwa kiwango fulani na sehemu nyengine ambazo wanapata *green pasture* za kwenda kujitafutia kazi nyengine.

Suala la mwisho kwa sababu ya muda wako Mhe. Mwenyekiti, nagusia kidogo kuhusu pencheni ya wastaafu. Kwa kweli juzi niliizungumza kidogo wakati nilipokuwa nikichangia Bajeti ya Serikali na leo naikumbushia tena, kwani ni sehemu ya utumishi.

Kwa kweli hawa wanaostaafu walikuwa watumishi jana na leo ndio wanastaafu. Kwa hivyo, wangestahiki kupangiwa pencheni yao kabla ya kustaafu na ile Idara ya Utumishi, kwa sababu ndiyo iliyowachukua na kuona wamefanya nini *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena tukimsikiliza sana Mhe. Waziri wa Fedha siku zote atasema hakuna fedha. Lakini yeye Mhe. Waziri wa Fedha sisi huwa

tunamtuma kwa ajili ya kutafuta fedha. Kwa hivyo, aje atuambie sisi amekosa na amepata wapi na sisi tunamwambia atafute *(Makofi)*.

Pendekezo langu Mhe. Mwenyekiti, kidogo nataka nitofautiane na kauli ya Mhe. Waziri Kivuli ingawa si katika kumpinga, isipokuwa ni kuiboresha kwamba yeye alisema wapewe shilingi 75,000/-. Lakini nasema sio shilingi 75,000/- au 20,000/- ama 25,000/- wala 75,000/-, jambo la msingi ni kuweka kiwango. Kwa sababu leo anaweza kuja huyu akakambia mpe shilingi 30,000/- na mwengine mpe 40,000/-, kwa hivyo hakuna.

Sasa ninachosema tuweke kiwango. Kwa mfano, kwa Zanzibar leo nimefanya hesabu kidogo hapa wakati nilipokuwa nikijitayarisha na kuchangia hotuba hii. Kwa kweli tunao uwezo wa kuwalipa wastaafu wetu mshahara wa chini wanalipwa wafanayakzi, yaani hivi sasa kwamba serikali ikitaka basi tunao uwezo huo.

Nadhani tujaribu na tuone Mwenyezi Mungu atatupa nini kwa sababu wale ni wazee na hata kwenye *Quraan* inasema uwashughulikie wazee hasa pale wapokuwa hawajiwezi. Kwa hivyo, nafikiri ni vyema tukarajibu kuwapa mshahara wa kima cha chini na tuangalie Mwenyezi Mungu atatuletea baraka gani *(Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa kuchunga muda. Sasa tunamaliza *session* ya asubuhi na tutakuja jioni na kuendelea na Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Mohammed Ali Salim, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Bihindi Hamad Khamis, tunakuombeni muwahi kwa ajili ya kupata mashirikiano kama nilivyoyapata hivi sasa *(Makofi)*.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo kwenye hotuba hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, iliyowasilishwa asubuhi na Mhe. Dk. Mwinyihaji.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Rais kwa kutekeleza ahadi yake ya kuwapelekea umeme watu wa Pemba kutoka Tanga. Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka Mhe. Rais aliwahi kusema kwamba asingependa kumaliza muda wake bila ya kuona kwamba watu wa Pemba wamepata umeme wa kudumu. Kwa vyovyote vile ahadi yake ile imekamilika. Nachukua nafasi hii kwa niaba ya watu wa Kiwani kumpongeza Rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi nyengine ambazo nataka nitowe ni kwa Mhe. Rais ni kuhusu suala zima la maridhiano ambayo kwa kweli hatua aliyofikia ni hatua ya ujasiri na ameonesha kwamba nia yake ni nzuri kwa maslahi na maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitowe nasaha kwa Wazanzibari wenzangu kwamba sasa wajipange na kumchagua Rais ajaye mbaye ataendeleza maridhiano haya, na yule ambaye ana nia ya kuyapinga basi huyu ana dalili ya kuwa hafai kuwa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza maswali na mimi kwa vile nilikuwa na haja ya kuuliza. Tuliambiwa kwamba miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ina mazingatio mazuri na kumekuwa na sekreterieti ambayo ina ratibu masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu la kwanza ningetaka Mhe. Waziri anifafanulie hiki Kiswahili cha mazingatio, kwamba miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imekuwa na mazingatio mazuri. Sasa hii ni lugha kidogo ya kificho, nataka kidogo anifafanulie. Mazingatio haya ni yepi, kwamba mazingatio yenyewe ni mafanikio au kwamba hayako hata katika ramani ya Afrika ya Mashariki?

Mhe. Mwenyekiti, sekreterieti hii ambayo imeundwa ningetaka nijuwe Zanzibar kama nchi imeshiriki vipi katika uundwaji wa sekreterieti hii ambayo hatimaye itazingatia miradi ya Zanzibar. Je, Zanzibar kama nchi, mchango wake ni upi kwenye kamati hii ambayo ndiyo hasa itakayopendekeza na kuamua miradi ya Afrika ya Mashariki kwa upande wa Zanzibar? Ni nani hasa alichagua au Zanzibar kama nchi tumeshiriki vipi?

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningependa nijuwe ni vipi kuhusu programu za miradi hii? Tumeambiwa iko miradi mitano, lakini Mhe. Haji amehoji kwamba muda wake ni upi ? Na mimi nataka nijuwe, programu au utekelezaji wake ni upi na ni mwaka gani miradi hii itaendeshwa na kwa mpangilio gani?

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika suala hili nataka nimuombe Mhe. Waziri pia atufahamishe kwa niaba ya Wazanzibari wote, Zanzibar tumejipanga vipi katika kukabiliana na changamoto katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa sababu tumeona nchi mbali mbali zimejipanga, zimeanzisha mipango mbali mbali wakijuwa kwamba Afrika Mashariki baadae itakuwa na soko moja, kwa hivyo kutakuwa na uhuru wa kutafuta ajira na uhuru wa kujipatia elimu. Zanzibar kama nchi yenye watu si zaidi ya milioni moja na nusu tumejipanga vipi na changamoto hizi za Afrika ya Mashariki, wakati wenzetu tayari wamejiandaa kwa mapambano ya soko huria.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningechangia kwa ufupi ni suala zima la Idara ya Mawasiliano ya Afisi ya Rais. Tumeona kwamba kumekuwa na programu mbili, programu ya kuandaa vipindi vya televisheni na uchapishwaji wa kalenda. Nipongeze kwamba programu zote mbili hizi zimetekelezwa na sasa malengo ya mwaka 2010/2011 ni kuandaa malengo matatu.

Malengo yote matatu Mhe. Mwenyekiti, ni malengo mazuri, lakini zuri zaidi ni kwamba ningemshauri Mhe. Waziri suala la mafunzo kazini kwa wafanyakazi lizidi kuendelezwa, kwa sababu bila mafunzo kazini itakuwa hatuwafanyii haki wafanyakazi wetu katika afisi hii na mbele ya serikali nzima kwa jumla. Kwa hivyo, programu ya mafunzo kazini ningeshauri kwamba iendelee kupewa kipaumbele na fedha hapa zitolewe kama zilivyopangwa, ili wafanyakazi wetu wazidi kujipatia mafunzo kazini.

Mhe. Mwenyekiti, ningefikiria kwamba sasa ni wakati tukawa na lengo la nne kwamba sasa tukapata kuwasiliana na Rais moja kwa moja. Kwa sababu hivi sasa kuna kamati au pengine kupitia kamati kwenye mawizara mbali mbali. Lakini Tanzania Bara wenzetu tumeona wananchi wanapata muda wa kuwasiliana na Rais moja kwa moja kwa njia ya redio au televisheni. Kwa hivyo, na Zanzibar ni wakati muafaka wa kuanzisha utaratibu huu kwa wananchi kuwapa fursa ya kuwasiliana na Rais kutoa maelezo yao au kero zao moja kwa moja, badala ya kupeleka kero kwa mtu mwengine halafu zikachujwa au zikabanwa. Kwa hivyo, tungewapa uhuru Wazanzibari kuwasiliana na Mhe. Rais ajeye uso kwa uso, ili tukapata fursa zaidi ya demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningeligusia ni Idara ya Huduma za Rais. Nipongeze kwamba kuna mpango mzuri ulioandaliwa. Lakini nashauri kuwa tujifunze basi. Mhe. Mwenyekiti, juzi tumesikia kuwa wenzetu kule SMT magari ya msafara wa Mhe. Rais yamekwama kutokana na uchafu wa mafuta. Sasa ikiwa Tanzania imetokezea hali hiyo, sasa Zanzibar ikitokezea hali hiyo itakuwa ni hatari kubwa. Kwa hivyo, tunahitaji sasa kuwa makini zaidi

kwamba huduma za Rais zipewe kipaumbele na ziweze kuwa za makini na zikaguliwe. Mhe. Mwenyekiti, magari ya viongozi wetu hawa basi yakaguliwe kila mara.

Kwa mfano Mhe. Mshimba tangu juzi amekuwa akilalamika kuwa gari la Mhe. Waziri Kiongozi linatoka mafuta na mambo mengine. Sasa kama hilo ni kweli basi ni vyema Mhe. Mwenyekiti, huduma za viongozi wetu hawa zikaangaliwa na zikapewa kipaumbele ili kuondosha aibu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Mhe. Waziri ametuambia kwamba wamebahatika kupata magari matatu *Toyota Land Cruiser* ningependa nijuwe magari hayo yako katika afisi gani, yametawanywa Unguja na Pemba. Kwa sababu Pemba kule tumekuwa na upungufu wa magari. Sasa magari matatu haya yako hapa Unguja Makao Makuu tu au yako na kule Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependa kuligusia ni maslahi ya wastaafu wetu pencheni. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba serikali imewapandishia kutoka Shs. 15,000/= hadi hiyo Shs. 25,000/=, wenzangu wamesema maslahi hayo ni madogo. Ni kweli kwamba ni vyema tukapandisha kima cha chini cha mshahara Zanzibar Shs.100,000/= wakapewa wastaafu wetu. Kwa sababu ukiangalia vitabu hivi kuna wastaafu wengi ambao wanasubiri kupumzika. Sasa nguvu kazi ile ambayo kuwa keshokutwa tunaipunzisha halafu kuwapa Shs. 25,000/= hatuwafanyii haki. Ni kweli Zanzibar ni changa na uchumi ni mdogo.

Lakini Mhe. Waziri tujibane, ili wenzetu hawa tuwape maslahi mazuri ili tuwafanyie haki. Lakini huku tukijiandaa kuwapa hiyo 25,000/= bado kuna malalamiko ya baadhi ya watendaji hasa mawasiliano bado wanapewa Shs.5,000/=. Mhe. Waziri, kuna malalamiko kwamba kuna watu wanapewa Shs.5,000/= hata hiyo Shs.15,000/= au Shs.25,000/= haijafikia. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri ukafanya utafiti wa kuwatafuta wastaafu wetu, kwa sababu bado kuna wengine wanasema kuwa kama lile posho la wazee Sebleni bado wanapewa Shs.5,000/=. Sasa nadhani tungewatafuta na tukaweza kuwapatia haki yao hiyo ili tuwe sambamba kwa Unguja na Pemba na Wazanzibari waweze kujisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba maslahi ya Shs.25,000/= kwa kweli hayatoshi, hivyo ningemshauri Mhe. Waziri tukajibana na tukapunguza matumizi mengine ambayo sio ya lazima ya serikali halafu tukawaongezea posho wazee hawa ili wakapata mshahara wa chini wa Shs. 100,000/= kama ndio pencheni yao kama ni wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na michango hiyo midogo kidogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aizingatie na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii kwa siku ya leo. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa, kwa sababu nategemea na wenzangu ambao bado hawajachangia wapate nafasi ya kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na hapo alipomalizia Mhe. Hija Hassan Hija, kwenye Idara ya Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi wa Idara ya Majenzi ambao wanalipwa kiinua mgongo Shs. 5,000/= kwa mwezi. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini wafanyakazi hawa walipwe kama wazee, wakati wafanyakazi hawa walikuwa wakifanyakazi serikalini katika Idara ya Majenzi?

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kazi waliyoifanya ni kubwa mno, mpaka kufikia hivi sasa watu wanalala majumbani mwao, kwa wakati ule kazi waliyoifanya na hivi sasa wanabakia kuranda na kulipwa kiinua mgongo cha Shs.5,000/=. Mhe. Mwenyekiti, ni lazima hawa watu waangaliwe na ionekane kwamba hawa ni watendaji ambao walifanyakazi kubwa mno mpaka kufikia hatua hii.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 40 na kifungu cha 65 kwenye Kitengo cha Usalama Serikalini, Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kidogo;

Kifungu cha 65

> “Katika kipindi hiki Idara ya Usalama Serikalini imetoa mafunzo ya salama kwa maafisi wa Idara ya Uhamiaji wa mikoa mitano ya Zanzibar. Aidha, wafanyakazi wa serikalini 464 walifanyiwa upekuzi”.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nataka nimuulize Mhe. Waziri, waliobainika na makosa ni wangapi kwenye hiyo idara katika hao watu 464 waliopekuliwa?

Mhe. Mwenyekiti, halafu nije katika ukurasa wa 34 kwenye kifungu cha 51, nacho vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu ili nipate kuuliza hilo swali?

Kifungu cha 51

> “Katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Idara ya Mipango na Sera imehamasisha wafanyakazi wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI

Zanzibar. Jumla ya wafanyakazi 153 walishiriki katika zoezi hilo wakiwemo wanawake 75 na wanaume 78".

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo ningeomba Mhe. Waziri atufafanulie kati ya wanawake hawa waliopima virusi hivyo ni wangapi ambao walibainika na wanaume ni wangapi? Sio lazima kuwataja ni fulani na fulani. Lakini tukijua Mhe. Mwenyekiti, kuwa ni watu watano au wanne, itakuwa tayari na wenzetu wataanza kujipanga kwamba hawa wenzetu hatuwajui ni nani, lakini wameshabainika kuwa wamo katika hili kundi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nakiomba hiki kitengo cha usalama kifanye kazi zake kwa vizuri, hususan kwenye kipindi hiki tunachoelekea cha uchaguzi wa kura za maoni pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kijitayarishe ili kisiweke ubaguzi wala kisiweke kwamba huyu nani na huyu nani? Nadhani Mhe. Mwenyekiti, utanielewa maneno yangu niliyozungumza ni matatu tu. Nadhani utayafahamu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi hii adhimu ya kusema mawili matatu katika hotuba hii ya bajeti. Naanza kwa kumshukuru *Allah* kwa sababu yeye ndiye anayestahiki kushukuriwa kwa kutupa uwezo wa kukaa hapa tukajadili mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuwashukuru viongozi wakuu, akiwemo Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Katibu Mkuu wa CUF, kwa kuandaa njia ya kufikia katika mustakabali mwema wa nchi. Kwa kweli tendo lao hilo ni tendo la kiungwana na ni la watu ambalo wanaojali maisha ya watu, basi lisingefaa kupita bure bila ya kushukuriwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, natoa shukurani zangu za dhati.

Pia naomba nimshukuru Mhe. Waziri aliyetuletea hotuba hii, kwa kweli kuna mambo mengi yaliyofanywa, na kwa sababu kuna mambo mengi yaliyofanywa pia tunastahiki kushukuru kwa yote yale yaliyofanywa, kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuhakikisha kuwa Mhe. Rais anaendelea vizuri na shughuli zake kama vile inavyostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, labda nikimalizia shukrani sasa nianze kuingia katika hii bajeti yenyewe, kwa sababu sitaki niseme mengi leo nitasema machache sana. Mhe. Mwenyekiti, jambo langu la kwanza nagusia tu kidogo suala zima la mageuzi ya utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, programu au mradi wowote ule unakuwa na ratiba maalum iliyopangwa, ratiba ya kuanzia tutaanza nini mwezi gani, tutafanya nini mwezi gani mpaka kufikia katika kukamilisha ratiba ile au grogramu ile. Ningemuomba Mhe. Wwziri basi, kwa sababu jambo hili limekuwa likizungumzwa muda mrefu.

Je, anaonaje basi akatuambia ile grogramu ya mageuzi haya ya utumishi wa umma yatakwendaje, yataanzia mwezi gani na yatamalizika mwezi gani? Nafikiri angetuambia hili lingekuwa jambo la busara sana, kwa sababu kila mmoja angeondoka hapa akijua kitu gani kitakachoendelea hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie katika kanuni za utumishi. Mhe. Mwenyekiti, katika mazoea yetu ya nyuma, ilikuwa kanuni za utumishi hazitumiki mpaka pale mtumishi anapofanya kosa anataka kuadhibiwa, hapo ndio hutumika kanuni za utumishi. Leo nina furaha kubwa kusikia kuwa wafanyakazi watasomeshwa kanuni za utumishi. Mhe. Mwenyekiti, ninaloomba katika hili wasije wakachaguliwa vifungu vya kusomeshwa, wakasomeshwa vile vifungu vya adhabu tu ambavyo wanaweza kupewa wao, wasomeshwe kanuni yote nzima, ili wajuwe haki zao, wajibu wao na wajuwe adhabu ambazo wanaweza wakapewa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba katika upandishaji wa mishahara inaonekana kuna kitu kipo katika serikali, yumkini inawezekana kuwa taarifa kamili za wafanyakazi wote wa serikali zinakosekana. Kwa sababu kama ingekuwa taarifa zote za wafanyakazi wa serikali zipo, basi inapopandishwa mishahara au yanapofanywa marekebisho ya mishahara, basi kusingekuwa na malalamiko mengi ambayo wafanyakazi wanalalamika, huwekewa na kipindi pia cha kila mtu kupeleka malalamiko yake.

Sasa hili linaonesha kuwa huu mpango unapofanywa inakuwa hakuna taarifa za kutosha, kwa sababu kama ziko taarifa za kutosha, basi itakuwa kuna watu wanapotosha ama wanafanya upendeleo au kuna jambo jengine ambalo halieleweki. Lakini kama hafanyi mtu upendeleo, kama taarifa zipo za kutosha na kama kuna *formula* maalum katika uongezaji wa mishahara hii basi kusingekuwa na tatizo hata moja.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba Mhe. Waziri kama taarifa zake haziko timilifu za wafanyakazi, basi afanye juhudi maalum ya kukamilisha taarifa za wafanyakazi ili mara nyengine litakapotokea lolote la kuhusu wafanyakazi, basi taarifa zao ziwe kamili na kusiwe na matatizo kama yalivyo matatizo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo labda kidogo nigusie habari ya uajiri. Mhe Mwenyekiti, nashukuru kuwa serikali imeruhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuajiri walimu, haidhuru mmoja, hawajatosha lakini pili, kuna wengine ambao wameshakaa muda mrefu tangu walipomaliza masomo yao hawajaajiriwa. Ninavyoelewa mimi unapokaa baada ya masomo ikawa masomo yale huyatumii, wala huyapitii basi yanatoka kidogo kidogo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunapowaweka muda mrefu hawa wahitimu bila ya kuwaajiri, tutarajie kwamba uwezo wao wa utendaji baadae ni lazima utapungua. Kwa sababu elimu yao imekaa haipandi, sana itakuwa inashuka kwa sababu atakuwa anayasahau yale ambayo amesomeshwa, kwa sababu hatuna utamaduni wa kujisomea wenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali katika hili basi ingekuwa na utaratibu maalum wa kujua kila mwaka na kila kada watamaliza wanafunzi wangapi vyuoni. Halafu wajuwe katika wanafunzi hawa ni wangapi tunataka tuwapeleke wapi na wangapi tunataka tuwapeleke wapi, ili wanapomaliza tu mtu anajijua kuwa mimi nakwenda pahala fulani basi. Hakuna tena nafasi ya kuwaachilia tena wazurure na kutafuta pahala wende, ingekuwa hakuna matatizo hayo.

Kwa hivyo, naishauri serikali ifanye mpango huo maalum. Ni mpango mzito, kwa sababu tuna wahitimu wengi sasa hivi wanaohitimu kila mwaka. Lakini kama itachukuliwa juhudi nzuri basi mimi naamini hilo litaweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili la uajiri, pia naomba nigusie kidogo suala zima la usimamizi katika kazi. Kwa kweli tuna matatizo katika usimamizi wa kazi na kwa sababu tuna matatizo ya usimamizi katika kazi, basi ufanisi wa kazi haupatikani. Sasa ikiwa ufanisi wa kazi haupatikani, ina maana tunatoa kingi kuliko tunachoingiza. Kwa hivyo, naomba suala la usimamizi lichukuliwe kwa mkazo unaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa matengenezo ya Ikulu na nyumba za serikali. Hapa naomba niseme kwamba pale katika Ikulu ya Mkoani. Kwanza Ikulu yenyewe inahitaji matengenezo, lakini pia jirani na Ikulu kuna nyumba moja ya zamani, nyumba ile kama itatengenezwa mbona ingefaa sana kwa wale wanaofuatana na Mhe. Rais wakakaa mule. Nadhani kuna haja nyumba ile kuishughulikia kabla haijaanza kuanguka kiambaza kimoja kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Mipango na Sera, moja katika majukumu yake ni kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha, Fungu nambari 10 Ikulu jadweli E. Nimeifungua jadweli E Mhe. Mwenyekiti, lakini nina wasi wasi kwamba

yale aliyoyasema *professor* Ali Denge yametoke kuwa compyuta imeruka. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba nijulishwe tu kuhusu hili Fungu nambari 10 lililowekwa hapa na kompyuta ikaruka je? Limerushwa kwa makusudi au limeruka kwa bahati mbaya. Ikiwa limerushwa kwa makusudi nitafahamu kuna nini, lakini ikiwa limeruka kwa bahati mbaya basi tuambiwe tulioko hapa.

Mhe. Mwenyekiti, labda nimalizie tu kwa kitu kidogo sana kuhusu hii habari ya GSO. GSO tunaambiwa kwamba miongoni mwa sehemu ilizopelekwa ni Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni na huko ilikwenda kuangalia nyaraka. Mhe. Mwenyekiti, hapa nina kitu kimoja ambacho nadhani umeshafika wakati sasa wa kubadilika. Umefika wakati wa kubadilika kuachana na nyaraka hizi za makaratasi kila wakati na tuwe na mfumo maalum wa kuweka nyaraka zeru ambazo huyo GSO akitaka kujua habari ya nyaraka hizi popote alipo basi atazijua, badala ya kuwa aende mpaka Mkokotoni kwanza kwenye Chuo cha Mafunzo ya Amali akaangalie nyaraka zilizoko. Mimi nafikiri tuna haja ya kubadilika. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia nisimsahau Mama Shadya na yeye nampongeza kwa juhudi zake anazozifanya kwa upande wa wanawake. Sababu ya kumpongeza hivyo ni kuwa juzi tu alifungua jengo la hospitali ya Micheweni ya kujifungulia mama wajawazito tukiwemo sisi wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Afisi Mdhamini Pemba katika Afisi ya Rais, kwa juhudi zake anazozifanya kwa Pemba nzima wanapokuja viongozi wa kitaifa, wa chama na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu kwa kweli hautokuwa mkubwa. Kwanza mchango wangu naomba nielekee kwenye jengo la *Rest House* Micheweni. Kwa kweli nikiangalia kwenye bajeti ya mwanzo ya serikali na mpaka hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sikuona kuitaja *Rest House* ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri nataka nijuwe sababu ya jengo lile tangu lilipoanza na jengo lenyewe ni dogo wala sio kuwa ikawa halijamaliza mpaka leo na Rais wa Zanzibar anamaliza muda wake, angalau wananchi wa Micheweni ilikuwa angalau Rais akija kutuaga na sisi tuwe pamoja kwenye jengo lile.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye Mkoa wangu wa Kaskazini na Kusini Pemba kwa kuyatengeneza majengo ya Ikulu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, majengo yale yanataka wafanyakazi na idadi ya wafanyakazi waliotajwa humu ya wafanyakazi wa kwenda kwenye mafunzo ni kidogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali waangalie, kwa sababu wafanyakazi wa Ikulu kuna vitengo mbali mbali, wanapokuja viongozi basi kila mtu awe ana hudumia upande wake.

Vile vile Mkoa wa Kaskazini Pemba Ikulu yake kwa kweli ni nzuri sana, naisifu serikali, waziri na Afisa Mdhamini Pemba kwa kufuatilia vizuri.

Mhe. Waziri mimi mchangio wangu si mkubwa lakini nije pale alipomalizia Mhe. Mwanajuma Mdachi yeye alisema kwamba kuna wazee wanalipwa mia tano, mimi ninavyokumbuka walianzia na shilingi hamsini huko tunakotoka kuanzia miaka ya nyuma nafikiri mwaka 1984 mpaka tumefikia mwaka 2000, namuomba Mhe. Waziri ile elfu tano wanayopata waengezewe kwa sababu ni kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti mimi sina mchango mkubwa nitamalizia hapo ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abass Juma Mhunzi: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwenye Wizara hii kwa sababu hata kwenye hotuba yake haikuwa kubwa, sio kwamba haikuwa kubwa kwa sababu haikuwa na kitu lakini ni hotuba mabyo ilikuwa imejaa hekma kubwa sana na mambo mazito na mimi niseme moja kwa moja ni hotuba ambayo naiunga mkono kwa asilimia hamsini kabla sijamaliza hotuba yagu.

Mhe. Mwenyekiti jambo la mwanzo ambalo ningependa sana kulizungumza linahusu *challenge* ambayo Mhe. Dk. Aman Abeid Karume amechukua kwa kushirikiana na Maalim Seif katibu Mkuu wa CUF, nasema hii ni *challenge* nzito sana kwa sababu viongozi kujitokeza na kuchukua *risk* mara nyengine huwa ni jambo lililo zito sana. Mhe. Mwenyekiti ungeweza kufikiria kwamba demokrasia inaweza ikawa ni muarubaini ya kila tatizo letu lakini sivyo hivyo, lazima kuwe na viongozi ambao wanaweza kuwa wabunifu wakachukua hatua za kufanya mambo ambayo hata wakiondoka watakumbukwa na mambo yale yatakuwa yanasaidia taifa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti suala hili la kukaa pamoja ilikuwa ni *challenge* kubwa na mimi nasema ni *challenge* kwa sababu wangetumia viongozi hawa mikondo ya demokrasia wakaenda katika vyama vyao sijui twende kwenye

Halmashauri halafu baraza kuu, halafu twende kwenye kamati hizo mimi nina hakika kwamba lingewekwa kwenye meza kama lisingekataliwa kabisa lingewekwa kwenye meza likaambiwa tutalijadili kwa mwaka unaokuja. Lakini waliweza kujitoa muhanga wakachukua *challenge* iliyo kubwa sana na hivi ndivyo wanasiasa wanavyotakiwa kufanya .

Mhe. Mwenyekiti tuna historia ya *challenge* kubwa sana ya marekebisho ya kiuchumi yaliyowahi kuchukuliwa na Mhe. Rais aliyeondoka Mhe. Rais Mwinyi nakumbuka wakati ule wa mwaka 1985/86 tulikuwa ndani ya Tanzania tuna mashaka makubwa ya kiuchumi, sembe la yanga ukisafiri kwenda Pemba jahazi siku saba hujaonekana, tulikuwa tunatafuta viazi vya kila mti kumbe mbatata ziko, wakati huo huwezi kupita ukaona watu wanakaanga chipsi. Kumbe viazi vinaliwa duniani tulifika pahala wanasiasa na watu tukafikiria kumbe ulimwengu ndio huu na hakuna jambo lolote la kulibadilisha ikawa kuna Wazanzibar wanaoweza kula vizuri japo kuwa hali yao ni ndogo, lakini ukila vizuri hakuna mtu aliyefikiria hivyo.

Mhe. Mwenyekiti pengine taimu yako kidogo niichukue lakini utafurahi sana mara moja tulitoka tukaenda Uingereza na Marehemu Mhe. Hamad Ali Fadau alikuwa ni mtu wa masihara sana na kwa kweli katika kipindi tulichokuwa nae katika baraza hapa ilikuwa ni kipindi kimoja kilichokuwa na *tension* kubwa lakini akismama Mhe. Hamad Ali Fadau tulikuwa tunacheka na tunafurahi, kwa sababu japokuwa mmeudhiana kiasi gani basi ule ukumbi aliweza kuurekebisha na kuweza kwenda vizuri Mwenyezi Mungu amrehemu alitoa mchango mkubwa wa kisiasa katika nchi hii.

Sasa katika safari ile tulipofika Uingereza wakaja vijana kutuchukua maana wameshasikia wamekuja Wazanzibar ndugu zetu wakaja na gari pale tukatoka tukenda zetu kutembea kila mmoja alikuwa kalala nikamuona ni Mhe. Fadau tu aliyekuwa macho nikamwambia Mhe. Fadau tutoke, tukaenda zetu karibu na anakoishi Malkia kwenye njiwa wengi, kule basi tukakaa ndio tunatoka shamba huko washamba wanaingia Uingereza sasa, tukaangalia Uingereza njiwa wanavyokwenda na majumba na magari yanavyokwenda. Mhe. Hamad Ali Fadau kama kawaida yake ni mtu wa masihara sana ananambia Mhe. Mhunzi unajua sisi wanasiasa tunaweza tukawa tunadanganya watu kweli kweli, nikamuuliza kwa nini Mheshimiwa, akanambia unajua mimi nilifikiri Dunia nzima tuko hivi hivi kumbe hii ndio Uingereza! Anasema leo nimeletwa na marehemu lakini nikirudi nataka kuja mwenyewe hayo ndio maneno aliyonambia Mhe. Hamad Ali Fadau ilikuwa ni joki lakini kulikuwa na ujumbe.

Tunaweza kufikiria maisha ndio haya haya kwa hivyo hakuna jambo wanasiasa tunaloweza kurekebisha tukawa tuna maisha mengine lakini iliwezekana katika

marekebisho ya uchumi, wakati ule baada ya mageuzi kutokea Zanzibar ikaonekana kwamba tunamuhitaji Mwinyi Tanzania.

Challenge ya pili ambayo ni kubwa sana ni hii ya maelewano Mhe. Mwenyekiti kwa Zanzibar demokrasia ilituletea mambo ya maana kabisa ya kwamba leo tuna pande mbili zinazoruhusiwa na wengine zaidi zingeweza kuja hapa vyama vingi ndani ya baraza, lakini jambo moja kwa *nature* ya nchi yetu ambalo lilibakia ni umoja ulio tepetepe ni umoja ambao hakuna nguvu utabakia umoja unaozungmzwa ndani ya sera zetu tu. Akizungumza CCM umoja , mshikamano na maridhiano na akizungumza CUF tuna umoja lakini ule umoja wa kweli wa kuitetea Zanzibar ulikuwa bado haujafika.

Mhe. Mwenyekiti nadhani mawazo ya viongozi hawa wawili ya kukaa pamoja hata kama wataondoka baadae katika siasa watakuwa wametuwekea jambo kubwa sana na kutufunga katika umoja sisi Wazanzibar, nilisema hilo kama ingekuwa zamani maana yake sasa hivi kuna utamaduni tuna katiba tunaiweka mbali tukasema tuna maelewano ya utamaduni, zamani tulikuwa na Rais akitoka kule hakuna uwezekano wa kutoka Rais wa Tanzania Zanzibar ulikuwa upo lakini sasa tulivyojifunga na ugombea mwenza huu, inawezekana tukaenda miaka arubaini mpaka mia mpaka wakaja wengine wakabadilisha katiba ikawa kumbe sasa Wazanzibar hawana haki ya kuwa tena Rais wa Tanzania na hili ni tatizo.

Kama ingelikuwa kama vile zamani mimi ningependekeza mageuzi haya ambayo ameyafanya Dk. Amani angestahiki kuwa Rais wa Tanzania, lakini kama angesimama kwa Rais wa Tanzania debe langu mimi ningelimpigia *Professor* Ibrahim Lipumba kwa sababu ndio mwenyekiti wangu, lakini nasema *chance* ingelikuwepo kwa sababu ni demokrasia ya kusimama kwa Rais wa Tanzzania, kwa sababu tunahitaji umoja Zanzibar. Lakini vilevile tunahitaji umoja wa Tanzania tunamkumbuka kwa jema jengine lipi Dk. Amani Abeid Karume? Mapinduzi haya ya kurekebisha na kuweka umeme Pemba kupitia Tanga ni jambo moja kubwa sana na tumelishangilia sana juzi pale uwanjani hili ni jambo la kujivunia na litabakia katika historia.

Sasa tuna matatizo ambayo Dk. Amani anaondoka matatizo ya kiuchumi ya mshahara mdogo, ya *over implement* ya kodi kubwa katika nchi ya uwezo mdogo wa Zanzibar kuweza kukusanya kodi ni tatizo ambalo anaondoka anatuachia, naamini Marais wengine wanaweza kuja katika mfumo kama huu wakaondoka wakatuachia, wenzangu wamekuwa wakilizungumza sana namna ambavyo maslahi ya wafanyakazi ni madogo, na mimi naungana nao mkono maslahi ya wafanyakazi ni madogo. Juzi nilisema kwamba Tanzania Bara ambao uchumi wake ulikuwa ukilega leg asana siku hizi umeimarika

wanatumia angalau asilimia kumi na nne ya CDP kwa maslahi ya wafanyakazi lakini hapa tunatumia asilimia tisa. Mhe. Mwenyekiti inawezekana tatizo kubwa lililopo hapa ikawa *over implement* katika serikali ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti mimi napendekeza tuanzishe mfuko wa ustaafishaji watu wako ambao wangepaswa kustaafu lakini kwa sababu ya mrititiko wa fedha ambazo zinakuwa hazipatikani mara nyengine serikalini watu wale ndio wamebakia wanaweza kukaa katika kazi japokuwa hawadhalilishi lakini tatizo linakuwa linaongezeka, niliacha tatizo hili Shirika la Meli kule kulikuwa na watu waliojitokeza kabisa mimi nataka kustaafu, na pale njia ya kustaafu ilikuwa ni jambo moja muhimu ili kuwaacha wafanyakazi walio kidogo na wakaweza kuliendesha lile Shirika kwa faida kubwa, halafu ikawa kuna mpango wa *sign of sign of* wanakaa nje anakuja mwaka mmoja melini halafu anarudi lakini mpango huo ulishindikana kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Nadhani basi kukiwa na *fund* ya aina hiyo basi tukapunguza hii *implement* naona hii *percentage* ya matumizi ya wafanyakazi wa GDP inaweza kuongezeka ingawa kuna mambo mengine ya kodi na unaweza kujiuliza, tuna maslahi yanayotafautiana baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kima cha chini na hata mishahara ya wafanyakazi kule inatofautiana, lakini kodi ya mapato asilimia ni ile ile imewekwa ya Muungano. Kama tungekuwa tunaweza kuichezea asilimia ya kodi ya mapato basi ingelikuwa mshahara ni mdogo lakini tukasema leo tunapunguza kidogo kwa maslahi ya wafanyakazi basi tupunguze hii kodi kidogo. Basi unaweza kufanya kwa mwaka mmoja ukajivuta kidogo ukangojea fedha zitakapokuwa nyingi ukaweza kupandisha kiwango chako, lakini sasa hizi ni matatizo ya *policy* hizi za *micro economy* ambayo hatuna uwezo nayo.

Kwa hivyo waheshimiwa hapa tuone kwamba *tools* zile za uchumi sio kuongeza mshahara na kupunguza tu lakini kuna mambo mengine ambayo yangestahiki tuwe na uwezo nayo tunayakosa, kwa hivyo kuna haja ya kuendelea kuimarisha muungano ambao tutakuwa na sauti kwamba hili litatusaidia wafanyakazi wetu na watu wetu lazima wenzetu watufahamu, namna hiyo hiyo ndio tunahitaji sasa sauti hasa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti hatuna muda mkubwa lakini sambamba na suala ambalo lilikuwa linazungumzia katika muundo wa serikali kwa sababu hapa naona ndio pahala pake, tumekuwa na Wizara ya Fedha na Mipango mimi nilikuwa nikisema sana hizi Wizara tunakokwenda baadae zigawiwe fedha na uhusiano wa kimataifa na tuwe na Wizara ya Mipango peke yake. Mhe. Mwenyekiti hii kuja kitabu kimoja ndio bajeti hicho hicho na mpango ndio hicho hicho kwa

sababu ya time tu kwa kweli tunakosa mambo mengi sana na Waziri atakayeleta vitabu vitatu lakini anasoma kimoja hawezi kuleta kitu ambacho kina maana, lakini tunahitaji wizara ambayo itaweza kupanga kweli.

Mhe. Mwenyekiti dua hiyo uendelee kuwa Spika, tungekuwa tuna Wizara ya Mipango peke yake mimi nadhani suala la serikali za mitaa na umuhimu wake leo ingekuwa limeshamalizika. Lakini ukimwachia Waziri wa Fedha na Mipango, hiyo huyo lolote atakalolizungumza la mipango anaangalia mfuko wake wa fedha kama fedha haziruhusu mpango hata kama ni mzuri atauwacha. Sasa ni afadhali aje Waziri wa Mipango aonyeshe mipango yake na Waziri wa Fedha nae ana majukumu yake, tunapaswa sasa Waziri wa Fedha na Uchumi awe anakwenda nje na kuwa na uwezo wa kukopa nadhani imo hiyo katika mapendekezo ya kero za Muungano, awe na nafasi ya kwenda nje kukopa na kuhusiana na kila mtu kuhusiana na masuala ya uchumi wetu hilo nilisema nilipendekeze sana Mhe. Mwenyekiti.

Lakini jengine hatuwezi kuwa na serikali ambayo atunataka umoja tukawa na Baraza la Wawakilishi ambalo ndio kielelezo cha demokrasia ikawa nacho kina matatizo matatizo, jana ilikuwa nichangie suala hili lakini naomba dakika tano, tuna Spika, wa Baraza la Wawakilishi mfumo wetu sisi Spika, hatoki miongoni mwa Wawakilishi. Tazania Bara Spika, ni Mbunge, Naibu Spika, ni Mbunge, kwetu sisi Spika, sio lazima kuwa muwakilishi lakini Naibu Spika, ni Mwakilishi. Hiki cheo cha Naibu Spika ni kikubwa mno na sisi katika Baraza bahati mbaya tumelidharau mpaka tumemdodesha mno, utakapokuwa na Naibu Spika anaingia katika kamati ya Baraza hapa ni Naibu Spika, mtu wa pili katika *administration* yetu. Lakini tunakwenda nae kwenye kamati Mhe. Hija ndio mwenyekiti na Naibu Spika ni mjumbe haionyeshi picha nzuri hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti huko tunakokwenda kama tunataka tuwe *consistent* basi ni afadhali Manaibu Spika, wote wawili wawe wanatoka wanakuja hapa kugombea na Wenyeviti huwa ni miongoni mwa wale wajumbe ambao wana kaa kwa hivyo ni vizuri kuwa ni Wawakilishi, hii itasaidia sana hadhi ya Mhe. Naibu Spika. Nasema hivyo serikali ifahamu kwa sababu hapo maslahi ya Naibu Spika, sasa yatakuwa yanaboreshwa angalau aweze kumkaribia Spika na kile cheo tukiheshimu kwa sababu sasa tunakwenda katika mfumo wa serikali ya pamoja, *inshaalla* iwe hivyo si vibaya kuona Spika anatoka upande mmoja na Naibu Spika anatoka upande mwengine. Mimi nasema hicho kitakuwa kielelezo kikubwa kwa sababu tukitaka kuendeleza umoja na pale pahala penye demokrasia watu wanapasikiliza pamekuwa kitu kimoja hilo linakuwa linasaidia sana katika mambo yetu.

Mhe. Mwenyekiti sitaki nichukue muda wako mwingi zaidi ya hapo isipokuwa ni kukushukuru tu na kwa kweli kuwashukuru sana viongozi wetu wakubwa waliofikiria na sisi wanasiasa tujitahidini sana tuwaunge mkono, tukizifanya kuwa ni juhudi za watu wawili tu na sisi tukasinzia basi tutarudi nyuma maguzo mia halafu ndio tuje tuanze tena wapi hatujui pa kuanzia. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafsi jioni hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pili nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake wote ambao waliandaa hotuba hii ambayo ni nzuri fupi lakini imekusanya vitengo vyote ambavyo vimekuwa ni muhimu.

Mhe. Mwenyekiti tatu niungane na wenzangu waliokwisha kuchangia kumpongeza Rais wetu Dk. Amani Abeid Karume kwa kazi kubwa na jitihada kubwa aliyofanya katika kutekeleza ilani yetu kwa kipindi hiki na kuweza kufikisha katika hatua kubwa sana, mambo mengi ambayo huko nyuma hayakutekelezeka kwa kipindi hiki nadhani kaondosha deni, miundo mbinu, maji hospitali kajitahidi katika kutekeleza hayo, tunaomba na hao watakaokuja wafuate nyayo zake.

Mhe. Mwenyekiti mimi nina *point* nne tu za kuzungumza na nitaomba kama nitarejea unistahamilie kwa sababu nina lengo na dhamira ya kuzungumza yale niliyokuwa nayo, nikiingia kwenye hotuba nije kwenye ukurasa wa kumi kifungu cha kumi na saba naomba ninukuu kidogo pamoja na cha kumi na nane halafu niseme yale niliyoyakusudia.Hotuba inasema:-

> " Mhe. Spika, naomba niliarifu Baraza lako tukufu kuwa serikali imeipatia Afisi ya Baraza la Mapinduzi kiwanda kwa ajili ya Afisi yake hapo Mazizini na ujenzi huo".
>
> Kumi na nane kinasema;
>
> "Tayari chuo cha Utawala wa Umma kimepatiwa kiwanja Tunguu na tayari mkandarasi kapatikana, nipongeze hatua hizi mbili lakini pia nipongeze na wenzetu wa Wizara mbali mbali ambao wamejitoa katika Mji Mkongwe na wamejenga sehemu ya Nje ya Mji Mkongwe".

Hii ni kuupa nafasi mji wetu kwa sababu unajulikana kimataifa sasa mji ukishajulikana kimataifa tuuwache na watu wake kuliko kuweka na maofisi kule kule.

Lakini yangu nije kwenye huu ujenzi wa hizi Afisi utakuta nyengine ziko Tunguu nyengine Mazizini na nyengine Mombasa, kimpangilio wa Ofisi haukukaa vizuri na huku nyuma serikali ilitenga eneo maalum sehemu ya Chuini kuanzia Melinane mpaka njia ya Mawimbini na nilisikia kwamba limetengwa eneo hilo kwa madhumuni hayo hayo ya ujenzi wa Maafisi na mambo mengine muhimu ya serikali. Sasa kila ikija bajeti hapa sikuti hata Wizara moja inayojengwa Chuini na watu kule wamzuiliwa wasijenge na nyumba zinaanguka lakini huu mwaka wa kumi na tano hatujasikia kauli ya serikali, kila afisi ikitoka Mji Mkongwe inakwenda Tunguu- Mazizini.

Sasa nimetumwa na wananchi wangu Mhe. Waziri wa Jimbo la Mfenesini wanaokaa Melinane na Chuini wapate kauli ya serikali je eneo hili limeondoshwa kwenye mpango huo, na kama limeondosha basi waruhusiwe mtu ajenge nyumba ya kudumu kwa sababu waliambiwa wasijenge nyumba za kudumu wabakie na nyumba zile zile za udongo na miti ili serikali inapotaka kuwaondoa iwaondoe kirahisi. Sasa muda umekuwa mkubwa lakini kauli ya serikali hatujaijua Afisi zinajengwa Tunguu, Mazizini na Mombasa lakini Chuini kumesahauliwa, sasa nadhani na hili muda utakuwa nao leo na kesho sasa jumaatatu ukija utakuja kutupa jibu ambalo wananchi wangu wanalingojea kwa hamu serikali ipo inasikia na wewe Mhe. Waziri pia unahisika na hayo wanaomba hili ambalo ni kero la muda mrefu tupate jawabu ambayo kidogo wananchi itawapa moyo.

Sasa nije ukurasa wa kumi na saba hapa naomba nitoe mchango wangu pamoja na kwamba wenzangu wengi wamepazungumza, kwanza nipongeze serikali kwa jitihada kubwa inayochukua kuwajali wananchi wake pamoja na wafanyakazi, hapa pamezungumzwa kwamba huko nyuma kima cha chini mshahara kilikuwa shilingi elfu thamanini, ukaja elfu tisini sasa uko kwenye laki moja. Jana Mhe. Ali Haji Ali alisema kwamba nchi nyingi zinazoendelea huenda kwa tafiti ili tafiti ikitoa habari fulani serikali inabidi ifuatilie na mimi nakumbuka juzi nilichangia kwenye Wizara iliyopita ile kwamba tafiti kwetu zinafanywa na leo nitatolea mfano kwa tafiti ya kaya.

Hivi sasa mshahara tunaambiwa umeongezwa kutoka tisini kwenda kwenye laki, lakini ukitizama kwenye tafiti zilizofanywa watu wengi wanaishi kwa mlo mmoja na ukimfanyia hisabu huyu mfanyakazi wa chini shilingi laki moja kwa siku moja anatumia shilingi elfu tatu na mia tano tuseme, sasa elfu tatu na mia tano kama mimi mfanyakazi wa kawaida nina familia mke na watoto watatu tu tunakuwa watu wanne lazima tule kilo mbili. Kilo mbili za mapembe shilingi elfu mbili , dagaa saadini watano shilingi elfu elfu tatu imeondoka mlo mmoja tu huo, chai asubuhi hajapata wala jioni ukiitaja kwa mwezi utaona kubwa lakini kwa siku ni ndogo sana.

Sasa ningeshauri serikali ikaangalia na hilo pia angalau tukamuongezea na mlo wa asubuhi tutoe elfu tatu tuweke elfu tano, apate elfu mbili kununua mikate ya boflo sukari na majani ya chai angalau watoto wanywe chai asubuhi na mchana na chakulalia ndio hicho hicho, sasa nashauri serikali pamoja na laki hatukuikataa lakini ukiipitia hisabu bado mtu anapata mlo mmoja, kwa hivyo naomba iongezwe elfu tano kwa siku ili mshahara wa chini uanze laki moja na nusu mtu apate mlo wa asubuhi na mchana, tafiti za kaya zipo na ukenda kaskazini Pemba na Unguja wako chini zaidi. Sasa naomba seikali itizame kwa jicho la huruma ili tuweze na wafanyakazi wetu nao waipende nchi yao, wapende kazi yao na wajipende wao wenyewe hapo hujatia sabuni, hujatia dawa mtoto akiumwa na hujatia chochote kile chengine huo ni mlo tu, sasa naomba na hilo wataalam wapo serikalini wakae waweze angalau kuwanyanyua wafanyakazi wetu hawa wa ngazi za chini.

Lakini pia tunakuja kwa wenzetu ambao tayari wamestaafu muda mrefu walikuwa wanalipwa elfu saba na mia tano ikapandishwa ikaja elfu kumi na tano, lakini pia sasa hivi elfu kumi na tano kwa mwezi huo mlo mmoja hautimii tumepata habari kwamba zimeongezwa na zimekuwa elfu ishirini na tano lakini naomba tusogeze angalau sabiini na tano, huyu nae tumjali kwamba ameshatumikia nchi yetu kwa muda mrefu mpaka kazeeka mikononi mwa serikali sasa lazima nae tumjali ili maisha yake yende pazuri. Yapo mambo kusema ni aibu lakini katika mifano ni lazima kusema. Hivi sasa ukienda mtu kafa utasikia wanasema mwenye deni aje kwa wafiwa, sasa watu wengi wanakufa na madeni na watu wanaridhi sio jambo zuri tunataka tukienda mazikoni iwe kimya tunazika tunaondoka, lakini siku hizi imekuwa mwenye deni aje kwa wafiwa inaonekana kweli watu wengi wana madeni na wanakufa nayo sasa sio jambo zuri kulizunguza kibinaadam sisi waislam.

Sasa naomba na hilo pia serikali waliangalie pencheni ni ndogo mno tunaomba na hilo liongezwe kutoka ishirini na tano iende mpaka sabiini na tano ili angalau tukienda kuzika tusisikie mwenye madeni atoke ajieleze angalau ipungue, sasa nadhani na hii itasaidia kuwapa moyo wale ambao wameitumikia nchi yao kwa kipindi kirafu.

Nikiendelea kwenye mchango wangu nije ukurasa wa kumi na nane kifungu cha thalathini kinazungumzia kwamba kuna vijana wahitimu mia saba na hamsini na saba ambao wamerudi katika masomo na wameajiriwa, lakini ninavyoona mimi bado ajira imekuwa ndogo sana serikalini kwa sababu ukenda walimu tu waliomaliza kusoma tokea 2007 wapo 2000 na kwenda mbele lakini unaambiwa hapa wameajiriwa mia tano tu. Bado elfu moja na nab ado wengine wako vyuoni hiyo ni taasisi moja tu na taasisi zipo nyingi.

Sasa naomba na hili pia serikali ingeliliangalia tukaweza kwamba wale inaowasomesha wakirudi wasikae wakafanya kutu, kwa sababu kisu unaweza kukinunua kipya lakini ukikitia mvunguni kitafanya kutu na ukiwa na kikukuu ukitumia kisifanye kutu, sasa naomba tusiwaweke wataalam mpaka kile walichokisoma wakaanza kukisahau kwa wababu taaluma kila ukiiwachia nayo inakuachia. Maalim Moh'd Ali Salim yupo hapo sasa naomba walimu nao watizamwe, tunashukuru kwamba wameajiriwa katika ile Mikoa yenye matatizo Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba lakini hata Mkoa wetu wa Mjini una skuli nyingi zina upungufu wa walimu.

Kwa hivyo na hili pia litizamwe hapa mjini watu wanasumbuka sana darasa moja watoto mia au sabiini lakini walimu wapo, madarasa yapo sasa naiomba serikali na hili ilitizame ili kusaidia ajira kwa vijana wetu ambao tayari wameshasoma na wanakuwa na hamu ya kuifanyia kazi nchi yao. Lakini la kuongeza pia kuna kilio cha muda mrefu katika mfuko wetu huu wa ZSSF utakuta taasisi nyingi zinakata mfuko huu katika mishahara lakini hazifiki kunakohusika na mtu akimaliza muda akenda kule anakuta kuna mapungufu mwezi wa sita hazikwenda mwenzi wa nane hazikwenda, sasa naomba na hili lifanyiwe kazi ili mtu akikatwa pesa zake ziende kunakohusika.

Lakini chengine cha muda mrefu ambacho nacho wanakililia hivi sasa ajira za watu binafsi wengi sana hawatimizi miaka ya kustaafu kama serikalini, unajaza mkataba miaka miwili unaambiwa umeiba kijiko unafukuzwa unakwenda taasisi nyengine, unaambiwa umevunja gilasi unafukuzwa bado hujatimiza miaka ya kustaafu na chako kiko kule ukifika unaambiwa hapa mpaka ufike miaka sitini, sasa utakuta wafanyakazi wanahangaika sana hawa wanaoajiriwa na taasisi binafsi. Sasa naomba na hawa kama kufuata sheria serikali ni ngumu wafanyiwe sheria zao yule mtu kamaliza mkataba miaka miwili apewe chake asogee mbele, kamaliza miaka mitatu apewe chake asogee mbele, utaratibu atajipangia mwenyewe lakini sasa hivi usumbufu ni mkubwa watu kazi wanafanya mtu miaka mitatu ameshapita taasisi nne, huku kafukuzwa huku kaachishwa.

Sasa naiomba serikali na hili ikaliangalia ili wenzetu hawa wanapomaliza wapate haki zao kwa wakati na waweze kuzitumia.

Point yangu ya mwisho Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 30 hapa naomba nitoe mawazo yangu. Hapa tunaambiwa Shirikisho la Afrika ya Mashariki hivi sasa tayari tumo ndani ya mchakato huo wa kuweza kuweka shirikishi hili kwa nchi zetu hizi ambazo tumeungana. Tunasikia kwamba vikao vingi vimeshakaa katika kutekeleza suala hili.

Mhe. Mwenyekiti hivi karibuni tulipata taarifa katika kufatilia tuliambiwa ni kweli wapo watu wanashiriki kutoka hapa Zanzibar kwenye katika vikao hivi muhimu. Cha ajabu kwamba kama kikao kipo tarehe 6/6/ yeye barua anapewa tarehe 10/6 kikao kishapita siku nne nyuma. Nilitaka kujua kwamba haya ni ya kweli ni habari za magazeti tu. Na kama ni hivyo sisi tupo katika nafasi gani katika masuala haya. Kwa sababu hili shirikishi linakwenda kwa hatua, kwanza tutaanza bandari huru, tutakuja biashara huru, tutakuja sarafu moja na tutakwenda mbele.

Je, na sisi tunatoa mchango wetu kikamilifu? Kama tunatoa nataka tuelezwe kama tunatoa na tumefikia hatua fulani, nadhani wananchi watafaidika na mchakato huu, kuliko kubaki kuwa wataalamu ndani ya madaftari. Lakini tukianza kujua kidogo kidogo siku ikikamilika inakuwa hatuna wa kumuuliza kwa sababau suala tumeshalifahamu. Naomba kama kuna maelezo ya msingi basi Mhe. Waziri wakati wa kutoa majumuisho tueleze na sisi tumeshiriki 1,2,3 na tuko nafasi hii. Hili tumelikubali na hili tumelikataa kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo mfupi niwape nafasi wenzangu. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini tunaikubali hotuba hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi kuzungumza machache kuhusiana na mjadala huu wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, hili kwa sababu sijazoea kwa hivyo naomba niliseme mwanzo nisije nikasahau. Naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. (*Vicheko*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hilo na mimi niungane na Waheshimiwa kuwapongeza viongozi wetu wakuu wawili Dokta Karume na Rais wa Zanzibar na Mhe. Maalim Seif Sharif katika nia yao njema ya kuwaletea wananchi wa Zanzibar umoja na mshikamano ambao nadhani ukinawiri vizuri huenda ikawa ndio suluhisho ya matatizo yetu mengi yakiwemo ya kisiasa na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, tunao wajibu wa kuwapongeza viongozi hawa kwa sababu jamii ya Wazanzibar ni watu wachache, mara nyingi huko duniani tunajulikana kama ni watu wa familia moja, lakini tulifika pabaya, haifai hata kutoa historia ya yale yaliyopita. Waliopita walijaribu kutafuta ufumbuzi lakini hawakufanikiwa vizuri. Nataka niseme Dokta Karume pamoja na Maalim hata kama bado tumo katika maazimio lakini mafanikio tayari yameshaonekana.

Kwa sababu miaka ya nyuma tukikaribia uchaguzi kama hivi basi kwa wakati huu tulionao tupo karibu bado miezi mine au mitano ilikuwa tayari bakora zikicheza hapa, matusi yakicheza, uhasama ulikuwa ukiendelea. Lakini mwaka huu shwari utafikiri hakuna uchaguzi, sasa haya ni mafanikio makubwa. Tuna wajibu wa kuwapongeza na mimi huwa naomba dua sana kwa Mwenyezi Mungu ayajaaliye haya maazimio tuliyonayo ya kufika huko tunakokwenda basi yawe kama matarajio ya wapenda amani yalivyo katika nafsi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri na ndivyo ilivyo Mhe. Rais Karume atakuwa ameweka historia kubwa katika nchi hii. Nilitaka niwaombe waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wenzangu basi tuungane na Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na Maalim Seif katika kuweka kumbukumbu kwamba ni Rais wa Zanzibar Dokta Karume na Katibu Mkuu wa CUF maalim Seif Sharif pamoja na Wawakilishi wa Baraza la saba ambao walifanikisha kuitisha umoja wa Wazanzibar. Hivyo itakuwa ni histori itakuja kutukumbuka siku za mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze baada ya utangulizi huo nianze ukurasa wa 32, pale kuna Afisi ya Uratib wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa. Moja katika majukumu yake Afisi hii na wenyewe wameyaeleza hapa ni kuendelea na juhudi za serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuimarisha uhusiano mwema na nchi marafiki na taasisi za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, maumbile ya Afisi hii ni uratibu wa uchumi na katika kufanya uhusiana wa Kimataifa basi mara nyengine malengo yetu huwa ni malengo ya kiuchumi zaidi. Sisi Wazanzibari tuna kilio cha miaka mingi cha OIC. Nafikiri Mjumbe mmoja jana alitaja hili suala. Kazi ya Afisi hii ni kutafuta uhisiano wa tasisi za Kimataifa, sisi ni muda mrefu tumenyimwa fursa hii ya kujiunga na OIC. Bila shaka pamoja na yote ya kutafuta uhusino mwema lakini malengo yetu zaidi ilikuwa ni uchumi. Nataka nimuulize Mhe. Waziri katika kuratibu huu uhusiano wa Kimataifa hivi hii Afisi yake haijakaa ikalizingatia kwamba kuna haja ya kufanya juhudi za makusudi ili Zanzibar iweze kujiunga moja kwa moja na hili Shirika la OIC.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoeleza wenzetu wamefaidika sana na Shirika hili na sisi bila shaka tungekuwa tumepiga hatua kubwa sana tokea miaka ile tuliyotaka kujiunga tukazuiliwa. Nilikuwa nahisi Afisi hii ingekuwa na juhudi ya makusudi ya kuhakikisha kwamba hili jambo linapatiwa uwezekano wa kujiunga ili tuendelea kufaidika kama wenzetu wanavyofaidika. Tunamapungufu mengi katika nchi yetu, tunaukosefu wa fedha, tuna mambo mengi ya kimaendeleo yanatushinda, tukiweza kujiunga hapa mimi nafikiri tutakuwa tumepiga hatua kidogo. Nilikuwa nashauri hivyo.

Niende kwenye Idara ya huduma za Rais. Hapa nataka nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii. Kwa kweli amefanya juhudi kubwa kwa sababu majengo ikiwemo Ikulu ya Mnazi Mmoja pamoja na nyumba za serikali katika maeneo tofauti zilikuwa katika hali mbaya sana. Lakini kwa juhudi za serikali kupitia katibu mkuu wake ameweza kufanya mambo mengi. Kwanza Ikulu ya Mnazi Mmoja sasa hivi iko katika hali nzuri sana, nyumba za serikali Chekechake, Wete, Mkokotoni, Dar-es-Salaam kwa kweli zimefanyiwa kazi vizuri na sasa hivi zipo katika hali nzuri sana. Hilo ni jambo la kumpongeza sana.

Sasa hivi ana maazimio ya kutengeneza nyumba ya Bwefumu na mimi naomba sana kwa sababu ile nyumba bado hali yake ni mbaya na ana malengo ya kutengeneza nyumba ya Dodoma naamini hakutaja lakini pia ana malengo ya kupaendeleza pale kwenye ile nyumba ya Migombani kwa sababu keshanunua kiwanja kikubwa. Nafikiri tumeombee duwa Mwenyezi Mungu ampe taukiq na hisi nyumba nazo ziwe katika hali nzuri.

Isipokuwa nimetishika kidogo na hii Bajeti ya Maendeleo ya hii Wizara, sijui kama itamuwezesha Katibu Mkuu kufanya mambo haya. Kwa sababu ni milioni 1.5. mambo aliyonayo ni mengi, nyumba ya Bwefumu, kuna nyumba ya Dodoma. Kule Dodoma tulikuwa tu na mpango wa kutafuta kiwanja chengine sijui Mhe. Waziri kama kile kiwanja kimepatikana au hii nyumba itajengwa pale pale ilipo sasa hivi. Lakini pale mazingira yake si mazuri ni machafu.

Pamoja na hayo pia kunamaazimia ya kuanza ujenzi wa Afisa Mdhamini kule Pemba. Kwa kweli nyumba yake hairidhishi afisi ile ni ya kizamani tokea enzi za Nabii Daudi ni ya kizamani sana, hailingani hata kidogo na mazingira ya sasa hivi, tumesema sana, tumeshauri sana. Sasa naona azma ya kujengwa ipo lakini kilichotajwa humu ni kidogo sana. Kwenye ukurasa wa 44 wamesema kuanza matayarisho kwa ajili ya ujenzi wa Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Sasa matayarisho yenyewe yatujui ni yepi ni ya kufyeka kiwanja au ni angalau ya kufika *foundation* au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, walituonesha kiwanja Tibirinzi lakini kule kuna nyumba ya serikali ya Ikulu. Tulishauri kwamba ni vizuri Afisi ya Afisa Mdhamini ibakie pale ilipo hivi sasa. Tunaomba Mhe. Waziri akija atufafanulie ni wapi atajenga kwa sababu kule tulisema kule ni afisi ya wakubwa zaidi na hii ni afisi ya utendaji tulitaka ikae pale pale ilipo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi sana ya kusema isipokuwa kuna maelezo ya Mhe. Waziri yamenifurahisha sana katika hitimisho yake nilitaka niyanukuu kidogo, ili kutoa zingatio maalum.

“Anasema hata hivyo tuelewe kuwa hatuwezi kupata maisha mapya ya kisasa ikiwa baadhi yetu tutakuwa bado tunang’ang’ania tabia, hulka na mienendo ya kizamani. Nawasihi viongozi na wananchi wenzangu kukubali mabadiliko yanayotokea wahenga wamesema “Penye nia pana njia”

Mhe. Mwenyekiti, haya ni maneno ya hekma. Nilisema niyataje tena hapa ili tuyaweke kwenye vichwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inaelekea kwenye mageuzi makubwa ya kimfumo wa utawala na hata uhusiano wetu wa kijamii. Sasa si vyema hata kidogo tubeza fursa hii tuliyoipata. Inasikitisha na kwa kweli inasikitisha sana kusikia kuna baadhi yetu wanathubutu hata kuandika maandishi yanayoashiria kutokukubaliana na huu umoja ambao wengi wetu tunalenga kuuanzisha. Inasikitisha pia kusikia kuna underground movement.

Mhe. Mwenyekiti, siku hizi kuna mtindo wa kupelekeana maseg unaweza ukatumia maseg kwenye simu yako, tena huyo anayetuma hizo maseg sijua anakuwa anakujua kuwa wewe ni nani au anabuni namba tu halafu anasukuma maseg yake. Ikija kura ya maoni sema hapana. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hivyo mambo kama haya kwa kweli, hapa tulipofika takriban ulimwengu mzima unaiangalia Zanzibar kama kwamba inajinasua katika matatizo waliyonayo. Sidhani kama tutaeleweka kuiachia fursa hii au kufanya mambo ya kudhoofisha hizi juhudi zinazoendelea sasa hivi. Wenzetu watatushangaa kweli kweli. Kwa hivyo mimi naomba kuwanasihi sana Wazanzibari wanzangu fursa hii tuing’ang’anie kwa magego na haifai kuibeza.

Mhe. Mwenyekiti, niungane sana na Mhe. Haji Faki Shaali, mnadhimu wangu. Yeye alisema Mungu amjaaliye mtu anayeomba uongozi wa Rais katika nchi hii ikiwa hana niya ya kuendeleza mazungumzo haya Mungu amjaaliye asipate. Mimi naomba nende mbali zaidi na hata kama kuna mwakilishi aliyekuwa hana nia ya kuendelea na mazungumzo haya na mustakbali huu Mungu amjaaliye asipate Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikapata nafasi ya kuchangia mawili matatu juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kutujaalia jioni hii ya leo kuwepo katika Baraza hili tukufu kwa madhumuni haya tunaendelea nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi vyema na kwa vitendo na *Alhamdulillah* tunashukuru mabadiliko makubwa ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, maendeleo makubwa yameweza kupatikana katika kipindi hichi cha miaka 10 ya uongozi wake. Hili kwa kweli halina ubishi wowote. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri Dokta Mwinyi ambaye anamsimamia Mhe. Rais katika Wizara hii, kwa juhudi zake mbali mbali anazozichukua katika kusimamia Wizara hii.

Pia nichukue nafasi hii kumshukuru kwa hotuba yake nzuri, fupi lakini imejaza mambo ambayo yanaonesha mafanikio makubwa katika Wizara hii. Mimi kama ilivyo hotuba yenyewe nitazungumzia maeneo matatu peke yake kwa ufupi kabisa.

Kwanza nitazungumzia juu ya Idara ya huduma za Rais hususan katika maeneo haya ya kufanya marekebisho, kufanya matengenezo katika nyumba za Serikali. Kwanza niwapongeze sana kwanza Mkurugenzi pamoja na wote ambao wanasimamia matengenezo haya au wanaosimamia nyumba hizi ambazo kwa kweli ni nyumba muhimu za viongozi wetu ambazo zinastahiki kuenziwa na zionekane kweli ni nyumba za viongozi katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, moja ambalo ningependa sana kulizungumzia juu ya nyumba ile ya Dar-es-Salaam Laibon. Mimi na Kamati yangu mara nyingi tumekuwa tukifanyia vikao pale tunapokuwa kwenye Kamati pale Dar-es-Salaam. Na kwa kweli huwa tunakuwa na masononeko makubwa juu ya hadhi ya nchi yetu lakini na lile jengo lenyewe jinsi lilivyo limefanyiwa matengenezo na wizara inajitahidi kulifanyia matengeneo lakini kwa kweli halilingani na hadhi ya Zanzibar kama ilivyo.

Kama tunavyojua kwamba Muungano huu ni kati ya Tanganyika na Zanzibar kwa hivyo tungepaswa kuwa na jengo linalolingana na nchi yetu Zanzibar ambayo itakuwa ni *center* kwa watu wa Zanzibar tena liwe jengo lisilopungua ghorofa tano au sita lenye kujumuisha katika mambo mbali mbali yakiwemo ya kibiashara na mambo mengine. Lakini leo kwa kweli inasikitisha Mhe. Waziri kwamba kijijumba kile, sijui tumekodi au vipi ndio kipo pale kama kielelezo cha Zanzibar. Kwa kweli hili jambo linatusononesha sana.

Mhe. Dokta Mwinyi, tukuombe kwa makusudi kama ikiwezekana katika eneo lile ni zuri kama wenzetu watakubali basi tujenge jengo linalolingana na hadhi

ya nchi yetu na kwa kweli pale pamekuwa hapatoshi. Kwa sababu hata kufanya mikutano mikubwa ya Kimataifa, sijui mnapokutana na mabalozi au wafadhili mnakubania wapi. Sisi tunakuwa na masononeko makubwa juu ya jengo lile na kutokana na hadhi ya nchi yetu. Kwa hivyo kwa makusudi tukae tujipange pamoja na hali ngumu ya uchumi lakini mimi naamini tukikusudia kufanya inawezekana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii umetueleza juu ya nyumba ambazo zinatakiwa kujengwa. Kitabu kinaeleza kuwa zitajengwa nyumba mpya Dar-es-Salaam na Dodoma. Sasa sijui ndiyo hiyo nyumba ninayoizungumza ya Dar-es-Salaam au nyengine sijui. Lakini nikiangalia hiyo kasma yenyewe ya fedha zilizowekwa bilioni moja na nusu sijui kama ndio zitakidhi haja ya hilo jengo ambalo tunalihitaji. Pengine tunaweza kujenga kijijumba cha chini vile vile cha ghorofa moja. Kama bajeti Mhe. Waziri ndio hii ya ujenzi huo unaokusudiwa basi hizi ni pesa za kiwanja tu peke yake, hazitoshi kabisa kabisa. La kama kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuweka hii *ivestment* basi utakuja kutueleza wakati utakapokuja.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo nimekusudia kulizungumza ni katika Idara ya Utumishi wa Serikali. Wenzangu wengi wamelizungumzia hili na unapoona wajumbe wako kila mjumbe anaposimama pale analizungumzia jambo hilo basi tujue lina umuhimu wa aina yake. Tusingependa jambo hilo likabezwa au likadharauliwa au likaonekana ah! ndio kazi yao kusema ni lazima suala kama hilo serikali ilichukulie uzito unaostahiki.

Suala la watumishi kila wakati tumekuwa tukisikia taarifa juu ya muundo wa utumishi umeshakamilika. Kama hapa mmetueleza miundo mipya ya mishahara imeshatayarishwa ambayo imezingatia miundo ya utumishi ya kada mbali mbali zilizomo katika utumishi wa serikali. Haya yamekuwa ni maelezo ya kila siku, mwaka jana mmetueleza hivyo hivyo na mwaka huu ndio mnatueleza hivyo hivyo, hakuna mabadiliko yoyote yanayoonekana yanaendelea. Kwa sababu tunafika pahala tunaelewa maana hizi bajeti ndio tunapitisha hapa mipango yenu ya maendeleo tunapitisha hapa, mipango yenu ya matumizi tunapitisha hapa. Sijui haya mabadiliko ni mabadiliko ya aina gani. Na sisi ndio sehemu ya jamii tunaelewa kila linaloendelea, wafanyakazi ndio wapo huko katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili jambo linahitaji kuchukuliwa hatua muafaka na kwa sababu ni jambo linaloathiri kada nzima ya utumishi. Juzi tu hapa tumekuwa tukisikia wenzetu Tanzania Bara wanapiga kelele juu ya mshahara wanataka kima cha chini cha mshahara kiwe laki tatu na ngapi. Mhe. Raisi akatoa *statement* kali kila mmoja akaisikia kwamba Serikali ya Tanzania haina

uwezo wa kulipa kima hicho. Lakini mbali na kima hicho lakini hichi kima cha laki moja ni kidogo mno hakitoshi, pamoja na unyonge wetu na umasikini wetu ni lazima na sisi tujikurupushe kidogo. Tusisubiri kama yale yaliyotokea kwa wenzetu Tanzania Bara basi *at least* tutoke hapa kwenye laki moja tusogee basi japo laki moja na nusu. Wafanyakazi wetu watajua kwamba kweli serikali ina niya ya kuwasaidia lakini hali yetu ni ngumu. Lakini tunapo *mark time* kila siku, kila wakati basi kwa kweli watumishi wetu wanakata tamaa, wanavunjika moyo. Kiwango hiki ni kidogo kinahitaji kuangaliwa kwa kina. Lakini pia na masuala mazima ya wataalamu wetu wanahitaji kuangaliwa, madaktari, wataalamu mbali mbali wanatukimbia. Sasa hivi lugha za kila siku tunafanya *scheme of service*, tunafanya hivi, lakini utekelezaji wake hauonekana kwa kweli mwisho lugha hizi watu watazichoka.

Mhe. Mwenyekiti, kauli zetu zifanane na vitendo au zifuatiwe na vitendo, tusiwe kila wakati tunazungumzia jambo ambalo hauonekani utekelezaji.Hapo hapo mwenzangu amezungumzia juu ya hiki kiwango cha pencheni ambacho kimeongezwa kutoka 15,000/ - 25,000. Mimi nitazungumzia zaidi juu ya wazee wetu wa Sebleni ambao tumewaweka pale, tumewatoa katika maeneo yao tukawahifadhi pale katika nyumba za serikali, wale hawana baba wala mama na ndio maana wako pale, wanalipwa shilingi 25,000 kwa mwezi.

Hebu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, *imagine*, kama wewe unapewa shilingi 25,000 utaishi vipi? Kwa kweli huwezi kuishi, wale ni watu wazima tuliowaweka pale, wanahitaji matunzo ya kila aina, wanahitaji kulala pazuri, kula vizuri, watunzwe vizuri afya zao, lakini tunawalipa shilingi 25,000 kwa mwezi. Kweli hatuoni kwamba itakuwa kama tumewatelekeza? Na sio wengi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kwa makusudi tumeamua kuwaweka pale, serikali imeamua kuwaweka pale ni wajibu wa serikali kuhakikisha wazee wale wanaishi kwa raha mustarehe. Wanapata chakula chao cha kawaida. Leo wanatoka pale wanakwenda kukopa katika maduka na hawana uwezo wa kulipa, wanakwenda kukopea shilingi 25,000, kweli wanaweza kuishi? Na badala yake wanakuwa omba omba sasa, wengine wanakwenda madukani kwa Wahindi kwenda kuomba, akiulizwa unakaa wapi, mimi nakaa kule Nyumba za Wazee Sebleni, masikini ya Mungu.

Sasa hawa lazima tuwaangalie tusijiangalia sisi tu wenye nguvu, wale tuwaangalie na tuwatupie macho. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mbali na uwezo mdogo tuliokuwanao lakini lazima serikali iwe inazingatia katika maeneo haya muhimu. Tutakapowazingatia hawa ndio tutakapopata baraka kwa Mwenyezi Mungu. Nchi yetu hii itafaidika, lakini leo tukiwafanyia hivi wanavyohangaika na kuomba, matokeo yake hata baraka katika nchi itakuwa haionekani.

Tusiwe kila wakati tunajivutia sisi tu kama pweza, lakhasha, na wale wazee wetu tuwaangalie ili tuone wanaishi maisha mazuri. Yasiwe maisha ya kuomba omba. Mimi Mhe. Mwenyekiti ombi langu ni hilo.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, ni suala la Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, afisi hii ina kazi kubwa. Kama tunavyojua sasa hivi nchi yetu imejiunga katika Jumuia za Kikanda hizi ziko nyingi, kuna *SADC*, *COMESA* na nyenginezo, ambazo kwa kweli jumuia hizi au umoja huu unahitaji kushughulikiwa ipasavyo. Pamoja na kwamba tumejiunga kupitia mwamvuli wa Tanzania, lakini sisi kama Zanzibar tuna maeneo yetu. Kwa hivyo, niiombe serikali iimarishe sana kitengo hiki, ni kitengo muhimu ambacho kitaweza kusaidia katika mambo ya uhusiano wa kimataifa na tusione gharama.

Wale wanaohusika kwenda katika mikutano basi washughulikie waende kwenye mikutano wakatuwakilishe, tena wawe wataalamu wasiende kule wakafunga mikono wakiondoka wakarudi. Tunataka watuwakilishe kweli katika mikutano hii ya kikanda. Kwa kweli afisi hii inahitaji kuwa na nyezo za kutosha, kuwa na afisi zenye hadhi, kuwa na wataalamu wa kutosha kwa sababu hawa ndio tunaowatuma kwenda kule.

Kama Mhe. Mwenyekiti, una wataalamu kidogo, basi afisi hii inahitaji kuwa na wataalamu wa kutosha. Sasa hivi tuna wasomi wengi, tuna watu wengi watoto wetu wamemaliza vyuo vikuu hawana kazi Basi angalau tumege sehemu ya pato letu tuwaajiri hawa wakatufanyie kazi. Watakapofanya kazi, watakapokwenda kule, watakaposhughulikia jambo hili, basi na sisi uwakilishi wetu utakuwa mzuri katika maeneo haya ya kikanda.

Lakini jengine katika eneo hili kumezungumziwa juu ya miradi ya Zanzibar. Pana miradi hapa ya Zanzibar katika *East African Community*, ambapo imesemwa kwamba, tayari miradi ya Zanzibar imewasilishwa kule ili iweze kutekelezwa kikanda na kupata mazingatio. Sasa mimi nataka kujua Mhe. Mwenyekiti, hii miradi ambayo sisi kama Zanzibar tumewasilisha kule ni miradi ipi na ipi. Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho basi utufahamishe. Lakini pia tujue kwamba miradi kama hii ambayo inawasilishwa kule kwenye *East African Community* inatafutiwa wafadhili. Ni sisi wenyewe tunaohusika au hii jumuia yenyewe ndio inayochangia kuwezesha miradi hii? Hapo tungetaka tujue.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema maeneo yangu makubwa ni hayo matatu ambayo nilitaka kutoa mchango wangu. Sina zaidi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia

mia moja na niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo wamesema watayatekeleza na waweze kuyatekeleza *Inshaallah*. Ahsante sana.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba hii.

Mimi sitachukua muda mkubwa, lakini pengine naweza kusaidia kwa sababu nilikuwemo serikalini muda mrefu. Nilipata bahati nikawa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, nikawa Katibu Mkuu Mipango, nikawa Katibu Mkuu Viwanda na Idara nyengine. Kwa hivyo, masuala ya utumishi nilikuwa ninauzoefu nayo. Sasa bahati nzuri baada ya muda nikenda Ng'ambo kwenda kujifunza vile vile masuala yanayohusu uongozi wa *Human Resource (Human Resource management*).

Katika serikali kuna shughuli mbili zinazostahiki kufanywa na serikali. Moja ni kuwaendeleza wataalamu wanaohitajika (*Human Resource Development*). Ninatoka skuli sekondari au *Form VI*. Aidha, unaajiriwa kwanza au kwanza unakwenda ukirudi unaajiriwa. Lakini kwa kawaida kunakuwa aidha na wizara kwa nchi kubwa au idara kama yetu inayoshughulikia na kuendeleza wafanyakazi.

Nakumbuka wakati huo tulipokuwa kule wakati ule idara ile ilikuwa kwenye Wizara ya Mipango na baadaye nadhani kukawa na mvutano kidogo wa usimamizi ikarejeshwa Wizara ya Elimu. Sasa wakati ule vile vile tulikuwa na kitu kinaitwa mpango wa miaka mitano, mpango wa mwaka mmoja, mpango wa muda mfupi, lakini tulifika *stage* tukawa tunajua kwa ile mipango tunayolenga ya nchi tunahitaji wataalamu wa aina gani.

Katika kukua kwetu tunataka kujenga hospitali, kwa hivyo, Wizara ya Afya inasema nitahitaji madaktari wa aina fulani kadhaa, nitahitaji watawala wa kuendesha hospitali kadhaa. Wizara ya Biashara inasema kwamba nataka watu wenye *degree of commerce*, swahibu yangu pale Wizara ya Maji ansema nataka ma-*engineer* wa mafuta, halafu lote lile kwa sasa unaliweka kwenye *screen* ya kompyuta halafu unaweza kusema mwaka huu lazima nipeleke watu 10 ili mwaka 2015 wawe wamerudi, mwakani nipeleke watu 20 ili 2016 wawe wamerudi na wakirudi huyu anakwenda hapa. Kwa jumla kulikuwa na kitu kinajulikana kwa wazi kabisa mipango yetu ya maendeleo ya mahitaji ya wataalamu.

Mhe. Waziri sina hakika ni muda mrefu nimetoka serikalini tangu mwaka 1988, siwezi kujidai kwamba nakujua. Lakini nadhani humu hamna kitu kama hicho, humu mna maelezo ya Idara ya Utumishi tu. Naomba utusaidie kwa hilo.

Kumeelezwa humu kwamba tayari katika utafiti wa Utumishi Serikalini kuna makada zaidi ya 25 zile sijui, zimegawika mafungu, kada 113. Hiyo nadhani ndio itakayotupa *structure* ya *scheme of service*. Lakini tukishaipata hiyo *structure* ya *scheme of service* tunahitaji kujua kwa hivyo hapo wataalamu wanaojaza hiyo *structure* ni nani. Ukishawasomesha kuna *human resource management*, wamesharudi sasa, unahitaji kuwa-*manage*, na kuwa-*manage* maana yake ni kujua ninawapeleka wapi, namhitaji huyu wapi kwa masharti gani ya kazi.

Moja katika kitu ambacho tunakisahau tunapokuwa serikalini, pengine na mimi nilikuwa hivyo hivyo, tunasahau kwamba kuna kitu kinaitwa *social contract*, Mkataba wa mahusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa. Kumekuwa na tabia ya kuamini kwamba ukishaniajiri unanimiliki, aa, uu, ata bwana, nimekuja aidha nina elimu yangu au na nguvukazi yangu, unanambia wewe utakuwa mfagizi wa ofisi hii nasema hewallah nakubali utanilipa kiasi gani kwa nguvukazi yangu.

Mahusiano yetu yanaanza hapo. Wewe unakuwa na masharti kwamba kazi hii bwana utakapofanya lazima uje saa moja na nusu uwe umeshafika kbala mimi sijaja ofisini, hewallah, saa saba nikitoka bwana nataka afisi uifagie kabisa kesho nikija safi, hewallah.

Yeye anasema sasa lakini jamani na mimi nikitoka hapa asubuhi nikienda huko tena sina kwenda shamba kulima muhogo ndio nimeshafika hapa. Kwa hivyo, utanigaia kiasi gani? Mnapatana ndio baadaye kunakuwa na mkataba wa mwajiri na mwajiriwa. Mwenzangu Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Salmin Awadh wamesema kwamba, hiki kilaki kimoja kiduchu sana, hakiungi.

Mhe. Abass Juma Muhunzi alikuwa akitoa hadithi hapa, mimi nataka kutoa kidogo na kina maalim Abdalla Juma wanajua. Sisi tulipomaliza Chuo Kikuu 1975 wakati ule kulikuwa na kitu kinaitwa *gross* , nadhani swahibu yangu Katibu Mkuu wa Ikulu ambaye ni Katibu wako sasa anaijua vizuri *gross*. Tulikuwa tunapata shilingi 144 ghafi kwa mwaka mzima, ni kama tulikuwa tunajitolea kwa ule utaratibu wa kwenda JKU, lakini kwa sababu tulikuwa tunahitajika kusomesha ndio tulilipwa hiyo.

Lakini baada ya kumaliza mwaka tulilipwa nakumbuka elfu moja, mia moja na kitu hivi, lakini siku zile mimi mwalimu wa Beit-el-Rass zikinitosha na

zinabaki, wale wenzetu mliokuja hivi karibuni mjue hivyo, 1,140 ilikuwa inazunguka mwezi bwana na ndani nina kilo 50 za packet ya sukari, unga na kipolo cha mchele, pengine na nazi kama mia za kukaa mwezi mzima. Sasa ninapokwenda Beit-el-Rass kushika chaki au Lumumba.

Mhe. Mwenyekiti nakumbuka alikuwa ni mwanafunzi wangu siku zile *Form IV* na *VI*, nilikuwa nikianza kushika chaki pale wananishangaa, lakini kumbe ilikuwa bukheri, najua nikienda nyumbani nitakuta mashondea kule yameshapikwa. Sina hakika kama mwalimu wa sasa yuko hivyo, sina hakika. Ni kwamba hali ya malipo hailingani na ugumu wa maisha.

Lakini kuna tatizo la pili vile vile. Kuna Idara ya Utumishi Serikalini na kuna Chuo cha Utumishi wa Umma, sina hakika labda Mhe. Waziri atatusaidia, sijui katika hivi inaonekana hiki chuo kiko chini ya hii idara, inawezekana. Kwa hivyo, Idara ya Utumishi itakuwa inapeleka watu wake kwenye Chuo cha Utumishi kwa kujua kwamba watu gani wanaowahitaji, pengine kama kinafanya hivyo.

Lakini kumekuwa na tatizo moja ambalo halipendezi kidogo. Kuna watu walikuwa na nafasi kubwa tu kwenye serikali, lakini mabadiliko ya uongozi kwenye serikali ni kawaida hata sisi tulikuwa tukibadilishwa. Lakini wote huishia kupelekwa Idara ya Utumishi na hali wana utaalamu, inakuwa kama ile ni *pool* ya wale waliokuwa vya kufanya hawana. Anakuwa kama vile ni *redundant*. Wengine ni wanafunzi wetu wakisoma na Mhe. Mwenyekiti pale. Wakikuta maalim shikamoo, marahaba, siku hizi uko wapi? Ehe anacheka, niko Idara ya Utumishi, lakini wewe nakumbuka kama …anasema ndio lakini bado sijapangiwa kazi. Kidogo haipendezi. Utaalamu wanao tena utaalamu wa uzoefu.

Bahati mbaya tu alikuwa Katibu Mkuu na lazima mmoja aingie mmoja atoke ndio kawaida, lakini kwa sababu ana uwezo nadhani tunahitaji kuwapangia kazi. Hii ndio *problem* ya *Human Recourse Management*, hapa ni tatizo la *management*, kwamba wataalamu tunao, wapo pale, tunashindwa kuwapa kazi na utaalamu wanao.

Hili linatokana na nini? Linatokana kidogo naomba kulaumu kidogo na siwalaumu nyinyi, nawalaumu hata marais. Kwamba tumechanganya shughuli za utumishi na siasa. Nakumbuka nilipokuwa nafanya kozi yangu Uingereza nikasoma taarifa moja ambayo ilikuwa inahusu nchi ya Ghana. Ghana walipokuwa wanapewa uhuru, yule Gavana pale katika kitu kimoja alichokiandika kuwaachia kumbukumbu anasema:

‘Bwana Nkrumah nakupa uhuru uendeshe nchi yako, lakini tafadhali usije ukauchukua utumishi wa serikali ukaingiza kwenye siasa, utakuwa umemaliza kabisa utendaji wa serikali’. Lakini kwa bahati mbaya takriban serikali zote za Kiafrika, tumeuchukua utumishi tumeuingiza kwenye siasa. Tunahitaji kuacha wataalamu wakafanya kazi zao za kitaalamu na wakawa wanapandishwa madaraka kwa kulingana na utaalamu wao na ndio maana ya hii *scheme of service*. Pale ninapohitajika kwamba sasa niingie kwenye nafasi ya kisiasa lakini isiwe ni kisingizio aidha cha tunza au adabu, iwe ni kuonekana kwamba hili nitaliweza kulifanya kuliko mwenzangu. Sasa matokeo yake ndio unapata hizi *redundancy*.

Tatizo si *redundancy* tu Mhe. Mwenyekiti, tunapata na kitu kinaitwa *over employment*. Madhali Juma Duni Haji mtu wa Kaskazini na Babu Hamadi tuko chama kimoja *CUF* basi nitamchukua babu Hamadi hata kama hawezi, ni makosa. Tunaharibu utumishi kufikiria kwamba fulani madamu jamaa yangu nimpe nafasi hata kama hawezi. Hilo moja.

Lakini la pili sekta yetu ya uzalishaji ni ndogo. Kwa hivyo, tungetegemea *establishment* au utumishi wa serikali uwe unakua kulingana na ukuaji wa sekta ya uzalishaji, matokeo yake utumishi unakua lakini tunaajiri walaji tu. *Most of the employed people are consumers* ni walaji tu, hajikusaidia kuongeza uzalishaji, yaani kuna kitu kinaitwa *productivity* hamna.

Mhe. Mwenyekiti, lililo baya zaidi ni kwamba tunamuajiri kwanza halafu ndio tunatafuta kazi ya kumpa, badala ya kuwepo kazi halafu tukamuona nani tumuajiri, matokeo yake tunapata tatizo.

Juzi tulipokuwa tukizungumza bajeti ya Wizara ya Fedha ya jumla niligundua *almost* 50, 50, asilimia 50 ya ile bajeti ni mishahara na asilimia 50 ni *other charges*. Ukiitizama hivi hivi Mhe. Mwenyekiti, huoni, lakini *other charges* maana yake ni kwamba karatasi iwepo, gari liwe na mafuta, limeharibika litengenezwe, simu inafanya kazi, umeme unalipiwa na vitu vya namna hiyo. Ikiwa *other charges* ni ndogo ndio ile aliyosema Mhe. Said Ali Mbarouk milioni moja kwa urojo. Watu wanazungumza cha kufanya hawana, saa nne wako marikiti au asubuhi anasema nimekuja kuandika jina lakini bosi akiniuliza mwambie leo kidogo nimedharurika. Hana kazi ya kufanya lakini analipwa.

Wakati mmoja Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi nilikuwa niko pale Mipango akawa anapata hilo tatizo la bili ya mshahara mikubwa, akatuita akatuambia nakupeni wiki mbili mniletee hasa mshahara halisi wa wafanyakazi wa serikali. Siku zile inaitwa Tume ya Mipango ile tukakesha pale, ikabidi tupitie kila *voucher* za

mishahara za kila wizara, tulikuta hewa nyingi kweli kweli. Watu walikuwa wapo wengine hawapo, mishahara inalipwa. Nadhani kuanzia pale tulikuwa na *scheme of service* nilipotoka mimi ilikuwepo lakini baadaye bila shaka inabadilika inakuja nyengine kama inavyofanywa sasa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji kubadilika tuhakikishe tunayemuajiri kazi ipo kwanza, tunahitaji kubadilika kwamba tunachokitaka kwa ajili ya watumishi tuwe tumeshakipanga na hapa nakuja kwenye tatizo la walimu. Bila shaka itakuja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hapa, lakini moja katika tatizo ambalo hivi sasa tunalipata ni ukosefu wa walimu wa *science*.

Ukosefu wa walimu wa *science* ni kwa sababu hatukujipanga katika hilo suala tunalosema la *human resource development*. Sioni aibu mimi ni mwalimu wa *science*, lakini leo niko Baraza la Wawakilishi mwanasiasa. Ni matokeo sikuchagua, lakini kuna siku nilipata shida nilikuwa ninahitaji madawa fulani, nilitaka *sulphur* dawa ya upele, kibiriti upele. Sasa nikasema ah, hebu niende Lumumba, kufika pale nikawakuta wanafunzi wangu waliokuwa pamoja na Mhe. Mwenyekiti ndio walimu. Akasema mwalimu naona haya kukupeleka *laboratory*. Kwa nini? Twende. Aa liko vibaya bwana, hamna chochote.

Sasa nikasema kama wanavyosema jamaa zangu kuwa, kama kilemba kimeroa sasa mkuti uko haligani? Kama Lumumba *laboratory* iko hivi, ile sekondari ya kule Mkwajuni na Mfenesini kwa Mhe. Ali Abdalla ikoje? Ilikuwa kila wiki lazima mwenyekiti wafanye experiment, lazima kila wiki, wanaingia *laboratory*, wanachezea madawa yale na wewe uko pale ni hatari kwamba wasiungue, mara nyengine wanafanya majaribio ya madudu ya ajabu ajabu. Wanakwenda wanalifungua lile dudu la *sulphur* pale lililokuwepo, unakuta chumba kizima, lakini ulikuwa unahisi kwamba kuna kitu kinafanyika.

Leo mtoto ukimuuliza *bunsen burner* haijui hajaiona, anapigiwa picha pale basi anaambiwa. Ukitaka ku-*test carbon dioxide* unafanyaje? Unatia hiki na hiki unapata hiki. Haoni anaambiwa kwa nadharia, matokeo yake siku zimepita mpaka ile elimu ya sayansi inadharauliwa inaonekana kama si muhimu. Tuna walimu wengi lakini si wa *science* na sisemi haya kwa kuwa labda naponda tu.

Nina mwanangu mtoto wa kaka yangu mwalimu wa dini, nina mwanangu mtoto wa kaka yangu mwengine mwalimu wa dini, nina mwanangu mtoto wa kaka yangu mwalimu wa dini, sisemi naiponda dini, lakini hee, nawaambia jamani ukoo mzima tutakuwa mashekhe nani atamsomesha mwenzake? Tuna tatizo jamani.

Juzi akaja mtoto mwengine wa ndugu yangu mambo yamemkaa huko Dar es Salaam nadhani mnafahamu. Nimekuja kaka nakutafuta, nikamuuliza vile wewe ndio nani? Mimi mtoto wa fulani. Nikamuuliza unafanya *degree?* Akajibu ehee, *Degree* gani? Akanambia ya *science*, nikashangaa ya *science*! Nilimuuliza mara nne, akaanza kunambia jinsi watoto wanavyochukia kufanya *degree* ya *science*. Sasa hii yote Mhe. Mwenyekiti ni kukosa mipango ya *Human Resource Development*.

Tuna vyuo vingi *Alhamdulillah* nashukuru, kuna vyuo *SUZA*, vyengine mpaka majina nayachanganya, kuna *SUZA* sijui na Tunguu na kwengine. Lakini idara za *science* nadhani hazijawa na walimu wa kutosha. Ni kwa sababu tuliidharau *science.*

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nimalizie kifungu 35 kimesema pale kwamba kuna mashirikiano. Bora nikisome.

Kifungu cha 35:

> "Utawala wa Umma umefanya kazi nzuri ya kuimarisha uhusiano na vyuo vingine. Katika kipindi hiki Chuo cha Utawala wa Umma kimekubaliana na Chuo cha *VETA* cha Chang'ombe kushirikiana katika maeneo ya kubadilishana wataalamu na uzoefu katika kuendesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi".

Hapa nina mifano miwili, nina kijana wetu hivyo hivyo, ninajitolea mifano mimi kwa sababu ndio ninayoijua. Huyu nadhani kamaliza *Form II* au *Form III*, analelewa na mashemegi zangu lakini mtundu wa mambo ya *electronic.* Hizi simu akizishika anazifungua anazichezea, sasa yule akanijia akasema kaka Juma huyu mtoto tunahitaji kumsaidia. Tumemsaidia ndugu zangu akaenda *VETA*, hivi sasa nadhani ndio anaongoza Idara ya *ZANTEL* hapa kwa *technician.* Kwa hivyo, siku hizi nikipata matatizo ya compyuta na nini, namwita babu Haji hebu njoo, akifika pale paratata paratata, anavuta hapa na pale, alikuwa kidato cha nne, lakini amesoma VETA ni kwamba amesoma *theory* lakini zaidi ni *practical* ambayo anatunza kwenye mikono yake, haji tena kutuomba pesa na siku hizi ana nyingi kuliko sisi. Kwa hivyo, haya mahusiano yasiwe ni ya nadharia yawe ni ya kufikiria vipi tutawasaidia vijana wetu wanaoranda mitaani huko.

Mhe. Mwenyekiti, kuna pale sijui elimu ya watu wazima nasikia wengine wanafundishwa kupika, sio kwamba ni jambo baya lakini nadhani tunahitaji elimu ya vitendo kuwaidia vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kile kifungu cha mwisho cha hitimisho. Mhe. Abdalla Juma alinukuu nilikuwa nimeshaiandika, ile aliyosema kuwa niwasihi viongozi na wananchi wenzangu kukubali mabadiliko yanayotokea.

Mimi nataka kuzungumza maneno mawili Mhe. Mwenyekiti, unistahamilie. Katika kujieleza ninapokuwa na wenzangu huwa nawaambia mfinyango wa miaka 50, hebu mfikirieni mama anavyokanda unga wakati anataka kufanya chapatti, yaani akili zetu kwa miaka 50 tunataka kupika chapati tunafinyanga tu. Unajua ule unga unakandwa tangu unakuganda mikononi unatia mafuta mpaka unakua laini, unaurusha mama ana ukata anazungusha, nadhani mnanielewa kina mama. Maana kina baba hawakai jikoni.

Kwa hivyo, miaka 50 tumefinyangwa tuchukiane. Sasa kufinyangua sio rahisi, lakini ni lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Sasa Mhe. Abass Juma Muhunzi alisema walioanza ni viongozi. Nilishawahi kusema kwenye Baraza hili kwamba anayestahiki kuanza kutufinyangua ni wale viongozi, kwa sababu wao ndio wenye amri. Yule mwenye nguvu za dola ni yule ambaye akisema hili liwe ndio mabadiliko yanaanza.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kutoa mfano hapa kwamba kama Diclac asingekubali kuzungumza na Mandela basi mpaka leo ngumi zingekuwa zinaendelea kule. Sasa tumepata bahati Mhe. Aman Karume na Maalim Seif Sharif wakazinduka na kusema jamani sisi ndio sisi na kabla ya sisi walikuwepo. Kulikuwa na wakati alikuwa anakaa Ramadhan Haji alikuwa aliitwa babu nahodha, kulikuwa na wakati alikaa Dk. Omar pale, kulikuwa na wakati anakaa Maalim Seif na alikuwepo Bilal. Kwa hivyo, sisi tupo tuwatayarishie wenzetu mazingira wanayokuja na hatuna cha kuwatayarishia isipokuwa kuwawekea mazingira ya amani. Kama hakuna amani uchaguzi wa nini, ndio nini uchaguzi kama hakuna amani, unamchagua Rais kwa vurugu ili aje aendeshe nchi kwa vurugu na ili wananchi wawe katika vurugu. Hata. Ni lazima tuwe na amani na uchaguzi uwe na amani na hakuna njia yoyote ya kuwa na amani kama hatujajitambua.

Sasa kujitambua maana yake nini. Namalizia Mhe. Mwenyekiti. Nisameheni kule kwenye chama chetu cha CUF kuna *slogan* huwa inaitwa zinduka, sasa ukisema hivyo zinduka maana yake ni kujitambua na kujitambua maana yake ni kujua kwamba mtendwa na mtenda ni mimi. Buku nimelinyanyua ni mtendwa, nimeizima spika ni mtendwa, lakini nikiondoka hapa nikija hapa mimi ni mtenda na mtendwa. Inapofika daraja hiyo unaambiwa umezinduka na unapozinduka ni kutambua kwamba kumbe kama mimi nataka raha, basi na

Mwinyi naye anataka raha na asingependa na yeye kuwa na shida kama mimi sizinduki.

Kwa hivyo, kimoja kinachotufikisha tuendelee kufikia kwamba mmoja ni bora kuliko mwengine ni umaskini. Nawaambia wazee wangu ukiona ugomvi umeanza popote kwenye familia basi kuna masuala ya kupata na kukosa. Utaanza kumwambia wewe ni wa Shangazi huhusiki, kwani kaingiaje, si mama yake kaja tu hapa kaolewa! Ndio inaanza hapo kwenye kupata na kukosa na kupata na kukosa wengine ni waroho, lakini hasa kunatokana na umaskini na umaskini wa Wazanzibari ni mkubwa mno, ni mkubwa ndugu zangu umaskini.

Umaskini sote tunaujua humu ndani. Siku moja nilikuwa pahala nahutubia nikawaambia zamani ulikuwa mchele unaitwa mchele wa chenga. Wazee mnaufahamu eeh! Kina Maalim. Mchele wa chenga ulikuwa unauzwa senti hamsini, babu Ali Abdalla, kibaba senti hamsini. Sasa siku hiyo mzee Duni hana pesa Mungu amrehemu akasema ndugu zangu wanangu nina senti hamsini hizi tuzifanye nini? Senti hamsini anatuonesha mzee. Kaka yangu na yeye ni marehemu akasema tukanunuwe mchele wa chenga, baba akasema tutaula vipi? Akasema baba hauna matatizo, kibaba kimoja kikipikwa uji hapa hatuuishi, baba akasema alaa! Haya nenda, tukafuatana ndugu zangu tukaenda kununua kibaba kimoja cha mchele wa chenga ukaja ukapikwa uji, tulikunywa tukatoka majasho mwingine tukauwacha tukaja kunywa asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, ni umaskini ambao naujua, nimeurithi. Wazanzibari ni maskini sana na moja linalofanya Wazanzibari kuwa ni maskini ni kwamba wale wenye madaraka tumeshughulikia kugombana, wewe bora, wewe mng'ang'anizi, wewe siye na watu wanateketea. Umaskini uko wa aina tatu. Umaskini maana yake ni kukosa pesa huo unaitwa umaskini kipato. Ukiwa na pesa ndio utapata boflo pale Darajani, ukiwa huna basi ukamuombe babu Juma au ukalale na njaa. Lakini ukishakosa pesa na mkate umekushinda unakuwa maskini hali.

Kuna siku moja nilimchukua mtu mmoja dhaifu hivi halafu nikamchukua na mmoja kavaa suti na miwani. Nikawaambia hebu niambieni hawa wawili twende kwa *Area commissioner* au *Regional commissioner* Maalim Abdalla Mwinyi tufike kwa karani wake, tumwambie tunataka kumuona. Huyu mwenye suti na miwani na huyu mzee nani ataitwa mwanzo ndani. Wewe mzee nadhani nafasi Mkuu wa Mkoa hana, lakini wewe bwana subiri. Yaani ile hali yake ya mkabala aliyonayo ndio kipimo anachopimwa. Haruhusiwi kuingia kwa maalim Abdalla sio kwa sababu hana akili, ni kwa sababu ya ile hali yake iliyotokana na ukosefu wa kipato.

Vile vile wakija watu wale wawili kwenye mkutano, babu Juma anaongoza mkutano, basi akinyanyua mkono mzee yule basi ataambiwa wewe mzee kaa kitako, eeh! Bwana mwenye miwani pale na suti hebu simama. Yaani hata ule mkabala wa kauli wewe unaonekana huna mawazo. Umaskini ndugu zangu maana yake sina ndio maana ya umaskini. Sina kitu, sina hali na sina chakula. Sasa haya yote yanatokana na sababu ya hali ya kisiasa ilivyo nchini, tukipata amani tutapata umoja, tukipata umoja tutapata maendeleo, tukipata maendeleo hatima ya mjukuu wangu na mjukuu wako wataishi maisha ya maana na maisha yanayoeleweka. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Pia mimi nikushukuru sana Mheshimiwa mwalimu wangu wa *Chemistry*, lakini kumbe hata somo la *Social* na *Political science* leo hapa umetuelimisha sana. Sasa na tumsikilize Mhe. Mzee Ali Ussi, kwa sababu ndio sasa hivi ameingia lakini pale mchana nilimtaja jina lake.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza ili tuweze kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa mmoja kati ya wachangiaji katika Wizara hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mimi kama walivyoanza wenzangu kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi ambavyo amewafanyia wananchi wa Zanzibar na leo tukiwa tunazungumza suala zima la kumpongeza sote kwa umoja wetu kwa pande zote mbili. Kila mmoja anayesimama amekuwa akimpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake za dhati kabisa na kujitolea katika kuhakikisha kwamba Zanzibar ni njema atakaye na aje inafanikiwa na kuona kuwa maendeleo ya Zanzibar yanafaidika kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo vile vile sina budi kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kutusaidia sisi viongozi wake ambao ametuteua kuwa wasaidizi wake katika nyanja mbali mbali Mawaziri, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa na wengineo ili kuweza kutekeleza vyema majukumu haya ambayo tumepewa.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumzia suala zima la amani na utulivu ni jambo ambalo limefanikiwa sana katika awamu hii ya sita ukilinganisha na huko tunakotokea. Hii yote inatokana na juhudi za viongozi wetu kuona kwamba

kuna haja ya makusudi kuona kwamba hali ambayo tumetokanayo nyuma basi tuiwache na hivi sasa umefika wakati twende pamoja. Mimi naunga mkono hayo kwa sababu yamesaidia sote kwa umoja wetu tunaishi kwa utulivu na amani.

Mhe. Mwenyekiti, hili sio la kificho. Kuna kipindi fulani nakumbuka tulikuwa kwenye kamati ya Baraza na mimi nilikuwa mjumbe wa kamati ya katiba, wakati ule kulikuwa na daftari katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Tulikuwa na wenzetu mbali mbali tunakwenda kule, kwa bahati nzuri baada ya kufika Chake Chake pale, wengi tulipotoka huku tulikuwa kitu kimoja, lakini baada ya kufika Chake Chake pale kama kesho yake nafikiri ndio daftari linahamia Kaskazini Pemba, basi watu wote walikataa wakasema sisi hatwendi, tutabakia Chake Chake. Lakini kwa bahati nzuri na mimi Mwenyezi Mungu alinipa ujasiri nikasema mimi nitakwenda huko huko. Nikakaa pale Bomani bahati nzuri mpaka tumemaliza tulikuwa salama, lakini ile hofu tu jinsi ilivyojengeka ndio watu walishindwa kwenda kukaa Wete ambako kulikuwa na daftari tu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo jema kwamba imefika wakati tuhakikishe kwamba tunakuwa kitu kimoja katika hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningetaka kuipongeza Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kama wenzangu walivyosema kwamba hii Idara ya Uratibu ambayo imeanzishwa katika afisi hii, ni idara ambayo inafanya kazi nzuri na imewezesha mambo mengi kwenda vizuri, hasa katika ufuatiliaji wa mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua idara hii inaongozwa na Katibu ndugu Raphael ambaye ni mzoefu katika mambo haya na kwa kweli anafanya kazi vizuri. Kwa hivyo, mimi ningependa kumpongeza ndugu Raphael katika kazi zake hizo. Kwa sababu mwanzo tulikuwa na malalamiko mengi Mhe. Mwenyekiti kama utakumbuka katika Baraza letu hili kuwa hatushirikishwi kwenye mambo mbali mbali. Lakini katika kipindi hiki kifupi baada ya kuanzishwa hii idara wajumbe wetu aidha watakuwa wameshindwa katika kutekeleza majukumu yao pengine pale pale ambapo pana upungufu wa fedha, lakini sio sababu ya kuona labda hakuna taarifa hii na hii. Kwa hivyo, suala hili ni la kupongezwa Mhe. Mwenyekiti.

Jengine ambalo nataka nilipongeze Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar ni suala zima la utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kuanzia mwaka 2000/2005 na 2005/2010. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi hapa kwamba tulikuwa na mambo mengi ambayo tulishindwa kuyatekeleza kutokana na uchache wa rasilimali hasa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, tulipoingia kwenye Baraza lako hili tuliwahi wengine kuona kwamba inafika mwisho wa mwezi huna uhakika kuwa mimi nitapata pesa, yaani mwezi wa pili ndio mnaweza kupata pesa au pengine katikati ya mwezi wa tatu ndio mnapata pesa. Hii yote ilitokana na pengine usimamizi ambao ulikuwa sio sahihi wa fedha. Kwa sababu hakujakuwa na mambo mengi, lakini ni mambo yale ya usimamizi wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwamba mara baada ya kuchukua nafasi hii akasema basi hii Idara ya Fedha niwe nayo mimi mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, ukilikumbuka hili hata Rais wa Zanzibar wa mwanzo Mhe. Abeid Aman Karume na yeye vile vile katika Wizara ya Fedha hakuwa na waziri wa fedha, yeye mwenyewe alikuwa anashughulikia masuala ya fedha kwa wakati ule wa awali. Kwa sababu bila ya fedha hakuna jambo litakalo kwenda.

Mhe. Juma Duni hapa ametuambia kuwa bila ya fedha maana yake kila kitu kinadharaulika, kwa hivyo kuwepo kwa fedha maana yake ndio kuthaminika kwa jambo lolote lile. Sasa kwa sababu ya kusimamia vizuri fedha nafikiria ndio tumekwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulipongeza ni katika utekelezaji wa ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ambapo tulisema tutafanya mambo kadhaa wa kadha. Kwa hivyo, katika kuangalia ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tumetekeleza ilani kwa asilimia 90 au zaidi kama tutafanya tathmini.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia suala zima la majengo yetu ya Michenzani tokea yalipokwama katika kipindi kile Mzee Karume alipoyawacha majumba yale hayakushikwa, yameachwa. Lakini katika uongozi wa awamu ya sita hii, ukiongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar umeweza kuyakamilisha na hivi leo wazee wetu pale ambao walikuwa wanadai nyumba zile wamepewa na kila mwenye haki yake amepewa. Kwa hivyo, hii inaonesha dhahiri kwamba utekelezaji wa ilani umekwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningependa nilipongeze ni suala zima la usimamizi mzuri katika wizara zetu mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, wizara zetu zote zimefanya vizuri kwa wastani. Kuna upungufu kama utakuwa umeangalia vizuri kwenye yale masuala mengi ambayo tulikuwa tukiulizwa basi sasa hivi yamepungua.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ilikuwa maana yake ukifika hapa basi unakuwa na wasi wasi kuwa utaulizwa hili na hili. Lakini hivi sasa Mhe. Mwenyekiti tumefanya vizuri katika wizara yetu, lakini pia nataka

niwapongeze sana wajumbe wa kamati ya mawasiliano na ujenzi wakiongozwa na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu na msaidizi wake Mhe. Hamad Masoud, pamoja na kina Mhe. Zakiya Omar Juma wametusaidia sana. Wametusaidia kwa sababu watu wanasema unapokuwa na mtu ambaye ana uchungu wa lile jambo basi lazima utafanikiwa. Wenzetu hawa wamekuwa wakiliona jambo mahala popote pale basi wamekuwa karibu na sisi kutueleza kwamba kuna sehemu hii na hii na sisi tunakaa nao pamoja na tunafuatilia na matokeo yake tunakwenda kwa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi Dk. Mwinyihaji.

Mhe. Mwenyekiti, Dk. Mwinyihaji kwa kweli tunafaa tumpongeze sana kabisa. Amekuwa ni mtu msikivu, ilimradi ujenge hoja nzuri, ukishajenga hoja basi suala la fedha kwa Dk. Mwinyihaji halina tatizo. Kwa hivyo, tunapokuwa na kitu kama hicho basi tunafaa tujivunie kwamba wenzetu hawa wamekuwa ni wawajibikaji.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko wa barabara umekuwa ni mkombozi sana kwa barabara zote ambazo zinajengwa. Leo asubuhi Mhe. Hija Hassan alikuwa ananiuliza kuhusu habari ya vyombo vile ambavyo vimepelekwa Pemba, ni vyombo gani na vyombo gani katika mambo ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara? Nikamwambia nitamjibu.

Mhe. Hija Hassan Hija nilimjibu asubuhi kwa barua yangu ndogo, lakini pia nataka niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kwamba tulipokuwa tukijenga barabara katika awamu hii ya sita, tulikuwa tunapata tatizo Pemba, kwa sababu barabara Pemba ukitaka kujenga lazima uwe na *bulldozer*. Sasa *bulldozer* kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine Pemba ilikuwa ni lazima upite mwituni, unaweza kutumia wiki mbili au siku sita au saba mpaka nane hujafika mahala unapokusudia.

Lakini leo tunalo lile gari kubwa la kuchukua *bulldozer* kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine hakuna sehemu yoyote ya Pemba ambayo hatuwezi kuifikia kwa muda wa saa 1:00 mpaka saa 1:30. Kwa hivyo, hili ni jambo moja zuri ambalo litatuwezesha kufanya kazi zetu vizuri. Yote hayo yanatokana na juhudi za serikali katika kuona kwamba tunafanyakazi hizo vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo napenda kulizungumza ni kuhusu suala zima la Tume ya Utumishi Serikalini. Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi Serikalini inafanyakazi vizuri na katika utendaji wake basi ni kwamba inahakikisha kuwa wale wote ambao wanafanyakazi na kuwajibika, basi aidha wanapandishwa vyeo. Sijafanya uchunguzi kama Mhe. Haji Faki Shaali asubuhi alivyozungumza labda pengine kuna watu wana miaka mingi

hawajapandishwa vyeo na mambo kama hayo. Lakini ninachoelewa mimi ni kwamba watu wanapandishwa vyeo kutokana na juhudi zao za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza kweli ukawa ulikuwa kazini kwa muda mrefu, lakini kuwepo kwako kazini muda mrefu hakusababishi kwamba wewe upandishwe cheo, kwa sababu pengine juhudi yako ya kazi haitoshi. Lakini unapokuwa na juhudi nzuri ya kazi maana yake yule ambaye anakusimamia basi anaona kwamba wewe kweli unafaa kusimamia kazi ile na kazi inakwenda vizuri. Sasa pengine sina hakika kwa wale ambao pengine hawajapandishwa vyeo au daraja kuna matatizo gani, lakini mimi ninavyoona ni kwamba katika utafiti wangu maeneo mengi tumeona viongozi au wafanyakazi ambao walikuwa wakifanyakazi katika maeneo ya chini, lakini leo wanafanyakazi katika madaraja ya juu ambayo inategemea na juhudi zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka wakati nacheza mpira, tulikuwa tukicheza mpira na mwenzetu mtendaji ndugu Omar King. Tuliwahi siku moja kuja kucheza nao hapa Kiwajuni wakati wako kwenye timu ya Small Simba ile, wakatupiga magoli kama matano hivi nakumbuka, kwenye timu yetu ya *danger boys*, maana yake kama hatumo. Lakini sasa kwa sababu hizo, ndugu yetu ambaye tulikuwa naye pamoja pale lakini kutokana na yeye mwenyewe kujielimisha, kwa hivyo, leo pale ndiye anayesimamia fedha na kwa kweli tunakwenda vizuri kutokana na utaalamu wake na juhudi zake lakini pia kutokana na mashirikiano ya uongozi moja kwa moja. Sasa haya yote Mhe. Mwenyekiti, yanatokana na lile ambalo nimesema usimamizi wa hali ya juu uko vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hii ni wizara yetu, kwa hivyo ni lazima tupongeze pale ambapo ni pa kupongeza, lakini vile vile pale ambapo panahitaji mkazo basi tutilie mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba imetajwa sana. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme kwamba Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba Afisi ya Rais Ikulu, kuna haja ya makusudi kuona kwamba jengo lile tunalifanyia kazi vizuri ili kuona kuwa na pale panakuwa na mahala ambapo kidogo panaridhisha, kutokana na hali yake ilioko hivi sasa.

Lile jengo ni la zamani Mhe. Zainabu Moh'd mara nyingi tulipokuwa tukitembelea katika kamati alikuwa akitupa malalamiko yake, lakini bado ikawa haijafanikiwa. Leo hii ninafuraha kuona kwamba Mhe. Waziri amezungumzia jengo hili, ili kuona kwamba linataka kujengwa na ninafikiri litajengwa wakati muafaka, ilimradi fedha zitakapopatikana basi tutapiga maendeleo.

Hata Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, asubuhi alizungumza hapa kwamba ni vyema sasa umefika wakati tuwe tunajenga majengo ya afisi zetu za serikali ya kisasa ili twende na wakati. Mimi nakubaliana naye kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nyumba nzuri na mambo yake yanakua mazuri tu. Lakini unapokaa kwenye kijumba kibovu basi na ukaaji wake unakuwa ni wa wasi wasi.

Mhe Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi pale afisini kwangu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi nimehama na nimekwenda Bohari. Nimehamishwa na watu wa Mji Mkongwe wanasema wakati wowote hapa pengine tunaweza kupata tatizo. Kwa hivyo, kuna haja ya makusudi kwamba tujenge majengo mazuri ya kisasa katika wizara zetu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jambo hili naona linawezekana kwa sababu tumeanza vizuri tu. Tulianza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tukenda Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Mazrui hakuliona pale, lakini tunalo jengo zuri. Pia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto nao wamefanyakazi nzuri wamejenga vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, na wizara nyengine Mwenyezi Mungu akitujaalia tunategemea kuona kwamba hata kama sisi tumeondoka, lakini angalau tumeweka misingi ya kuona angalau basi tumepata japo kiwanja cha kuona kiwanja hiki kitajengwa wizara fulani. Kwa hivyo, hilo nalo ni la busara.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumza ni kurudia tena kumpongeza Mhe. Rais katika suala zima la ustaamilivu wake wa kisiasa. Mhe Mwenyekiti, tunakumbuka mwaka 2005, tulikaa muda mrefu ikawa wenzetu upande wa pili walikuwa na mataizo ya hapa na pale hawakutaka kushiriki kutokana na mataizo yaliopo. Lakini hata hivyo, tulipofika katika hatua ile ya kujaza nafasi ikawa nafasi zimekwenda tupu mpaka baadae zikajazwa na viongozi waliopo kwa upande mmoja.

Lakini kwa upande wa pili kipindi hiki tunachomalizia tumeona kwamba yale ambayo yameleta ustaamilivu wenzetu wameona kwamba Mhe. Rais kwa kweli ni mtu ambaye kuna haja ya kuungwa mkono, wamekubali wenzetu kwamba Mhe. Rais ni Rais wa Zanzibar ambaye amechaguliwa kihalali na Katibu wa Chama cha CUF amekwenda Ikulu kuonana na Mhe. Rais ili kuondoa tofauti ziliopo. Leo tunaye Mhe. Nassor Ahemed Mazrui katika Baraza letu hili ambaye anatoa mchango wake kwa Baraza hili, wa kina kabisa na pengine kama tungekuwa hatupo basi tungekosa mchango wake. Hii yote ni kuonesha kwamba utekelezaji huu wa ilani yake na ahadi zake zimekwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningependa nilizungumze, ni hili suala ambalo pengine Mhe. Zakiya Omar alipokuwa akichangia asubuhi alilitaja na bahati nzuri liligusa wizara yangu, ni kuhusu suala zima la barabara ya Chuo cha Utalii Maruhubi. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ina ahidi mbele ya Baraza hili tukufu kwamba hili suala bado hatujalifumbia macho, lakini kama tunavyoona kwamba kazi tunazo nyingi kama mnavyoziona, kwamba tuna kazi za ujenzi katika maeneo mbali mbali ya barabara na tunaangalia pengine lipi tuliweke mwanzo na lipi liweze kusubiri.

Lakini tunachosema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hali hiyo ya barabara tumeiona na tutaifanyia kazi pengine kabla ya kumaliza kipindi chetu hichi ambacho tunacho na Mhe. Zakiya Omar pengine tutakuja kukualika kuja kuona eneo la Maruhubi pale kwamba likoje. Hasa ukizingatia kwamba sasa hivi tumekamilisha karibu taratibu hizi za ujenzi wa barabara ya Mkokotoni hapa tulikuwa tukifanya mtengenezo madogo madogo pamoja kuweka *overlay* katika zile sehemu ambazo zilikuwa zinahitajika kuwekwa *overlay*.

Pia tumeweza kukamilisha barabara ya Chumbuni leo tumemaliza hapo barabarani. Kwa hivyo, nimoja katika mambo ambayo kwa kweli tunayathamini sana kuona kwamba tunakuwa na barabara nzuri. Kwa hivyo, ukiwa na barabara nzuri maana yake maendeleo yatapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi kwa upande wangu nilikuwa zaidi nataka nitowe pongezi tu kwa Mhe. Rais wa Zanzibar, sikutaka ziadi kuangalia kwenye kitabu hapa na kuangalia mambo ya mahesabu na nini na hasa kwa sababu nisinge changia wizara hii, basi nisingejifanyia vyema mimi mwenyewe binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti kwanza na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii kupunguza kumalizia muda maana siumalizi, mimi nimekusudia nichangia Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti nianze moja kwa moja kwa sababu muda uliobakia ni mdogo na nataka niuchangie vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti nataka kuzungumzia kuhusu soko la biashara yaani *free trade area* tunapoyazungumza mambo na sisi wenyewe tuwe tunayafahamu na wananchi wetu wayafahamu, hivi ukizungumzia mambo ya SADEC husikii popote mpaka wakati wa bajeti. M natwambia nini tukawaambie wananchi kule tunakokwenda. Kwa sababu wataona kama tunaimba tu hivi, mmejaza vitabu

vyenu hivi kwa mambo ya nje huko hatupati maelezo tunayakuta hapa hapa. Hebu twambieni tukusaidieni nini katika michango maana yako maneno yanasemwa Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

> *"Hatua za awali za ushirikiano katika eneo hili zilizochukuliwa ni wananchi kupunguziwa kodi pole pole kiwango kama kilivyo"* mwisho wa kunukuu.

Sasa hebu tuulizane hawa wananchi wanapunguziwa kodi ipi maana yake masoko haya ni masoko ya biashara za nje ya nchi na sisi Wazanzibar kwanza hatuna ile bidii ya kuhimiza ya uzalishaji, sasa sentensi kama hizi kama mimi mshamba wa mbali mnanichanganya ndio maana ukaona kitabu hiki cha Dk. Mwinyi Haji kila mtu akikigusa anakiweka, analeta mambo ya siasa. Kwa sababu hamna kitu ambacho tunakielewa lakini vitu kama hivi mnatuelewesha kabisa tuvijuie kwa sababu mnatutuma tukaseme, sasa nyinyi mkienda kwenye mikutano ya Afrika ya Mashariki mnakuja na vitabu vyenu hivi sisi hatuyajui, sasa sijui kama mimi tu au na mwenzangu Mhe. Hijja Hassan Hija hajui maana washamba ni wengi.

Mhe. Mwenyekiti kinachotakiwa kuzungumziwa sisi ni mambo yanayohusu ajira na mishahara. Haya ni mambo ambayo Wazanzibar wenzetu wanayasikia, haya mengine ni yenu nyinyi wataala katika kutega uchumi, sasa mara nyengine mnapoandaa vitabu hivi lazima muwe na hadhari sana kuona kwamba munazungumza nini katika Baraza. Haya hamtupi semina, hatuna mikutano, hatuna chochote nyie mkifika hapa mnajaza tu angalau vitabu vyenu viwa na kurasa arubaini mpaka hamsini. Mtwambie kitu ambacho tunakielewa kwa sababu sisi tunashughulikia uchumi wa wananchi sasa kama uchumi wa wananchi tunauzungumzia nje kwamba tunapunguziwa kodi hebu tuulizane sisi tunapeleka nini kule? Tulikuwa na mazao ya pili pili hoho, serikali imesahau kwamba yalikuwa yapo, tulikuwa tunauza mbata nje sasa hivi hatuna, mikarafuu inakufa hatuimarishi. Kazi yenu ni kupanda ndege na kwenda kwenye mikutano mikubwa mkatutungia vitabu.

Mhe. Mwenyekiti tunataka mageuzi ya kiuchumi ambayo yanaweza kuzalishwa na wananchi wenyewe hapa paha Zanzibar na haya hamuyafanyi tusipambe kitabu, tunataka kufanya mageuzi ya kiuchumi tuna sema tuna bahari kuu waleteni wawekezaji na katika hiyo miradi minne ambayo mlizungumza kwamba mliipeleka huko basi ingekuwa umo uvuvi wa bahari kuu tungeona afadhali mnazungumza kitu, kwa sababu sisi bahati kuu tunayo lakini mnatuletea mambo ya ajabu ajabu, tuna masoko ya pamoja, tuna masoko ya SADEC hayatuondoi katika umasikini haya, lazima tuone kwamba

tunayafanya mambo ambayo ndani ya familia zetu wanafahamu tunafanya nini?

Mhe. Mwenyekiti ukurasa mwengine niliotaka kuchaniga kwa muda mrefu serikali imekuwa inapiga kelele kwa mishahara hewa, mishahara hewa ndio inayofanya serikali isiongeze mishahara lakini muda huo ilikuwa mishahara hewa imekithiri hapa nchini, sasa ilikuwa cha kutwambia kwamba sasa hali imefikia vipi haya ndio mambo ya kuzungumza ndani ya nchi yetu sio mengine. Sasa pamoja na kuwa ni mchango lakini nakuuliza Mhe. Waziri mishahara hewa sasa hivi imedhibitiwa kwa kiwango gani?

Si muda mrefu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa inanuka kwa wafanyakazi hewaa . Ajira za kitoto toto mtu kafa juzi leo anaajiriwa mjukuu wake kwa njia ambayo maafisa wanajipatia mapato, sasa mnadhibiti vipi kwa sababu ndio mnasema mmewapa mafunzo watu juu ya kuona kwamba hali ya udhibiti wa hizi pesa na mambo mengine yanakwenda vizuri. Je, bado iko pale pale au hali inakwenda vizuri kama ilivyo?

Mhe. Mwenyekiti Idara ya Utumishi Serikalini hii nasema haikujipanga vizuri katika kuzuia kuajiri wananchi hivi sasa maeneo mengi ya hatari yanahitaji watu waajiriwe na ajira hazitoki mfano mzuri tu vituo vya hospitali, kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi hata wa chini. Tatizo hili kubwa linawafanya watu wasumbuke sana na bado serikali inasema ata tumezuia! Sasa twambieni mmezuia kwa nini? Kwa sababu haiwezekani kwamba gari zipo hospitali lakini dereva hamna, hivyo dereva anatakiwa awe na utaalam gani si ile kujua tu njia, hii pita kushoto na hii kulia, kama tungelikuwa na nia ya kupunguza serikali kuwa kubwa basi na sisi tuambizane kwa mfano ukienda pale Kivunge ndio nilipokuwa na uzoefu napo sana unaweza kupata tabu sana kuhusu huduma hata wale ma- *orderly* pia nao hawaajiriwi!

Sasa sijui Mhe. Mwenyekiti lengo la serikali lipi kupunguza ukubwa wa serikali au kuona kwamba bado wanafanya *scheme of service* kila mtu awe na eneo lake. Lakini bado tunasema kwamba serikali katika maeneo mawili izingatie, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejitahidi bila ya mwalimu huwezi kufanikiwa kumsomesha mtoto. Lakini na kule Hospitali kama hakuna wahudumu na madaktari basi tatizo kubwa, kwa hivyo katika eneo hili la afya muangalie sana kuona kwamba munawaajiri watu japo kwa kiwango ambacho sicho kinachofikiriwa na wananchi hili muhimu na nimetumwa hasa, kwa sababu hili tatizo kubwa sana lazima tulione na lazima tuseme tusiseme mambo ambayo petu hayapo hayatukeri sana wala hayatuathiri.

Lakini sasa nije katika Idara hii ya Utumishi utaambiwa ajira hamna lakini watoto wa wengine wangu mimi hamna maana nimemtafutia udereva pia hajapata, watoto wengine wanaajiriwa sijui kwa utaratibu gani nchi yetu, serikali yetu wenyewe sio kwamba yetu sisi CCM tu na wale wenzetu lakini hata sisi tunapiga kelele kwa hili, kwamba ajira hizi zinatoka ndivyo sivyo, leo hapa Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alihojiwa juu ya kuwapeleka wale watoto wa kuwasomesha wenye sifa na wasio sifa. Kuna siku nitaomba serikali iunde tume yale kweli yaliyozungumzwa na Mhe. Hijja Hassan Hijja, lazima tusafishe makosa yetu ndani ya serikali ili tuonekane kwamba sisi sio wabadhilifu ndani ya nchi hii.

Isiwe huyu anajuzi anaachwa lakini asiye ujuzi anapelekwa itakuwa ni ulalamishi sawa sawa na mchezo wa karata, kwa hivyo tuone kwamba tunayafanya mambo tujuane kwamba sote Wazanzibar. Tunayo haki kwa mujibu wa Katiba watu wote sawa mbele ya sheria, lakini pia wanaambiwa wanazaliwa huru na sawa. Sasa tuone kwamba huyu sio mtoto wa Ali Abdalla huyu sio mtoto wa Mzee Ali Ussi, tuone kwamba Uzanzibar wetu unafanya mambo yanayolinganisha na kutuweka sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti wenzetu wamesema kwamba tumetoka mbali katika mvutano wa kisiasa na mambo mengine ili kuleta umoja wa kitaifa kuondoa mifarakano, ni jambo zuri japokuwa mimi linanitia shaka, kwa sababu ulikuwepo muwafaka wa Mhe. Haji Mkema hapa ukenda kenda kidogo haukufika pahala, tukafanya muafaka wa pili yule aliyetia saini sikumjua nani kwa sababu nilikuwa nje na watu walikuwa wanatia saini ndani Ikulu, lakini bado nauliza tunaweza? Kwa sababu kinachokosekana hapa Mhe. Mwenyekiti ni uvumilivu wa kisiasa, atatokea mtu atie fitina huko basi ukija hapa yule mwenziyo aliyeambiwa vile kavimba mashavu hakusemeshi wala hacheki, au akisikia dogo tu *allahuakbar* namnukuu mwana falsafa mmoja hapa tulikuwa tunamuita Waiseman.

Mhe. Mwenyekiti, watu wa mwanzo walioishauri CUF kwamba tumtambue Rais ni Mhe. Abass Juma Mhunzi lakini wakati ule CUF juu haijataka jambo lilikuwa gumu na alisema mtamalizika kisiasa nafikiri anabashiri yule jamaa, lakini jamani hebu tuacheni hizi mbwembwe za kisiasa tuendeni lakini nafikiri Mhe. Abass Juma Mhunzi alisikia huko huko Baraza Kuu akashindwa kulidhibiti. Sasa najua mpaka hivi sasa madam limetoka vile vile basi lilikuwa hili jambo lipo. Lakini kwa nini tunachelewa kutoa maamuzi hii nchi yetu viongozi wetu wanasikiana lakini sisi watu wa chini ndio tunakuwa wakaidi kwa nini maana kila mtu anakuwa anataka apate sifa nzuri kwa kiongozi wake hili jambo ndio baya, utajua hili gumu lakini tunafanya.

Mimi sikufukiria kama rafiki yangu Mhe. Juma Duni Haji anaweza kutoa kauli kama hizi kwa sababu kwa nje maana kwa ndani nilikuwa sijasikia nimemsikia mtu madhubuti sana katika chama huyo akisema hapa hapana basi hapana, lakini kwa vile anavyosisitiza tokea juzi najaribu kumpeleleza sana basi naona hili jambo ni zuri na huenda likawa. Lakini sasa tunachohisi uvumilivu wa kisiasa lazima uwepo na katika uchaguzi kuna mambo mawili lazima ukubali matokeo, sasa mimi naomba sana kwa sababu tunajua CCM tunashinda lakini mukubali matokeo wakati CCM imeshashinda tena isiwe huko mbele tunakwenda kuharibu hali ya hewa.

Kuna jamaa mmoja hapa kasema mwaka 2005 mishahara ilivuka muda ni kweli kwa sababu mimi nimeanza kujiunga na Baraza hili mwaka 1995 pamoja na Mhe. Moh'd Ali Salim, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Muhidin Mohammed Muhidin ni kweli kwa sababu tulikuwa na mvutano wa kisiasa humu ndani ya nchi na nnje ya nchi, kwa hivyo wakati ule halaumiwi Dk. Salmin Amour wala nani kwa sababu ndani ya mvutano wa kisiasa na hasa mfumo ulikuwa mpya kwa hivyo serikali haikuwa na kosa kufanya vile, kwa sababu sisi wenyewe ndio tuliopeleka fitna nje tumekosa misaada na mambo mengine na wele Wazanzibar wenyewe wengine walikuwa wabaya, kwa sababu zile kodi ambazo zinakusanywa pale bandarini na sehemu nyengine zilikuwa hazipatikani ilikuwa ni uchumi huru kila mtu anatia mfukoni mwake.

Sasa lazima tuondoe mfarakano kweli ili tuone kwamba tunaimarisha siasa na uchumi maana vitu viwili hivi haviendi kila kimoja pake vinakwenda kwa pamoja, hizi ghasia unazoona zote hizi ukimwambia mtu si mjumbe wewe anakuwa kimya na mnyonge. Hasemi kwa sababu ile nguvu yake ya kujipalilia haipo na mimi nasema sana hapa kwa sababu najipalilia huko jimboni. Sasa hivi siasa haziendi peke yake siasa inakwenda na uchumi na hao unaowasikia wanawanywa hao katika nafasi za urais katika pande zote mbili kila mmoja anaomba dua awe Rais awe Makamo wa pili wa Rais kwa chama chake kinachoshinda au awe Makamo wa Kwanza wa Rais kwa sababu utaratibu unabadilika.

Lakini hao hao ukiwaambia huuziki na huna sifa atatugeuka humu humu kwa sababu siasa inatengeneza mazingira ya uchumi sasa hili lazima tujuane, hivi sasa watu wanaanza kuchukuana humu humu Barazani akisikia unazungumza na Shamhuna ameshaanza nongwa , yule anasema na mzee wangu hapa nongwa, kwa sababu kila mmoja anahisi kwamba akipata fulani mimi nitakuwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba umalize.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti tumepewa dakika kumi na tano , mimi mwenyewe binafsi baada ya kupata maelezo mazuri kuhusu jumuiya ya SADEC na Soko la Afrika ya Mashariki, basi nitaunga mkono sasa hivi bado lakini nitaunga mkono mia kwa mia. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe utaratibu wetu tulivyojipangia majadiliano yanaendelea mpaka jumatatu lakini mpaka sasa hivi nina jina moja tu la Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa hivyo majina ningeomba yaletwe ili tuendelee kwa siku ya jumatatu. Kwa leo naomba nimalizie hapa.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/06/2010 Saa 3.00 asubuhi)